MYRTLEFIELD
HOUSE

# Lulu za Biblia

# Myrtlefield Encounters

*Myrtlefield Encounters* ni masomo ya vitabu vya Biblia yanayosaidia kuielewa Biblia kwa ujumla wake. Masomo haya yanavihusu vitabu vya Biblia, mafundisho ya Kikristo na utetezi wa imani. Katika mfululizo huu vitabu vinatoa changamoto kwa fikra za waamini na wasioamini. Vinaonesha jinsi Mungu alivyonena katika Biblia ili kutoa jibu kuhusu maswala yanayojitokeza kila siku, yenye utata, uzuri na nafasi zilizopo ndani ya maisha.

# Lulu za Biblia

*Dhana halisi za Biblia*

David Gooding

John Lennox

Kanisa la Biblia Publishers | Myrtlefield Encounters

Copyrights:

© 1997, 2013 for English Edition *Key Bible Concepts*, Myrtlefield Encounters, Myrtlefield Trust, Coleraine, N Ireland

© 2014 for Swahili Edition, Myrtlefield Encounters, Myrtlefield Trust, Coleraine, N Ireland

**Published and distributed by**

Kanisa la Biblia Publishers

P. O. Box 1424, Dodoma, Tanzania

1st edition 2014  2.000 copies

Toleo la Kiswahili limetafsiriwa na Mecka Ogunde, Dorothy na Hugh Prentice.

Madondoo ya Maandiko Matakatifu katika maelezo yote yanatoka katika Biblia. Revised Union Version, Toleo la 2006, lililotolewa na Chama cha Biblia cha Tanzania, S.L.P. 175, Dodoma, Tanzania.

ALL RIGHTS RESERVED – HAKI IMEHIFADHIWA

Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kuhifahdi kwa njia yoyote ile au kutoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote pasipo idhini ya Kanisa la Biblia Publishers.

Cover Design: Mathias Havemann

Cover: Mathias Havemann

Printed by: www.cleftrockindia.com, India

ISBN: 978 9976 74 074 5

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| 1 | Utangulizi | 1 |
| 2 | Utakatifu: Utukufu, Usafi, Uzuri na Upendo wa Mungu | 10 |
| 3 | Dhambi: Ugonjwa, Dalili Zake na Tiba Yake | 19 |
| 4 | Upatanisho: Njia ya kuifikia Amani | 27 |
| 5 | Kuhesabiwa Haki: Kuweka Mambo Sawa Kisheria | 36 |
| 6 | Fidia na Ukombozi: Gharama ya Uhuru | 45 |
| 7 | Uzima wa milele: Mahali hapa na Wakati huu | 53 |
| 8 | Toba: Ni Zaidi ya Majuto | 61 |
| 9 | Imani: Siyo kuthubutu kuruka bila kuwa na uhahika wa wapi kutua | 69 |
| 10 | Imani: Kuitikia Ushahidi uliopo | 77 |
| 11 | Imani: Unamwamini Nani? | 93 |
| 12 | Utakaso: Mtoto wa Simba ni Simba | 101 |
| 13 | Utakaso: Uwana Wala Si Utumwa | 110 |
| 14 | Hukumu ya Mwisho: Kutaka Haki Itendeke | 118 |
| 15 | Hukumu ya Mwisho: Wema na Ukali wa Mungu | 127 |
| 16 | Wokovu: Neno Linalojumlisha Yote | 136 |
| | Marejeo ya Biblia | 145 |
| | Kuhusu Waandishi | 152 |

# Sura 1

## Utangulizi

Hakuna awezaye kujiita ameelimika kwelikweli asipokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu Biblia. Tangu zamani mpaka sasa, Biblia imekuwa na bado ina mchango mkubwa katika tafakuri za dunia. Ilikuwa ni kitabu mashuhuri cha kwanza kuchapishwa na cha kwanza chenye kupigwa chapa katika mfumo wa herufi zihamishikazo. Tafsiri ya Kilatini ya Biblia ilipigwa chapa katika kiwanda cha chapa cha Gutenberg, huko Mainz, Ujerumani, mwaka 1455. Hakuna kitabu kingine ambacho kimesomwa na watu wengi zaidi na kupigwa chapa katika lugha nyingi zaidi kuliko Biblia.

Kadiri tunavyoisoma Biblia, ndivyo tunavyokutana na maneno na mawazo ambayo, ingawa kwa namna fulani yanatokea kuwa yamezoeleka, lakini hatutayaelewa mara tu tunapokutana nayo kwani maneno haya yanatumika kama maneno ya kitaaluma. Hili lisitukatishe tamaa — bali badala yake, liongeze nia zetu. Katika dunia hii ya leo, sasa au baadaye, tutapaswa kujifunza maana ya maneno ya kiufundi katika nyanja moja au nyingine za maarifa. Mtu anapofahamu maneno hayo ndipo anapopata nia sahihi. Msichana ambaye anataka kuwa mpishi mzuri ni lazima ajifunze tofauti iliyopo kati ya kuchoma, kubanika, kukaanga, kuvukiza na kuchemsha, na kwa nini angetumia njia mojawapo kati ya hizo, kuandaa baadhi ya vyakula na njia nyingine kwa

vyakula vingine. Mvulana mwenye lengo la kuwa fundi wa magari ni lazima aelewe pistoni ni nini, na kabureta, na silinda; na tofauti kati ya injini ya petroli na injini ya dizeli; pia klachi, gia, na akselereta na kazi zake. Nasi sote ambao tunataka (au kulazimishwa!) kujifunza matumizi ya kompyuta kwa sababu zozote zile, tunajikuta tukikabiliwa na mlolongo mrefu wa maneno ya kiufundi tunayohitaji kuyamudu vema.

Kama ilivyo kwenye medani nyingine, ni hivyo pia katika kushika maneno ya kitaaluma yanayotumika katika Biblia; na pia hutufanya tupate kuelewa kwa kina kuhusu maneno hayo. Aidha, uwezo wa kueleza maana ya maneno hayo huongezeka kwa wanafunzi katika madarasa yetu, hivyo kuwafungulia madirisha juu ya ulimwengu mzima wa kisasa.

Hivyo katika sura chache hizo tutakuwa tukijifunza maneno hayo ya kitaaluma, na katika sura hii ya utangulizi tutachunguza kwa ufupi misingi ya yale tunayotarajia kuyapitia.

## Utakaso

Mahali pa kuanzia kwa kutumia mantiki hii ni neno **Mungu**. Kwa sababu mojawapo ya maneno muhimu ambayo humwelezea Mungu ni neno “mtakatifu” tutaanza na neno hili. Hata hivyo, papo hapo tunaweza kukutana na pingamizi. “Simwamini Mungu,” mtu fulani aweza kusema: “hivyo sina haja na utakatifu wake, vyovyote vile linavyomaanisha neno hili. Ninaishi maisha yangu bila kumtambua mungu awaye yote.”

Vema, hizo ni kauli na madai yanayovutia sana. Madai ya kwanza na ya pili yanaweza kusadikika, lakini yale ya tatu yanakuwa na nafasi ndogo kuwa kweli. Uzito wa uzoefu wa wanadamu kwa karne nyingi za historia unakinzana na madai hayo. Hata hivyo, yote hutegemea una maana gani ukisema *mungu*. Idadi kubwa ya watu kwa miaka mingi iliyopita waliamua kukubaliana na mfalsafa wa Ujerumani aitwaye Nietzsche kwamba “Mungu kafa” na kuamua kufutilia mbali katika fikra

zao, imani yoyote ndani ya Mungu Mmoja wa Kweli. Kwa kiwango fulani wamefanikiwa, lakini imewagharimu. Kwani baada ya hapo wametambua kuwa haiwezekani kuishi ama kwa uelewa (*intellectually*) au kihisia tu kwenye dunia isiyo na uungu kabisa. Huku wakijua ama kutokujua, wamejaza ombwe (nafasi) iliyoachwa wazi kwa kumwondoa Mungu Mmoja wa Kweli kwa aina zote za miungu bandia.

Hata yule anayemkana Mungu kwa nguvu zote hawezi kujizuia kutafakari ni nguvu zipi zilizosababisha yeye na ulimwengu kuwepo, na ni nguvu zipi zitaangamiza vyote viwili mwishowe. Anaweza asiziite 'miungu,' au pengine anaweza kuziita hivyo; kwani ni nguvu ambazo humdhibiti, wala yeye hawezi kuzidhibiti. Asiyemwamini Mungu hukataa wazo la kuwepo kwa Muumba wa kwake mwenyewe binafsi. Badala yake hudhania kwamba, maada pofu na misukumo isiyo na ufahamu wala uhai ndiyo inahusika na kuwepo kwake na kuwepo kwa ulimwengu. Hivyo anaharibu mara moja tumaini lote la nia na malengo yoyote ya kuishi kwake. Lakini mwishoni hutambua kwamba hawezi kuishi tu bila lengo lolote la kuishi kwake, pasipo jambo lolote lililo kubwa zaidi yake analopaswa kuliamini. Hawezi kuishi pasipo maadili yoyote anayopaswa kuyaheshimu, na pasipo kusudi lolote analopaswa kujitoa mwenyewe kwake, na, kama ni lazima, kufa kwa ajili yake. Kwa kuwa hawezi kuishi kwa ajili ya Mungu Mmoja wa Kweli, na kumtumikia, anaibua makusudi na malengo mengine dhaifu zaidi, baadhi yake makubwa na yenye heshima, baadhi yake yakiwa madogo na yasiyoheshimika sana. Hata kama hayaiti 'miungu' au pengine anaweza kuyaita hivyo: mwisho wake hutokea kuwa ni jambo lilelile.

Katika mkondo wa historia, watu walijifanyia miungu mbalimbali: kama vile mungu wa kike kutokana na kujamiiana (Wagiriki walimwita *Aphrodite*), mungu wa vileo (Wagiriki wakamwita *Dionysius* au *Bacchus*), mungu wa vita (kama miungu-vita wa Wajerumani iliyowahamasisha sana siku zilizopita), mungu wa pesa, wa starehe, wa umaarufu, mungu wa taifa au

hata mtu mwenyewe kujiita mungu (kama jinsi watawala wa kiimla wengi walivyojifanya). Anapokabiliwa na mabadiliko ya maisha yasiyotarajiwa, mtu wa kawaida asiyemwamini Mungu mara nyingi hufikia uamuzi kwamba kila jambo linatokea kwa bahati na akiwa ananunua tiketi ya bahati nasibu anatumaini kwamba Bahati Nzuri itamfurahisha. Wagiriki wengi wa kale pia walidhania hivyo, kiasi kwamba wakatengeneza mungu wa kike na kumwita Tyche. Wanasayansi wanaofuata nadharia ya wanamageuzi (*evolutionists*) wa kale na wale wa sasa pia hushikilia kwamba bahati nasibu ndiyo msukumo unaosababisha kuwepo kwa wanadamu duniani. Aidha, wapo wengine wanaochukua mtazamo wa tofauti, kwamba wanadamu ni mashine tu wasiokuwa na hiari, na kwamba utashi wa binafsi ni fikra potofu. Watu wa kale walikuwa na jina kwa ajili ya hilo pia. Waliliita Majaliwa (*Fate*), nalo wakalifanya mungu.

Uzoefu katika karne nyingi umeonesha kwamba suala si iwapo utamwamini Mungu au la, bali iwapo utaamini katika Mungu Mmoja wa Kweli anayesema kuwa alikuumba wewe mwenyewe, au utaamini wingi wa mambo haya mengine ambayo umeyafanya kuwa miungu badala yake.

Basi, tutaanza kwa kujifunza Biblia inamaanisha nini inapoongelea utakatifu wa Mungu Mmoja wa Kweli. Hata asiyemwamini Mungu anaweza kuona kuwa Biblia inatoa maelekezo akilinganisha tabia na sifa za Mungu na zile za miungu bandia.

## Dhambi

Kwa kweli, mara mtu anapokiri uwezekano kwamba sisi wanadamu tumeumbwa na Mungu Mtakatifu anayetafuta uhusiano na sisi binafsi, ndipo haitachukua muda kabla swala la **dhambi** halijajiingiza kwenye mjadala. Watu wote wenye akili timamu wanapingana na makosa ya jinai, na hukubali kabisa kwamba inabidi yashughulikiwe kwa haki na kwa makini. Kwa

ajili hiyo, kuna magereza na taasisi za kuhudumia wagonjwa wa akili. Walakini wahalifu si zaidi ya asilimia ndogo sana ya idadi kamili ya watu. Ukweli muhimu zaidi ni kwamba kila mmoja wa watu si mkamilifu wa kimaadili, iwe kwa kiwango kikubwa au kidogo ama kwa wakati mmoja au mwingine. Kwa hakika wahalifu husababisha uharibifu na usumbufu mwingi. Kwa upande mwingine mtu wa kawaida mara nyingi huathirika kutokana na uchoyo, kinyongo, na kukosa kuwa makini kitu ambacho huwafanya hata marafiki zake wa karibu kupata ugumu kuishi naye nyakati zingine; kutokana na kukosa uaminifu, chuki, msongo wa mawazo, ukatili ambavyo huvunja familia, husababisha talaka, na kuumiza nafsi za watoto. Ni somo lililo wazi la historia kwamba katika nchi nyingi kwa karne nyingi idadi kubwa ya watu wameathirika kutokana na ahadi za uongo za wanasiasa, falsafa za uongo na uonevu wa ngazi za juu zaidi kuliko wanavyoumizwa na wahalifu ambao serikali hizo zimewatupa magerezani.

Basi, hiyo imekujaje, kwamba sisi sote, kwa ujumla wetu, tuna upungufu kimaadili? Je, tulaumu asili yetu au hitilafu ya kinasaba (*genes*), tuseme kwamba hatuwezi kuepuka makosa, tuyakane majukumu yote kwa mienendo yetu, na tujigeuze kuwa mashine? Jambo hili ni hakika: tusipoweza kupata majibu yanayotosheleza na ya kweli ya hali yetu mbaya kimaadili, hatutakuwa na tumaini halisi la kujiboresha, wala hata la kujitibu.

Kwa hiyo, tutajifunza majibu ya Biblia juu ya nini kisichokuwa sawa kuhusu mwanadamu. **Dhambi** ni neno la jumla ambalo Biblia inalitumia kumaanisha chanzo cha msingi wa ugonjwa wenyewe na pia matokeo yake. Lakini neno la ujumla 'dhambi' hujumuisha vipengele kadhaa ambavyo Biblia huvielezea kwa maneno maalum. Dalili ambazo husababishwa na dhambi ndani ya watu vilevile hupewa majina mbalimbali. Kwa hiyo, tutajifunza juu ya chanzo chake na juu ya dalili zake pia, ili kwamba hatimaye tuweze kuamua jinsi gani mpango unaopendekezwa na Biblia ili kushughulikia dhambi ulivyo wa kweli.

## Wokovu

Neno la jumla la Biblia kwa ajili ya mpango huo ni **wokovu**. Lakini hili ni neno linalohitaji funzo makini na la kina. Tunaweza kusema kwamba wazo la watu wengi kuhusu neno 'wokovu' ndani ya Agano Jipya humaanisha kinyume cha iliyo maana yake halisi.

Mtazamo wa watu wengi kuhusu wokovu hupunguza maana yake hadi iwe tu ushawishi wa kuishi maisha yenye maadili kiasi, na kila siku kuboresha mwenendo wa mtu. Mtu huongozwa na tumaini lisilo na uhakika wa kwenda mbinguni wakati huohuo akiwa na hofu ya kuishia jahanamu. Tatizo ni kwamba kwa watu wengi inaonekana wazi kuwa ni sawa. Ikiwa unataka kwenda mbinguni, wanadai, ni dhahiri kwamba utahitajika kuwa mwema. Kama wewe si mwema, ni dhahiri kwamba hutafika mbinguni. Na hivyo wameweka wazo hili kwenye akili zao kiasi kwamba hawaoni umuhimu wa kusoma Agano Jipya ili kufahamu linasema nini. Wanadhani tu kwamba litasema kile wanachotarajia liseme.

Bali ukweli ni kwamba Agano Jipya hufundisha mtazamo ulio kinyume cha mtazamo huo wa kawaida. Neno lake 'wokovu' si jina lingine tu la kanuni ya maadili ambayo tunapaswa kuishika ili kupata kukubalika kwa Mungu na kupata nafasi kwenye mbingu yake. Neno 'wokovu' kwa hakika humaanisha linachokisema. Thamani ya sura yake ni thamani yake ya kweli. Ni tendo la uokoaji ambalo Mungu hutekeleza kwa ajili ya wale ambao wasingeweza kujiokoa wenyewe, hata wangejaribuje, wasingeweza. Sio ushauri wa jinsi ya kufanya matendo mema ya kujitosheleza ili kufaulu kuingia mbinguni. Agano Jipya linatangaza kwa uwazi na kujirudiarudia kwamba wokovu sio kwa matendo yetu: ni zawadi ya Mungu kwa wale ambao wasingeweza kuulipia, wala hawakuustahili.

## Maana ya Wokovu

Yafuatayo ni maneno ambayo Agano Jipya hutumia (na ambayo baadaye tutajifunza) kuelezea vipengele mbalimbali vya wokovu.

Neno la kwanza ni **Fidia**, neno hili linaashiria gharama ambayo Mungu tayari ameshalipa – siyo ambayo sisi tunapaswa kulipa – ili kwamba atuachilie huru toka kwenye kifungo cha kimaadili na kiroho. Neno la pili ni **Kuhesabiwa haki**. Jambo hili pia, ni kwa neema ya Mungu wala si kwa matendo wala ustahili wetu. Na matokeo yake ni kutufanye wenye haki mbele za Mungu na kutupa amani naye hapa na sasa.

Mtu **aliyehesabiwa haki** anaweza kuishi maisha yake kwa furaha na kujiamini kwamba tayari ameshakubalika kwa Mungu. Hiyo ni tofauti, na kuishi maisha yetu bila uhakika kama baada ya kifo tungekubaliwa na Mungu au tusingekubaliwa. Neno la tatu ni **upatanisho**, neno ambalo pia tutajifunza, litasisitiza ukweli huo. Kazi ambayo Kristo amefanya ni kutimiza upatanisho kamili kati ya Mungu na mwanadamu, ili kwamba hapa na sasa katika maisha haya tuweze kuunganishwa kwenye amani na ushirika pamoja na Mungu.

Hii hutusaidia, hapa na sasa, kuumiliki na kuufurahia **uzima wa milele**. Maana 'uzima wa milele' sio maisha ambayo kwayo watu huingia mara tu baada ya kifo, ni tofauti na mawazo ya wengi. Uzima wa milele ni maisha ambayo tunaweza kuingia na kuyafurahia hapa katika dunia hii. Tunahitaji kuyaingia sasa, la sivyo hatutayaingia kamwe katika ulimwengu ujao.

Walakini watu wengi, wanaposikia kwa mara ya kwanza mtu akifafanua mafundisho ya Agano Jipya kuhusu wokovu kwa jinsi hii, hudhani ni uongo dhahiri, au pengine upuuzi. Wanasema, awali ya yote, jitihada zote za dhati za kujiboresha zinakatishwa tamaa. Hivyo wanadai, wokovu uwe ni matokeo ya matendo mema yaliyofanywa, na sio tu zawadi wapewayo watu bila kuzingatia iwapo wametenda mema au mabaya, eti tu kwa sababu wanadai kuamini. Wanahoji, kama mtu angeweza kuwa na hakika kwamba alikuwa tayari ameokolewa "kwa imani wala si kwa matendo," hiyo ingemaanisha kwamba angeweza kuishi maisha yake yaliyosalia bila kuwajibika kimaadili, na bado mwisho wake akaokolewa. Jambo hili linakosa maana kimaadili.

Ni dhahiri kwamba, vipingamizi hivi vina msukumo fulani wa juu juu tu. Vipingamizi hivi vinatokana na kutokuelewa na mara vinatoweka pindi mtu anapofungua Agano Jipya na kusoma nini hasa linachokisema. Hakuna kitabu duniani ambacho kinahimiza utakatifu zaidi ya Agano Jipya linavyofanya. Kwa hiyo, somo letu la '**utakatifu**' litanuia kutambua nini Agano Jipya humaanisha kwa neno hili; nini Agano Jipya linaitambua kuwa ni nia pekee inayokubalika kwa kuwa mtakatifu (ambayo ndiyo sababu linashikilia msimamo kwamba wokovu lazima uwe zawadi wala sio malipo kwa ajili ya kuwa mtakatifu). Ni nguvu gani Agano Jipya linawapa watu ili waweze kuishi maisha yenye uzuri kamili.

## Masharti ya Wokovu

Agano Jipya linasema, nguvu hiyo ipo kwa masharti mawili, sharti la kwanza ni **toba**. Maana ya neno hili yaweza kuonekana kuwa dhahiri. Hata hivyo, tutatambua kwamba kwenye Agano Jipya hilo neno mara nyingi hubeba maana nzito zaidi kuliko inavyokuwa katika maongezi ya kila siku.

Sharti la pili ni **imani**. Lakini hili, watu wengi huhisi, ni eneo dhaifu kabisa la Ukristo. Wanasema, "Dini zote hutegemea imani, ila sayansi hujishughulisha na uthibitisho. Kwa hiyo sayansi ina misingi imara. Inaweza kuthibitishwa kuwa ukweli. Ukristo hauwezi kuthibitishwa kuwa ukweli, na kwa hiyo hauna msingi wa kutegemewa kabisa."

Bali watu hao husahau kwamba sayansi yenyewe kimsingi inategemea imani, na kwamba nadharia zilizo nyingi na fasiri zake za sasa za ulimwengu hazitokani na vithibitisho bali fikra za kifalsafa wanazodhani wanasayansi. Wanasahau pia kwamba mahusiano yote kati ya watu hutegemea imani mwishowe. Kwa sababu Mungu wa Biblia anatamani uhusiano wa binafsi wala yeye si nguvu fulani isiyo ya karibu, uhusiano wetu na yeye kwa vyovyote hutegemea imani. Swali halisi ni: Agano

Jipya linamaanisha nini juu ya 'imani'? Jambo moja tutatambua kwa uhakika zaidi ni kwamba halimaanishi kuamini jambo lisiloonekana bila ushahidi. Biblia inatoa ushahidi tele ili kuweka msingi kwa imani yetu.

## Hukuma ya Mwisho

Na mwisho, tutachunguza Biblia inamaanisha nini kusema **mauti ya pili**. Katika jambo hili Biblia humaanisha kile ambacho katika lugha ya kawaida huitwa jahanamu. Basi kwa watu wengi neno 'jahanamu' huwaletea picha ya mashetani yakiwazoa watu na kuwarusha kwenye tanuru la moto, na wanaliona wazo zima kama dhana za ushirikina. Hata hivyo wazo hilo ni mbali sana na maana ya 'mauti ya pili' katika Agano Jipya. Kwa kweli Biblia inafundisha kwamba Mungu ni lazima Mungu aadhibu dhambi, siyo tu kwa sababu yeye ni mtakatifu na mwenye haki asiyebadilika, bali pia kwa sababu yeye ni pendo lisilotetereka. Hakuna mtu anayewajibika kimaadili kwenye jamii iliyostaarabika anayeshikilia kwamba makosa ya jinai yaruhusiwe kuendelea bila kukomeshwa wala kuadhibiwa. Mungu anashikilia msimamo kama huo pia kuhusu dhambi.

Katika makala hizi hatutakuwa na kawaida ya kuweka aya ndefu za Biblia, bali tutafanya marejeo. Tunapendekeza kwamba itakuwa vema kutazama kila aya, kuisoma kwa sauti na kuona ni jinsi gani inavyosaidia kuthibitisha maelezo yanayotolewa kwenye kitabu hiki.

# Sura 2

## Utakatifu

### *Utukufu, Usafi, Uzuri na Upendo wa Mungu*

Haipingiki kuwa watu wengi hawapokei wazo la kwamba Mungu yupo na kukumbushwa kuhusu utakatifu wake ni tishio kwao. Mungu kwao ni kama chukizo, mdhalimu mwenye enzi aliyejizatiti kuzuia uhuru wa mwanadamu na kumnyima maisha yenye raha isiyo na mipango. Watu hao hujifariji kwamba fikra ya kuwepo kwa 'Mungu' ni mabaki ya mawazo yaliyoaminiwa kabla ya maendeleo ya sayansi, na wanajaribu kumwondoa kutoka katika akili zao (japo bila mafanikio).

Yote haya, hata hivyo, yanakinzana na jinsi watu katika Biblia wanavyojisikia na kufikiria kuhusu Mungu. Wanamwelezea Mungu kama furaha na shangwe yao (Zaburi 43:4); na wanatangaza kwa ujasiri wanachokiita sifa zake. Kwa kweli wanazungumzia kumcha Mungu, katika namna ya kumtii na kuzidi kumheshimu. Hata hivyo, hisia na hali hizo hazitokani na hofu, kama ya mtumwa mwenye woga uliokithiri. Bali kujisikia hivyo ni mwitikio thabiti wa viumbe wenye akili waliokutana na utukufu, uweza, na usafi wa Muumba wao mwenye enzi. Hata wanasayansi wasioamini kuwepo kwa Mungu wakati mwingine hustaajabishwa na kiwango cha ukubwa wa anga na ugumu wa kuelewa kwa ulimwengu,

pamoja na uzuri wake unaopendeza sana. Mathalani ni wazazi gani ambao hawajawahi kushangazwa wala kustaajabishwa na vidole vidogo vya watoto wao wachanga, vikikamilishwa na kucha ndogo! Kwa hiyo si jambo la kushangaza, kukuta wanaume kwa wanawake katika Biblia wakiitana kwa moyo wote kumwabudu Bwana kwa uzuri wa utakatifu (taz. 1 Nyakati 16:29).

## Uhusiano kati ya Mungu na uumbaji wake

Basi awali ya yote, utakatifu wa Mungu ni njia ya kuuelezea uhusiano kati ya Muumba na ulimwengu ulioumbwa na viumbe vyake vyote, akiwemo mwanadamu. Hii huashiria kwamba:

1. Mungu hujitegemea na hujitenga na ulimwengu. Yeye si sehemu yake. Si mmoja kati ya misukumo (*forces*) yake: wala yeye si mkubwa katika hiyo misukumo. Aliiumba misukumo: hakuna mtu wala kitu kilichomwumba yeye. Alikuwepo tangu mwanzo bila kutegemea uwepo wa chochote. *"Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye"* (Wakolosai 1:17). Yeye huushikilia, huuimarisha, na kuuongoza ulimwengu: hakuna wa kumshikilia (taz. Isaya 46:1–7). Yeye si Mungu mkuu miongoni mwa jopo la malaika (ingawa wapagani wakati mwingine wamemwongelea kwa jinsi hii). Malaika hawako katika uungu kama yeye. Wao ni viumbe; yeye ni Muumba. *"Hakuna aliye mtakatifu kama Bwana: kwa maana hakuna yeyote ila wewe"* (1 Samweli 2:2).

2. Mungu pekee ndiye muumba wa ulimwengu. Hakukabidhi suala la uumbaji wa ulimwengu na vitu vilivyomo kwa miungu ama wakala fulani, kama dini zingine zinavyoona. Yule Neno, ambaye kwake, vitu vyote vilifanyika, na pasipo huyo hakuna kilichofanyika, alikuwa ndiye yeye Mungu (Yohana 1:1–3). Nchi na mwanadamu sio uumbaji hafifu uliofanywa na miungu hafifu. Bali nchi na mwanadamu wana heshima ya kuumbwa kwa tendo la hiari la Muumba pekee wa vitu vyote, ambaye ni mtakatifu katika yote. *"BWANA, Mtakatifu wa Israeli, na Muumba wake, asema*

*hivi. . . Mimi nimeiumba dunia, nimemhuluku mwanadamu juu yake; Mimi, naam, mikono yangu mimi, imezitanda mbingu, na jeshi lake lote nimeliamuru. . . Maana BWANA, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu. . .* [anasema,] *Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine"* (Isaya 45:11, 12, 18).

3. Kama Muumba wa mwanadamu, Mungu ana haki zote za kuabudiwa na mwanadamu. Mwanadamu si tu aliumbwa na Mungu, bali pia aliumbwa kwa ajili ya Mungu. *"Wala hawapumziki mchana na usiku wakisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja. . . Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa"* (Ufunuo 4:8, 11). *"Mwabudu Bwana Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake"* (Mathayo 4:10 kwa kunukuu Kumbukumbu 6:13).

Hapa ndipo heshima na utukufu wa mwanadamu hupatikana. Maisha na kazi ya binadamu sio bure wala upuuzi mtupu kama wanafalsafa walivyofundisha wanaofikiri kwamba mwanadamu ndiye chanzo cha maarifa yote (*existentialism*). Kutenda yaliyo mapenzi ya Muumba humpa mwanadamu lengo pekee linalokidhi akili, hisia, na juhudi zake.

Hapa pia hupatikana uhuru wa mwanadamu. Kumcha yeyote, au chochote, zaidi ya Mungu, mwisho wa yote huifikisha nafsi ya mwanadamu katika utumwa na kutoheshimika. Wakristo wa kwanza walikabiliana na serikali za kiimla zilizowataka kumwabudu Mkuu wa Dola. Lakini mitume waliwafundisha kutoiogopa serikali, bali kumtakasa Kristo Bwana mioyoni mwao (1 Petro 3:14–15). Hii ina maana kuwa, daima iliwapasa kuuweka ufahamu wa utakatifu wa Mwana wa Mungu katika vilindi vya mioyo yao. Pia iliwapasa kufahamu kuwa Yesu ana haki ya kuabudiwa. Kwa kukumbuka utakatifu wake walipata ujasiri wa kukataa madai ya serikali zao za kiimla, za kuabudu sanamu. Kwa kujitoa maisha yao, waliweza kupigania uhuru wa roho ya mwanadamu.

## Nuru ya Utakatifu wa Mungu

Kumwita Mungu Mtakatifu pia ni namna ya kuurejea usafi wa ajabu na uliotukuka wa Mungu. "*BWANA ni mwenye adili. . .* [wala] *ndani yake hamna udhalimu*" linasema Agano la Kale (Zaburi 92:15). "*Mungu ni nuru,*" linasema Agano Jipya, "*wala giza lolote hamna ndani yake*" (1 Yohana 1:5), si kiakili, wala kimaadili, wala kiroho. Katika maisha ya kawaida, rangi za vitu hutegemea uwepo wa nuru. Na katika hali ya kiakili, kimaadili, na kiroho ni nuru ya utakatifu wa Mungu ndiyo inayoleta uzuri na maana kamili ya maisha. Dhambi hufanya kinyume: hufumba rangi za maisha, hulemaza hisia zake za ndani, hupumbaza akili, na hupofusha roho.

Kwa upande mwingine nuru ya utakatifu wa Mungu huifunua dhambi. Wala si kuifunua tu; kwani utakatifu wa Mungu sio hali isiyobadilika tu, kama ambavyo mwamba mkubwa unakaa shambani. Bali utakatifu wa Mungu unajishughulisha kuonesha haki ya ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi ya mwanadamu. Wakati mwingine hukumu hii hujidhihirisha katika namna ambayo Mungu amefanya sheria za asili kutenda kazi. Kwa mfano, iwapo wanadamu waking'ang'ania kwenye uzinzi na uasherati watajikuta hali asilia yenyewe inawageuka na kuangamiza miili yao: *"wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao"* (Warumi 1:27). Kwa nyakati zingine, Mungu anaruhusu majanga ya kiuchumi na kisiasa kuwaadhibu wale waliomwasi yeye. Na anapofanya hivyo, Biblia inasema kwamba *"Aliye Mtakatifu hujitakasa katika haki"* (Isaya 5:16), ambapo "kujitakasa" ina maana "hujidhihirisha kuwa ni mtakatifu" kwa kuhukumu dhambi kwa haki.

Katika siku za Nabii Isaya, taifa lake lilikuwa na hatia ya uonevu na vurugu, biashara isiyo halali, ulevi uliokithiri, upotevu mkuu wa maadili, kutomjali na hivyo kumwasi Mungu. Hivyo Isaya, siyo tu alikemea dhambi zao: aliwaonya kwamba Mungu atadhihirisha utakatifu wake kwa kushusha hukumu yake juu yao na kulishusha taifa liathirike kiuchumi, kijamii, na kisiasa:

> *Na mtu mnyonge ainamishwa na mtu mkubwa amedhilika, na macho yao walioinuka hunyenyekezwa, bali BWANA wa majeshi ametukuzwa katika hukumu, na Mungu aliye Mtakatifu ametakaswa katika haki. . . Kwa sababu wameikataa sheria ya BWANA wa majeshi, na kulidharau neno lake aliye Mtakatifu wa Israeli.* (taz. Isaya 5:7–30; hasa mst 15, 16, 24)

Yatupasa kuchunguza zaidi jambo hilo. Utakatifu wa Mungu si tu unawakemea watenda dhambi wakuu. Nuru ya utakatifu wa Mungu hudhihirisha dhambi zetu hata pale tunapoona tumetenda vyema sana. Isaya huyo huyo alipooneshwa maono ya Mungu, kazungukwa na jeshi la malaika walioitana, bila kukoma, wakisema, *"Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake"* (Isaya 6:3). Isaya mwenyewe alipigwa na butwaa kwa kutambua uovu wake mwenyewe, naye akalia akisema, *"Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi"* (Isaya 6:5). Hivyo ndivyo kila mmoja wetu atakavyojisikia iwapo tungetambua uhalisia wa utakatifu wa Mungu. Uongo, unafiki, ulaghai, udhalilishaji, ufidhuli, masengenyo, kejeli, majivuno, pamoja na dhambi iwayo yote, kwa ghafla zingewekwa wazi kama mambo batili na mabaya kwa jinsi yalivyo. Na tutatambua kwa uchungu kuwa ubatili huo usingeweza kuruhusiwa kuingia, na kuchangamana na ukweli na uzuri wa mbingu ya Mungu.

Lakini hapa hapa tunakutana na fumbo kubwa. Kwenye Biblia watu waliojitambua kwa uchungu katika nuru ya utakatifu wa Mungu, ghafla walianza kunena kwa ujasiri jinsi nuru ya Mungu ilivyo ya ajabu. Hiki ni kifungu kinachoeleza hayo: *"Bali ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu: ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema,*

*bali sasa mmepata rehema"* (1 Petro 2:9–10). Ni dhahiri kwamba watu hawa wamegundua kuwa utakatifu wa Mungu si uweza tu wenye kukanusha. Bali ni uweza wenye kujenga ambao kwa upendo na rehema zake unaweza kusafisha watenda dhambi na kuwabadili kuwa watakatifu.

## Upendo mtakatifu wa Mungu na Nguvu zimpingazo

Kwenye Mambo ya Walawi 19, Mungu anawaamuru watu wake kwanza kwa kusema: *"Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa mimi BWANA, Mungu wenu, ni mtakatifu"* (mstari wa 2). Kisha akawaelezea kwa kina maana halisi ya kuwa mtakatifu kwa kuzingatia kanuni za vitendo. Na moja ya kanuni hizo ni *"Umpende jirani yako kama nafsi yako; Mimi ndimi BWANA"* (mstari wa 18). Basi, maana ya utakatifu ni upendo; na Mungu ambaye ni mtakatifu kuliko vyote, ni upendo mkuu, kwa kuwa Mungu ni pendo (1 Yohana 4:16). Sifa hiyo hiyo ya utakatifu wa Mungu inaonekana katika tangazo rasmi la utakakatifu na heshima ya jina la Mungu katika Biblia (taz. Kutoka 34:5–7).

Kwa hiyo, tunamalizia sura hii kwa kuonesha kwamba falsafa zinazopunguza utakatifu wa Muumba, matokeo yake yasiyozuilika humharibu mwanadamu mwenyewe:

Watu wasioamini kuwepo kwa Mungu (*Atheism*): Kwa kukataa kumtambua Muumba watu wanalazimika kuamini misukumo fulani ya asili isiyo na mwelekeo wala nafsi kuwa nguvu za kimsingi. Bila lengo nguvu hizo zimeumba wanadamu wenye akili na maadili, na sasa zinawadhibiti, na mwishowe zitawaangamiza. Hivyo mwanadamu ni mfungwa wa misukumo hiyo ya ulimwengu. Werevu wake hauna thamani. Amenyang'anywa sababu na malengo ya uwepo wake na ameondolewa tumaini na lengo la kuishi.

*Pantheism*: *Pantheism* inamfananisha Mungu na uumbaji. Inafundisha kwamba ulimwengu ni Mungu, dunia ni Mungu, jua ni Mungu, mwanadamu ni Mungu, wanyama ni Mungu, kila kitu ni

Mungu. Lakini ikiwa kama kila kitu ni Mungu, basi maadili mema na mabaya pia ni Mungu. Hakika hii si kweli. Mungu alipoumba dunia, alitazama kila kitu alichokifanya kuwa ni chema (Mwanzo 1:31). Mungu hapaswi kuwekwa kwenye kundi moja na uovu. Yeye ni mtakatifu. Na katika ukweli huu kuna tumaini thabiti kuwa siku moja uovu utashindwa.

Kama uovu ungekuwa Mungu, kama *pantheism* inavyofundisha, kusingekuwepo tumaini kuwa uovu utashindwa siku moja. *Pantheism* sio tu kwamba ni uongo—lakini falsafa hii, ingawa ina mvuto kwa namna fulani, ni mfumo mbaya kupita mingine kwa kuwa huleta hali ya kufikiri kuwa mambo yote ni mabaya, hivyo hakuna tumaini.

*Re-incarnationism* inaonekana kwa namna tofautitofauti: Baadhi ya dini na falsafa za kidini zinashikilia kuwa mwili na kila kitu kilichoumbwa ni mbaya sana. Zinafundisha kuwa Mungu mkuu asingeumba mwili na vitu. Kwa mujibu wao, alichokifanya kilikuwa ni kuumba miungu midogo (*lesser gods*), ambao walikuwa na uweza wa uumbaji kama alivyo yeye. Wao kadhalika waliumba miungu wengine wadogo zaidi, na hatimaye mmoja kati ya miungu hiyo, bila hekima, akaumba ulimwengu na wanadamu. Hivyo wanadamu ni mchanganyiko usiotakiwa kati ya nafsi (ambayo ni njema) na mwili (ambao ni mbaya). Mwili huambukiza na kuchafua nafsi. Mwili huvuta nafsi kuingia katika mwenendo mwovu na hatimaye unamtia mtu kwenye mateso yasiyoepukika. Iwapo mateso haya hayakuondoshwa hadi mauti yanapomkuta mtu, nafsi ya huyo marehemu italazimika kurudi duniani katika mwili mwingine. Iwapo nafsi hiyo itaendelea kuishi maisha maovu hapa duniani, itaendelea kupata mateso na kuzaliwa tena na tena. Tumaini pekee ni kwamba, iwapo kwa namna moja au nyingine, nafsi hiyo ikiweza kuondoa mateso yote na kujitenga kabisa na mwenendo mwovu, basi itaweza kurejea katika kundi la ulimwengu wa nafsi safi na hivyo kuepukana na hatua yoyote ya kuzaliwa tena kwenye mwili mpya.

Mafundisho haya yanaukosea utakatifu wa Mungu kwa namna mbili: (*a*) Kwa hakika kuna Muumba mmoja tu, si wingi wa waumbaji wadogowadogo. (*b*) mwili na uumbaji si mbaya kwa asili yake, bali ni mwema kwa asili yake, kama tulivyokwisha tazama. Matatizo ya mwanadamu hayatokani na ukweli kwamba yeye ana mwili, bali kutokana na utashi wake mwenyewe wa kutenda dhambi na kumwasi Mungu.

Kwa nyongeza, mtazamo huu ni uongo, pia ni wa kikatili sana. Unafundisha kuwa mtoto anapozaliwa na ulemavu, hii huwa ni matokeo ya dhambi za awali za nafsi hiyo zilizotendeka katika miili yake iliyotangulia. Ikiwa, baada ya hali hii ya kuzaliwa mara elfu kadhaa, mtoto atakuwa bado hajapumzika na mateso ya dhambi zilizopita, mtoto ana tumaini gani katika kuyaondosha mateso katika maisha ya sasa – achilia mbali uwezekano kwamba atatenda dhambi zaidi maishani mwake na hivyo kuongeza hitaji lisiloepukika la kuzaliwa tena.

Hivyo, mtazamo huu umekithiri uongo na ukatili. Mwanadamu hawezi kujiokoa kwa kujitesa mwenyewe bali anaokolewa kwa mateso ya Kristo:

> *Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.* (Isaya 53:5)

Hakuna haja watu kuishi kwa hofu ya mlolongo wa miungu wasiowajibika, na wakati mwingine miungu wasababishao uovu kushamiri. Kuna Mungu mmoja tu, na Mungu huyo anatupenda na amejitoa kuwa Mwokozi wetu:

> *Hawana maarifa [hao]. . . wamwombao mungu asiyeweza kuokoa. . . Wala hapana Mungu zaidi ya mimi; Mungu mwenye haki, mwokozi; hapana mwingine zaidi ya mimi. Niangalieni mimi, mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia; maana mimi ni Mungu; hapana mwingine.* (Isaya 45:20–22)

*Maana mimi ni BWANA, Mungu wako; Mtakatifu wa Israeli, mwokozi wako.* (Isaya 43:3)

*Yeye ataitwa Mungu wa dunia yote.* (Isaya 54:5)

# Sura 3

## Dhambi

### *Ugonjwa, Dalili Zake na Tiba Yake*

Si lazima mtu aishi kwa muda mrefu ili kugundua kuwa kitu fulani kinawafanya wanadamu kutokuwa sawa. Baadhi ya watoto huwa na bahati mbaya ya kugundua hili mapema wakati wa utoto wao. Yaani pale wazazi, ambao kimsingi watoto wangetegemea wawe wapole na wenye upendo, watoto wanapotenda isivyotakiwa, wazazi wanajawa na jazba na kuwatenda vibaya. Baadaye wanagundua kwamba 'hiki kitu kinachomfanya binadamu kutokuwa sawa' hakiishii kwa wazazi na familia zao tu: katika namna tofautitofauti, na kwa viwango vikubwa kwa vidogo, kila mtu hayuko sawa.

Historia inaonesha kwamba 'kitu hiki kisichokuwa sawa' kimeenea hata kwenye uhusiano wa kimataifa kwa miaka yote; na hata leo, pamoja na maendeleo makubwa na yenye manufaa yaliyofikiwa katika kila aina ya sayansi na teknolojia, kitu hiki kinajidhihirisha katika matendo yanayotisha na ya ujinga. Iwapo tu mataifa yangeweza kuaminiana na kushirikiana badala ya kushindana kwa kuendeleza rasilimali za dunia, wangeweza kuigeuza dunia kuwa paradiso. Majangwa yangewezeshwa kuzaa mazao; umaskini, njaa, na magonjwa ya kuambukizwa

yangeondoshwa; na ustawi na umri wa kuishi ungeongezeka. Lakini mambo hayako hivyo; mataifa hayaaminiani, wala kamwe hayawezi kuaminiana; na matokeo yake fedha, muda, na nguvu nyingi zinatapanywa katika kuboresha silaha za hali ya juu za maangamizi.

Yamkini si mataifa tu huenenda kijinga. Sisi sote tunatenda bila kutafakari vema; wewe, hata mimi pia. Kwa muda mfupi au mrefu, pamoja na makubaliano yote na nia zetu njema tunapaswa kukiri, kama Paulo alivyoagiza karne kadhaa zilizopita: *"kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo"* (Warumi 7:19).

Ni kitu gani basi kinachotufanya tusiwe sawa? Ni ugonjwa gani huu wa ulimwengu ambao sote tunaugua? Wataalam Wagiriki wa kale walioandika tamthilia za majonzi, Akela (*Aeschylus*), Sofoklia (*Sophocles*), na Yuripida (*Euripides*) walitafiti dalili zake na wakajaribu kutafakari chanzo chake. Wanafalsafa wa kale wa mabara mengine pia walifanya hivyo, tena hata wale wa kizazi cha sasa. Pia hata waandishi mashuhuri wengine wanajaribu kutafakari shida hii. Ni wazi kuwa kamwe hatutaweza kujielewa sisi wenyewe au dunia tunamoishi, tusipokabiliana na ugonjwa huu kiuhakika. Biblia inasisitiza kwa ujasiri na furaha kuwa tunaweza kupata ukombozi endelevu na wa kudumu kutoka kwenye shida hii; nayo inauita ukombozi huo **wokovu**. Lakini hatutaelewa wokovu una maana gani, au unafanya kazi vipi, ikiwa kama hatutaelewa neno la kibiblia la ugonjwa huu.

Neno hilo ni 'dhambi.' Ili kutusaidia kulielewa, ebu tulifananishe na ugonjwa wa kimwili. Tabibu lazima atofautishe kati ya dalili za ugonjwa na ugonjwa wenyewe na kiini kinachosababisha ugonjwa huo. Kwani ili mtu aweze kupata uponyaji, si vema kudhibiti dalili tu bila ya kuutokomeza ugonjwa kabisa. Na hakuna tumaini la uponyaji isipokuwa mtu amekabili na kuondoa kabisa kiini cha sababu ya ugonjwa.

Chukulia kwa mfano homa ya manjano, ambayo kimsingi si ugonjwa bali ni dalili za nje za maradhi ya ndani ya mwili,

kama jeraha kwenye bandama, au kansa ya ini, n.k. Ni dhahiri kuwa, haitakuwa na maana kujaribu kutokomeza homa ya manjano, kama mtu asingefanya uchunguzi kujua chanzo cha homa ni nini.

## Dalili za Dhambi kwa undani

Agano Jipya linatupatia orodha kadhaa za dalili za dhambi, na kwa kawaida huongeza onyo kuhusu uzito wa dalili hizi. Hii hapa ni orodha mojawapo:

> *Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, mafarakano, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.* (Wagalatia 5:19–21)

Hii hapa ni orodha nyingine, inayotoa maelezo ya kuogofya ya dalili zinazoweza kutokea wakati ugonjwa huu wa dhambi ukiwa kwenye hatua iliyokomaa zaidi:

> *Kama ilivyoandikwa, ya kwamba,*
> *Hakuna mwenye haki hata mmoja.*
> *Hakuna afahamuye;*
> *Hakuna amtafutaye Mungu.*
> *Wote wamepotoka, wameoza wote pia;*
> *Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja.*
> *Koo lao ni kaburi wazi,*
> *kwa ndimi zao wametumia hila.*
> *Sumu ya fira iko chini ya midomo yao.*
> *Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu.*
> *Miguu yao ina mbio kumwaga damu.*
> *Uharibifu na mashaka yamo njiani mwao.*

*Wala njia ya amani hawakuijua.*
*Kumcha Mungu hakupo machoni pao.* (Warumi 3:10–18)

Kwa hakika hakuna orodha yoyote miongoni mwa hizi inayoonesha kwamba dalili zote zitapatikana kwa viwango sawa kwa kila mtu. Kwa upande mwingine, Agano Jipya linasisitiza kwamba kila mtu huonesha baadhi ya dalili hizo kwani ugonjwa huu umetapakaa ulimwenguni kote.

## Dalili za Dhambi kwa Ujumla

Basi kuna dalili ambazo huweza kuitwa dalili za ujumla. Mojawapo ni **Udhaifu wa Kimaadili**. *"Tulipokuwa bado wanyonge. . ."* (Warumi 5:6, Habari Njema).

Kama mfano tunaweza kumchukua Pontio Pilato, Gavana wa Kirumi, aliyeagiza kumsulubisha Yesu Kristo (Mathayo 27:11–26; Luka 23:1–25; Yohana 18:28–19:16). Huyu ni wa mwisho miongoni mwa watu ambao wataonekana kuwa dhaifu. Alikuwa ni mwanajeshi wa ngazi ya juu kabisa, kamanda mkuu wa jeshi la Warumi huko Yudea; na pia aliwajibika kutunza sheria na kanuni katika nchi.

Kwa kuonekana kwa nje, Pilato alikuwa kama boriti kubwa mno la mti ambao huonekana thabiti na imara, bali kwa ndani limeliwa na mchwa; na pindi utakapoongeza kuligonga, litavunjika.

Alipozungumza na Yesu faraghani, na kupata kuelewa uhalisia wa Mungu na ukubwa wa dhambi ambayo angefanya kama angemsulubisha Mwana wa Mungu asiye na hatia, aliamua ni lazima afanye kile alichofahamu kuwa haki kwa kumfungulia Yesu (Yohana 19:8–12). Lakini alipotoka nje, makutano wakapiga kelele kwa ghadhabu na viongozi wao wakamshinikiza, wakitishia kumshitaki kwa Kaisari wa Rumi. Na Pilato akasalimu amri. Ingawa alijua kuwa alichotaka kufanya kilikuwa ni sawa na kosa la kusaliti haki, hofu ikavunja msimamo wake wa haki na kwa hofu hiyo akatoa hukumu ya kusulubiwa kwa Yesu.

Hii inatufanya tujiulize hivi: je, hatujawahi kusema uongo kwa sababu ya kuhofia madhara yanayoweza kutupata ikiwa tungesema ukweli? Hatujawahi kufanya kitu ambacho tulijua kuwa si sawa, kwa sababu kundi tulilomo limesisitiza kulifanya, tukaogopa kulipinga kundi?

Dalili nyingine ya dhambi ni Ukafiri (***Ungodliness***):

> *Akilifahamu neno hili, ya kuwa sheria haimhusu mtu asiye na hatia, bali wavunjao sheria, waasi, na makafiri, na wenye dhambi, na wanajisi, na wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji, na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na linginelo lolote lisilopatana na mafundisho ya kweli; kama ilivyonenwa katika Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye, niliyowekewa amana.* (1 Timotheo 1:9–11)

Neno halisi la Kigiriki lililotafsiriwa hapa kama 'kafiri' humaanisha 'watu wasio na heshima ama uchaji.' Yeye ambaye hawamheshimu wala kumtii, awali ya yote, ni Mungu. Lakini mambo hayaishii hapa. Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu; na watu wakipoteza heshima na uchaji kwa Muumba, wanaanza kuishusha thamani ya kiumbe chake, ambacho ni mwanadamu. Wanapoteza heshima ya utakatifu wa mwili wa mwanadamu – mwili wao wenyewe na ya wengine pia. Ndiyo maana dhambi mbaya na nzito zinazoongoza ni kama za zinaa, za ulevi na za matumizi ya madawa ya kulevya ambazo huathiri afya ya mwili na kudumaza akili. Wanapoteza heshima kwa utakatifu wa ukweli. Hii huelekea katika kila aina ya uongo, udanganyifu, na ahadi zisizotekelezwa. Mwishowe, wanapoteza heshima kwa utakatifu wa maisha. Hivyo huleta uhalifu usio na mwisho wa matendo ya ukatili.

Dalili nyingine **ni farakano na uadui dhidi ya Mungu**:

> *Ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu.* (Warumi 8:7)

> *Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmetengwa, tena adui katika nia zenu kwa matendo yenu mabaya.* (Wakolosai 1:21)

Mifano mikubwa ya dalili hiyo, imeonekana wazi kabisa katika karne hii. Serikali katika nchi nyingi zimetumia uwezo wao wote kuunda mifumo ya kufuta imani yote ndani ya Mungu na Kristo. Walakini uadui dhidi ya Mungu hauishii kwa wale wasioamini kuwepo kwa Mungu tu. Wakati mwingine, hata watu wanaoonekana kwa nje kuwa wenye dini, mioyoni mwao wanaweza kuwa maadui dhidi ya Mungu. Paulo, Mtume wa Kristo, daima alikuwa ni mcha Mungu sana; lakini alikuwa adui mkubwa wa Yesu Kristo kabla ya kuongoka kwake (1 Timotheo 1:12–17).

Ukweli ni kwamba kuna uasi dhidi ya Mungu katika moyo wa kila mmoja wetu. Mungu anapotuamuru kwenye Biblia, tufanye au tusifanye mambo fulani, amri yake mara nyingi huamsha chuki ndani yetu na kutushawishi kufanya kinyume chake. Mtume Paulo alitoa mfano unaotokana na uzoefu wake mwenyewe (Warumi 7:5, 7–9). Kwa miaka kadhaa aliishi bila kuelewa amri ya Mungu "Usitamani." Kisha Mungu alimfunulia amri hii ndani ya moyo wake; na Paulo akaona amri hii ikichochea kila aina ya tamaa moyoni mwake ambazo, ingawa alijitahidi sana, hakuweza kuzitawala – na zaidi ya yote, katika kilindi cha moyo wake, hakutaka kuzitawala.

Kwa hakika, uadui huo dhidi ya Mungu mara nyingi hauonekani kuwa chuki iliyo wazi dhidi ya Mungu. Mara nyingi zaidi uadui huo huchukua mtindo wa kutomjali.

Sasa iwapo mtu atasema, "Sivutiwi na muziki au sanaa," tunaweza kufikiri kuwa inahuzunisha; lakini hatusononeshwi nayo, kwani ni namna ya upendeleo tu. Walakini ikiwa mwanamke atasema, "sivutiwi na mume wangu," ni huzuni; kwani ni uthibitisho ulio wazi kwamba amefarakana na mumewe. Upendo umeharibiwa. Na ikiwa mtu atasema, "Sivutiwi na Mungu," hii ni huzuni kubwa zaidi. Tupo hai kwani Mungu ametujalia. Kutokuwa na hamu naye ni dalili dhahiri kwamba, mahali fulani kumetokea farakano kubwa kati yetu na Mungu.

Basi, hizi ni baadhi za dalili tu. Bali kiini cha ugonjwa wenyewe unahusisha **nia ya kujitenga na Mungu, Muumba wetu, ili kujitawala wenyewe**. Kwa mujibu wa Biblia (Mwanzo 3), dhambi ya kwanza kabisa aliyotenda mwanadamu haikuwa ukaidi wala dhambi ya kutisha kama uuaji au uasherati. Ilitokea wakati Adamu na Hawa walipojaribiwa na Shetani kujitenga na Mungu, ili wajiamulie wenyewe ni kipi kilicho chema na kipi kilicho kiovu, walidhani kuwa wao wangeweza kuwa miungu yao wenyewe bila ya hatari yoyote kutokea. Hivyo walikula tunda lililokatazwa. Mara moja, ikawasababishia kutengana na Mungu na kujawa na fikra za hatia na aibu zilizowafanya watake kujificha na kumkimbia Mungu ambaye walijisikia kwamba amewakasirikia. Sisi sote tumefuata nyayo zao kwa kutotii na kutaka kujitawala. Bali kuishi maisha ya jinsi hiyo ni sawa na kuishi maisha yasiyo na ukweli, wala uhalisia. Sisi hatukujiumba. Sisi ni viumbe wa Mungu. Kuishi kwa kujitenga na kutafuta kujitawala mbali naye ni kinyume cha kanuni ya msingi ya kuwepo kwetu.

Basi, Agano jipya linasema kwamba **dhambi ni uasi**:

> *Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.* (1 Yohana 3:4)

Sasa tunafahamu ni hatari gani zinazoweza kutukabili tusipotilia maanani kanuni za asili za Muumba, kama vile kanuni za umeme kwa mfano. Ebu fikiria mtu akinunua birika ya umeme bila kufanya jitihada za kusoma na kufuata maelekezo ya mtengenezaji wa kifaa hicho toka kiwandani. Halafu akaziunganisha nyaya jinsi anavyoona vyema yeye mwenyewe. Na matokeo yake anajiua kwa umeme yeye mwenyewe. Hatuna haja ya kumwonea huruma: tunapaswa kumwita huyo mjinga kwa kutofuata maelekezo ya mtengenezaji na kwa kutochukua tahadhari ya kanuni za umeme. Vivyo hivyo, kukataa na kutozingatia maadili na sheria za kiroho za Muumba ni lazima italeta hali ya janga la kimaadili na kiroho. Hali hiyo ni chanzo kikuu cha dalili nyingi za dhambi.

Jambo la maana ni kwamba, kwa mujibu wa Biblia, kuna dawa. *"Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi"* (1 Timotheo 1:15). *"Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye"* (Yohana 3:17). Kwa hiyo, sura zinazofuata zitatafiti maneno ambayo Agano Jipya hutumia kuelezea wokovu huu na namna unavyotenda kazi.

Lakini kuna mambo mawili yatupasayo kujihadhari nayo. Watu wengi hufikiri kwamba tunaokolewa tunapokuwa tumejitahidi kutokomeza kabisa dalili zote za dhambi kutoka katika maisha yetu. Hilo ni jambo jema kufanyika; bali haliwezi kutuokoa. Unaweza kuchuma maembe yote kutoka kwenye mwembe; lakini mwembe huo utabaki kuwa mwembe. Hiyo ndiyo asili yake. Hivyo hata kama tungeweza kudhibiti dalili zote za dhambi, bado tungebaki na asili ya dhambi ndani yetu. Na kama Agano Jipya lisemavyo, hili si kosa letu. Tulizaliwa katika hali hiyo. Tulirithi asili ya dhambi kutoka kwa mzazi wetu wa kwanza, Adamu. Bali kwa njia ile ile, tunaweza, kama tunapenda, kupokea maisha matakatifu toka kwa Kristo, ambayo asili yake ni kuishi maisha ya kumpendeza Mungu. *"Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja* [Adamu] *watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja* [Kristo] *watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki"* (Warumi 5:19).

Na jambo la pili la kujihadhari nalo ni hili: Mungu anatupenda japokuwa bado sisi ni watenda dhambi. Ndiyo maana wokovu wa Mungu ni rahisi kupokelewa na mwanadamu na wokovu huo unatenda kazi kweli. Hatuna haja ya kujiboresha wenyewe kabla ya Mungu kuwa tayari kutukubali na kuanza kazi yake kubwa ya wokovu ndani yetu. Yeye anatupenda sisi na yuko tayari kutukubali jinsi tulivyo. Hiki ni kiini cha hoja katika Warumi 5:6–11, kifungu ambacho mtu yeyote aliye makini kuhusu tatizo la dhambi anapaswa kukitafakari kwa kina zaidi.

# Sura 4

## Upatanisho

### *Njia ya kuifikia Amani*

Katika sura iliyopita tumesoma kuhusu ugonjwa wa kimaadili na kiroho ambao sisi sote tunaugua, na dalili zake za kututenga na Muumba, yaani dhambi. Sasa tunaanza kuchunguza maneno yanayoelezea tiba.

Kwanza tunaona neno jema *upatanisho* pamoja na tendo linalofuatana nalo 'kupatanisha.' Yamkini ni neno la kueleweka kwa urahisi zaidi kati ya maneno yetu yote kwani tayari tunafahamu lina maana gani kwenye mahusiano yetu na watu wengine. Wengi miongoni mwetu kwa wakati fulani maishani tumepitia suala hili kama ifuatavyo. Tumetenda, ama kunena, yasiyo sahihi ambayo yameumiza au hata kujeruhi rafiki yetu fulani. Mwishowe rafiki huyo ametukabili na kutuambia kosa letu. Lakini badala ya kukiri, na kuomba msamaha, kiburi au hofu zetu zimetusababisha kukataa kosa letu, au hata kuongopa kuhusu jambo hili; na tukakasirika, na kutoa shutuma nyingi dhidi yake. Na kisha tukatokomea, tukinong'ona, "Sitaki kuongea naye wala kuonana naye tena." Kwa hiyo hapo kimeanza kipindi kirefu cha utengano, umbali, na upweke. Kwa wakati huo, kama atajitokeza mtu yeyote – asiyefahamu shida hiyo – na kumsifia

rafiki yetu wa awali, tunachukizwa. Na kisha tunaelezea jambo hilo lililotokea kwa kujipendelea, bila kuzingatia ukweli, ili kuchafua sifa ya rafiki yetu wa kale, na hivyo kuhalalisha chuki yetu dhidi yake.

Kama inavyotokea kwa mahusiano ya watu wengi, ndivyo yalivyo na mahusiano yao na Mungu. Kumbukumbu na utambuzi wa makosa yao umewafanya kuelewa mioyoni mwao kwamba kama yupo Muumba, lazima atakuwa kinyume cha dhambi zao na, hivyo wanadhania, yuko kinyume chao pia. Kwa hiyo, badala ya kukiri dhambi zao, wanapinga kuwepo kwa Muumba. Kama wakikutana na mtu anayemwamini Mungu, na kumpenda na kumwabudu, wanachukizwa naye na kumlaumu Mungu kwa maovu yote ambayo watu wa dini wamefanya kana kwamba hayo ni makosa ya Mungu (na kana kwamba wasioamini kuwepo kwa Mungu hawakutenda kamwe uovu wowote), ama wanamlaumu Mungu kwa kuruhusu mateso mengi duniani, na kadhalika. Kwa hivyo utengano wao na Muumba wao huendelea, na maisha hubaki kuwa hafifu yaliyofunikwa na giza nene lisilooonesha kusudi wala tumaini. Giza hilo linapenywa mara tu dhamiri yao mbaya inapolalamika kwa sababu dhamiri inakataa kunyamaza na kutulia.

## Hatua ya Kwanza

Upatanisho ni neno ambalo hutuambia ya kwamba Mungu mwenyewe amechukua hatua kushinda utengano huu, kufuta mawazo ya uongo yaliyo msingi wa utengano huo, na kuondoa vikwazo dhidi ya amani. Kuna aya mbili kwenye Agano Jipya ambazo hutuambia ni kwa jinsi gani hayo hutokea:

> *"Naye* [Yesu Kristo] *ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au milki, au enzi, au*

> *mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye. Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi au vilivyo mbinguni. Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmetengwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama.* (Wakolosai 1:15–22)

Waweza kupata aya ya pili kwenye 2 Wakorintho 5:18–21.

Jambo la kwanza kutambua linalozungumziwa kwenye aya hizi juu ya upatanisho ni kwamba **Mungu amechukua hatua ya kwanza kutafuta upatanisho**:

> *Kwa kuwa katika yeye* [yaani katika Kristo] *ilipendeza utimilifu wote ukae na kwa yeye* [yaani kwa Mungu] *kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake. Yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake.* (taz. Wakolosai 1:19–20 na 2 Wakorintho 5:19)

Sasa jambo hili ni la kipekee, kwani sheria ya kawaida ya Mungu kwa wanadamu wanapotenda makosa miongoni mwao ni kwamba ni wajibu wa yule mtu aliyetenda kosa kuchukua hatua ya kwanza ya kuleta upatanisho. Kristo alisema, *"Basi ukileta sadaka yako madhabahuni, ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako, iache sadaka yako mbele ya madhabahu, uende zako, upatane kwanza na ndugu yako, kisha urudi uitoe sadaka yako"* (Mathayo 5:23–24). Bali Mungu hakutenda kosa dhidi ya ulimwengu. Hakuna alichopaswa kuombea msamaha. Ni wanadamu walioanzisha uadui kwa kumwasi. Lakini ni Mungu

aliyechukua hatua ya kwanza katika kutafuta upatanisho kati yetu na yeye, kwa kumtuma Mwanawe ulimwenguni.

Na hii ni ya kipekee kwa sababu nyingine. Mara kadhaa, wanadamu wawili wanapokuwa wamekosana, wanapenda waweze kuchukua hatua ili wawe marafiki tena. Lakini kila mmoja anahofia kukataliwa na yule mwingine. Bali Mungu alimtuma Mwana wake ulimwenguni hali akijua ya kwamba atakataliwa, atadhalilishwa, na kusulubiwa. Hakika hiyo ndiyo maana Mwana wa Mungu, ambaye kupitia kwake ulimwengu uliumbwa, alikuja miongoni mwetu akiwa na utukufu wake uliofichwa katika maumbile ya binadamu. Bila kuuficha utukufu wake ingesababisha washindwe kumwendea, achilia mbali kudhihirisha uadui wao kwake. Kama ilivyokuwa, walidhihirisha chuki yao dhidi ya Mungu kwa Yesu Kristo na kumweka msalabani. Na wakisha kuyafanya hayo, Mungu alitangaza kwamba bado aliwapenda na alikuwa tayari kuwasamehe kwa walilomtendea na kwa dhambi zao zote nyingine (Matendo 2:36–39). Kwa maana aliwapenda hata walipokuwa bado wana uadui naye.

Kwa maana hiyo, hili hapa ni jibu la Mungu kwa madai ya uongo ya Shetani aliyoingiza katika fikra za wanadamu: ya kuwa Mungu ni mtawala wa kiimla anayesubiri tu nafasi ya kwanza kuwazuia wanadamu kuishi maisha yao kikamilifu na kuyafuatilia malengo yao mazuri (Mwanzo 3).

Si kwamba Mungu hakuichukia dhambi, wala hakuwa tayari kuvumilia kiburi na udhalimu wa mwanadamu ili adumishe au kurudisha urafiki wa mwanadamu. Mwenyezi siyo mnyonge. Asingeweza wala asingetaka kuchukulia kwamba dhambi ya mwanadamu si kitu. Kwa hiyo, tunahitaji kuelewa Agano Jipya linamaanisha nini kuhusu neno 'kupatanisha' linaposema, *"Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake."* Ili kufanya hivyo tunapaswa kutilia maanani jinsi neno hilo lilivyotumika katika lugha ya Kigiriki cha kale, lugha ambayo ilitumika kuandika Agano Jipya.

Ikiwa mtu moja (tumwite A) alimchukiza mtu mwingine (tumwite B) kwa matendo yake maovu, basi B ana kila haki ya kumkasirikia A, na kumhesabu ana hatia ya uovu wake. Kwa hiyo, ili kumpatanisha A na B ni lazima kweli kuubadili mtazamo wa A dhidi ya B, lakini zaidi ni lazima kuondosha sababu ya hasira halali ya B dhidi ya A.

Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi si matokeo ya kukasirika kwake kwa muda mfupi yanayomsababisha kutenda mambo kinyume cha tabia yake. Wala sio hisia za kuudhiwa zitakazopungua mwishowe. Wala siyo dukuduku ambalo Mungu analitunza kimyakimya moyoni mwake. Dhambi inachokoza uwepo wa Mungu na tabia yake. Na kama mtawala wa maadili wa ulimwengu, Mungu anapaswa aoneshe waziwazi na adhihirishe hasa uchungu wa moyo wake wote anavyokerwa dhidi ya dhambi. Hiyo inamaanisha kwamba daima hawezi kutojali dhambi, ama kuichukulia kama tendo dogo lisilo na maana. Hadi pale dhambi itakapoadhibiwa, tena hadharani machoni pa ulimwengu wote, ndipo hasira ya Mungu itatulizwa na sifa zake zitathibitishwa. Kwa hiyo kuupatanisha ulimwengu na yeye ilimbidi Mungu kwanza aondoe sababu za kukerwa kwake na ulimwengu: alilazimika kuadhibu dhambi ya ulimwengu. Mbali na hiyo, kusingekuwa na upatanisho naye, wala wanaume kwa wanawake wasingekaribishwa na kurudishwa tena katika urafiki wake.

Na hiyo ndiyo sababu, katika tamko la pamoja la Mungu katika utatu wake, Mwana wa Mungu akawa mwanadamu, pasipo kuuacha uungu wake. Kutokana na ukamilifu wa Mungu kukaa ndani yake, aliweza kumwakilisha Mungu kwa wanadamu. Kile wanadamu walichomfanya yeye, ndicho walichomfanya Mungu. Jinsi Mwana wa Mungu alivyowajibu wanadamu, ndivyo Mungu alivyowajibu. Katika yeye wanadamu waliweza kuona namna sahihi Mungu alivyo.

Kwa wakati huohuo kwa kuwa alikuwa mwanadamu kamili (japokuwa si mwanadamu tu) aliweza kusimama kama mwakilishi

wa wanadamu wote mbele za Mungu. Hivyo aliweza kuzichukua dhambi za ulimwengu, na ndivyo alivyofanya, akiwa kama Mwakilishi na Mbadala wa wanadamu. Na hivyo akakubali hadharani hasira ya Mungu iwake juu yake na kuteseka kwa adhabu ya dhambi. Hivyo aliondosha kabisa sababu ya hasira ya Mungu dhidi ya ulimwengu na kufungua njia kwa mwanadamu kupatanishwa na Mungu na kuwa na amani naye.

Tunasoma katika 2 Wakorintho 5:19–21,

> *Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao. . . . Yeye asiyejua dhambi alimfanya* [Yesu Kristo] *kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.*

Hiyo ni kusema, Kristo alipozichukua dhambi za ulimwengu kama mwakilishi wa wanadamu, ingawa yeye hakuwa na dhambi, Mungu alimchukulia kama vile dhambi za dunia zilikuwa zake. Hivyo adhabu ya haki dhidi ya dhambi za wanadamu ilichukuliwa na Kristo na kuondolewa, na matokeo yake ikawa hakuna kizuizi tena kwenye njia ya mwanadamu ili aweze kumrudia Mungu. Haki haimlazimu Mungu tena kuhukumu dhambi za ulimwengu juu yao. Wote wanaweza kuja kwa Mungu kwa njia ya Kristo, wakapatanishwa naye, na kuwa na amani naye sasa na hata milele. Mwanadamu hana haja ya kutafuta amani yake mwenyewe na Mungu. Kristo alifanya tayari hilo kwa ajili yake. Jambo pekee analopaswa kufanya mwanadamu ni kuukubali upatanisho na amani iliyofanywa na Kristo. Hivyo mwanadamu akifika kwa Mungu, anajikuta akikubalika kana kwamba alikuwa ni Kristo mwenyewe, au, kama Biblia isemavyo, anachukuliwa kama mwenye uhusiano mwema na Mungu kama Kristo alivyo nao (*"tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye"*).

Je, hii humaanisha kwamba wanadamu wote kokote kule waliko wameokolewa, au wataokolewa, hata kama wataendelea kutomtii Mungu na kuishi maisha ya dhambi, ama hata kama

wataendelea kutoamini kuwa Mungu yupo? Hapana, la hasha. Kristo kwa hakika amefanya upatanisho na amani na Mungu kwa watu wote. Walakini swali linabaki iwapo kwa upande wetu tupo tayari kukukubali amani au la. Imetokea nyakati fulani katika historia ambapo viongozi wa mataifa mawili yaliyokuwa vitani walikubali kusitisha mapigano na kutia sahihi kwenye makubaliano ya amani. Pengine kundi fulani lililojitenga la taifa mojawapo limekataa amani. Kundi hilo liliendelea kulitazama taifa lingine kama adui, na kuwachukulia wale wa taifa lake waliokubali amani kama wasaliti. Hivyo wakaendeleza mapigano.

Ndivyo ilivyo kati yetu na Mungu. Wale walioikubali amani aliyoifanya Kristo wanaelezewa kwenye Agano Jipya kuwa wamepata *"amani kwa Mungu"* (Warumi 5:1, 11) na hivyo wameingia kwenye amani ya kudumu na Mungu. Lakini inawezekana kwa watu kuukataa upatanisho, kutomjali Mungu na kuendeleza chuki zao kwa Muumbaji wao. Bali kiumbe kifanyacho hayo, kwa vyovyote, hakina budi kinajiangamiza.

## Mahusiano na Kurejeshwa kwa mambo yote

Faida mbili zaidi zinapatikana kutokana na amani ambayo Kristo ameleta. Faida ya kwanza ni hii: Wale ambao kwa njia ya Kristo wamepatanishwa na Mungu wanajikuta wakipata amani pia kati yao na wale wengine wote waliopatanishwa na Mungu kwa njia ya Kristo.

> *Kwa ajili ya hayo kumbukeni ya kwamba zamani ninyi, mlio watu wa Mataifa kwa jinsi ya mwili . . . mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli . . . Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Naye akiisha kuuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili afanye hao wawili kuwa mtu mpya*

> *mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani. Akawapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiisha kuumaliza ule uadui kwa huo msalaba. Akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na amani kwao wale waliokuwa karibu. Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja.* (Waefeso 2:11–18)

Aya hii inafafanua jinsi Kristo alivyotokomeza uadui wa muda mrefu kati ya Wayahudi na wasio Wayahudi. Lakini alitokomeza pia vizuizi vingine kama mbari, utaifa, tabaka la kijamii, na dini, ambavyo vimesababisha mipasuko mikubwa kati ya wanadamu. Kwa bahati mbaya ni kweli kabisa kwamba mara nyingi katika mwenendo wa historia mataifa yanayodai kuwa ya Kikristo yamewatesa na kupigana dhidi ya watu na mataifa mengine ambayo vivyo hivyo yamedai kuwa ya Kikristo. Lakini mienendo hiyo huleta mashaka kama kweli wahusika wamepatanishwa na Mungu. Badala yake, inaonesha kwamba ukiri wao juu ya Ukristo umekuwa ni wa kufuata taratibu na desturi za nje tu; kama lisemavyo Agano Jipya, wamepokea *"neema ya Mungu bure"* (2 Wakorintho 6:1).

Faida ya pili na iliyo kuu sana ni hii: siku moja Mungu atapatanisha ulimwengu wote wa wanadamu walio hai kwake mwenyewe (taz. Wakolosai 1:20, *"na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni."*). Na tena, kwa bahati mbaya, hiyo haimaanishi kila kiumbe kilicho ulimwenguni, Shetani akiwemo, watafanywa kuwa marafiki watiifu wa Mungu. Kwani Mungu hataondoa uhuru wa kuamua kutoka kwenye kiumbe chochote, hata kama angependa kubadilisha wahalifu kuwa watakatifu. Ila hali ni hii: Mungu hatasubiri milele. Siku moja atazirejesha na kuziboresha dunia na ulimwengu. Kwa hiyo itambidi kuharibu wote ambao wameng'ang'ania kubaki katika uasi wao dhidi yake. Bali atakapofanya hivyo, hakuna mtu atakayeweza kupaza sauti

yake kupinga uamuzi wake. Msalaba wa Kristo utanyamazisha upinzani wowote. Wote wangeweza kuokolewa kwa neema ya ajabu ya Mungu kwa kupitia Kristo. Hata wale watakaopotea hawataweza kumkosoa Mungu juu ya misingi ya maadili yake. Ulimwengu utakuwa umetulizwa kwa amani kabisa (Ufunuo 5:11–14).

# 5
# Sura

## Kuhesabiwa Haki

### *Kuweka Mambo Sawa Kisheria*

Maneno mawili ya msingi yanayofuata ambayo Agano Jipya hutumia kufafanua kitu ambacho Mungu amejiandaa kutufanyia ni kuhesabia haki na kuthibitishwa kuwa mwenye haki. Hayo ni maneno ya kisheria. Hii huwaudhi baadhi ya watu. Wanadai kuwa kama kweli Mungu yupo, lazima atupende kama baba anavyowapenda watoto wake na atakuwa tayari kuwakaribisha watoto wake waliopotea kama baba alivyofanya kwa mwanawe katika mfano mashuhuri wa Yesu unaozungumzia habari ya mwana mpotevu (Luka 15). Baba huyo hakujifanya kama hakimu na kuchukua kijana wake aliyetubu kwenye mahakama ya sheria; wakosoaji husema, wala Mungu asingefanya hivyo.

Hayo mawazo ni ya juujuu tu. Maana hata kwenye mfano huo, tunaona kuwa, ingawa baba alimsamehe mwanawe mpotevu na kumrejesha kama mwanawe, hakuchukua mali ya urithi wa mtoto wake mkubwa na kumpa nusu ya mali hizo yule mpotevu aliyerudi ili kufidia hali ya yule mpotevu aliyekuwa ametapanya sehemu yake. Hiyo isingekuwa haki kabisa; msamaha wa Mungu hauwezi kamwe kutolewa kwa gharama ya haki yake mwenyewe au ya watu wengine.

Ebu fikiria binti yako alikuwa akifanya kazi benki. Siku moja jambazi akaingia benki, akampiga risasi, na kutokomea na kiasi kikubwa cha pesa. Ungefikiriaje hakimu mwenye dhamana ya kesi iliyofikishwa mbele yake kama angesema, "Japokuwa mtu huyu amevunja sheria, ni mwanangu nimpendaye sana. Anaomba radhi. Hivyo nitamsamehe bila kumpa adhabu yoyote"? Je, usingepinga na kusema kuwa msamaha huo haukuwa wa haki kabisa kwako na kwa binti yako pia, na kwamba inakinzana na misingi yote ya jamii inayojali haki na iliyostaarabika? Funzo litokanalo na mfano wa mwana mpotevu ni sahihi kabisa: Mungu yu radhi kusamehe watoto wake. Bali huo ni upande mmoja tu wa ukweli. Upande mwingine ni kwamba msamaha wa Mungu hauna budi kwenda sambamba na kanuni za haki zinazokubalika ulimwenguni, tena lazima uonekane hivyo.

Mpaka sasa tutaona kwamba kitenzi cha 'kuhesabia haki' kina maana mbili za msingi:

1. Kutangaza mtu kuwa katika haki
2. Kuthibitisha kwamba mtu au kitu kina haki

Neno hili halimaanishi *"**kumfanya** mtu kuwa mwenye haki."* Luka 7:29 inasema kwamba *"watu wote. . . waliikiri haki ya Mungu."* Hiyo haiwezi kumaanisha kwamba watu **walimfanya** Mungu kuwa mwenye haki. Mungu kamwe hakupungukiwa kuwa mwenye haki, hakuna mtu aliyehitaji kumfanya awe mwenye haki. Ina maana "watu **walitangaza** ya kwamba Mungu alikuwa mwenye haki."

Ebu sasa tuanzie mwanzo. Huu hapa ni mfano wa matumizi ya neno hilo katika mahakama za haki za wanadamu nyakati za kibiblia.

> *Pakiwa na mashindano kati ya watu, wakaenda maamuzini, na hao waamuzi wakawaamua; na wampe haki mwenye haki, na wamhukumie makosa yule mwovu.* (Kumbukumbu 25:1)

Maana ya maneno 'wampe haki mwenye haki, na wamhukumie makosa yule mwovu' ni dhahiri. 'Kumhukumia makosa yule mwovu'

haimaanishi 'kumfanya kuwa mwovu' bali 'kumtangaza kuwa mwovu,' au 'kuwa mwenye makosa.' Vivyo hivyo 'kumhesabia haki mwenye haki' humaanisha kwamba mwanadamu aliyethibitika kuenenda katika haki lazima atangazwe kuwa katika haki.

Kwa bahati mbaya, hutokea kwa nyakati fulani katika mahakama za wanadamu kwamba mtu ambaye kwa hakika amefanya makosa anaweza akamhonga hakimu na mahakama ili itolewe hukumu ya uongo. Biblia kwa nguvu zote inashutumu aina hii ya kupindisha haki.

> *Yeye asemaye kwamba asiye haki ana haki; naye asemaye kwamba mwenye haki hana haki. Hao wote wawili ni chukizo kwa Bwana.* (Mithali 17:15)

Ukiweka hilo akilini, soma mfano ufuatao uliosimuliwa na Yesu. Utakuta maajabu fulani ndani.

> Akawaambia mfano huu watu waliojiamini ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine wote. Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote.
>
> Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipigapiga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi. Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa. (Luka 18:9–14)

**Jambo la kwanza** kutambua ni kwamba hapa Yesu anatumia neno 'kuhesabiwa haki': mtoza ushuru alikwenda nyumbani kwake

amehesabiwa haki. Hii sasa inavutia. Farisayo na mtoza ushuru hawakwenda kwenye mahakama za sheria za kidunia mbele ya hakimu wa kidunia. Walikuwa wamekwenda hekaluni kusali. Kadiri walivyosimama mbele za Mungu na kutafakari maisha yao, Mungu alikuwa hakimu wao na kupitisha hukumu yake juu yao.

**Jambo la pili** kutambua ni kwamba, kwa mujibu wa Kristo, mmoja kati ya watu wale wawili alikwenda nyumbani akiwa amehesabiwa haki; maana yake ni kwamba kama hakimu, Mungu alimtangaza mtu huyu kuwa sahihi mbele ya mahakama yake.

**Jambo la tatu** kutambua ni kwamba ingawa mmoja wao alihesabiwa haki na Mungu, mwingine hakuhesabiwa haki. Na hii inastaajabisha sana. Kwani mtoza ushuru alikiri yeye mwenyewe kuwa mtenda dhambi; na watu wengi katika nyakati zake wangetazama ukusanyaji kodi kwa ajili ya mabeberu wa Kirumi, na ubadhirifu wote uliotendeka, kama dhambi kuu. Na bado ni yeye aliyehesabiwa haki na Mungu! Farisayo, kwa upande mwingine, ni mtu aliyejaribu kuishi maisha mema kwa kadiri ya uwezo wake, aliishi maisha ya kidini, ya kibiashara, na ya kijamii: hakuwa asiye na haki, wala anayelaghai, wala mzinifu, alifunga mara mbili kwa wiki, alitoa mali zake na kuwapa maskini. Na bado Mungu hakumhesabia haki.

Kwa kuangalia mara ya kwanza, siyo kwamba inastaajabisha tu, bali inashitusha. Biblia yenyewe, kama tulivyokwisha tazama, inakataza mahakimu wa kidunia kuwahesabia haki waovu, na kuhukumia makosa wenye haki. Ni vipi basi, watu hao wawili walivyojitokeza kwenye mahakama ya Mungu, Mungu akaweza kumhesabia haki mtoza ushuru, aliyekuwa '*mtu mbaya*' na kutomhesabia haki Farisayo, aliyekuwa '*mtu mwema'*? Sehemu ya majibu ya swali hili yanapatikana kwenye kanuni zifuatazo.

**1. Viwango vya sheria ya Mungu ni kamili.** Viwango vya Mungu hutofautiana na vyetu. Kijana akiwa amefanya mtihani shuleni na kupata asilimia 70, yamkini atahesabiwa kuwa amefaulu, ijapokuwa amepungukiwa alama 30 kufika 100. Bali sheria ya Mungu haiko hivyo. Inahitaji ukamilifu kwa asilimia 100 wakati

wote. Na hakuna awaye yote miongoni mwetu aliyefanikiwa katika hilo. Baadhi yetu wanaweza kuwa wema zaidi ya wengine. Bali Mungu ni mkweli: hawezi kujifanya kana kwamba anatuona tuko wema kuliko tulivyo. Uamuzi wake ni kwamba *"kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu* [yaani, kiwango kikamilifu] *wa Mungu"* (Warumi 3:23).

**2. Sheria ya Mungu ni kamilifu.** Ukivunja amri moja utakuwa na hatia ya kuvunja sheria yote, Biblia isemavyo (Yakobo 2:10). Pengine mwanzoni itaonekana kana kwamba hii siyo sawa, lakini sheria ya Mungu si mkusanyiko wa amri zisizo na mahusiano kiasi kwamba kama ukivunja amri moja tu haitadhuru zingine. Sheria ya Mungu ni muunganiko. Inalenga na inadai ukamilifu. Ukivunja amri moja, na kisha, hata kama utazingatia zilizosalia, matokeo yatakuwa bado hujashika sheria kwa ukamilifu. Ukivunja kiungo kimoja cha mnyororo wa nanga, meli itaanza kuelea na kuondoka. Ukifanya kosa moja kwa kujumlisha orodha ndefu ya namba, utapata jumla yote ya uongo. Na hata watu bora miongoni mwetu wamevunja zaidi ya amri moja ya Mungu.

**3. Kwa hiyo sheria ya Mungu inatuhukumu sisi sote.** Iwe tumejaribu kutenda mema kama yule Farisayo, ama tumetenda sivyo kama mtoza ushuru, sote tumeivunja sheria ya Mungu. Na Biblia inasema: "Basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu" (Warumi 3:19).

## Jibu la Sehemu ya kwanza ya Tatizo letu

Sasa basi tunaweza kuanza kutazama angalau nusu ya jibu la tatizo letu: Kwa nini yule Farisayo hakuthibitshwa kuwa mwenye haki? Kwa sababu, alipokwenda mbele za Mungu, aliorodhesha matendo yake mema, jitihada zake za dhati kushikilia sheria za Mungu; na alitumaini kuwa kwa misingi hii Mungu angemhesabia haki. Bali hilo halikuwezekana. Ingawa jitihada zake zilikuwa njema,

bado alipungukiwa, alikuwa amevunja sheria ya Mungu. Kwa hiyo alistahili kubeba adhabu yake ipasavyo. Mungu asingeweza kujifanya vinginevyo. Neno lake linasema: *"kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria"* (Warumi 3:20).

"Ikiwa ndivyo ilivyo," anasema mtu fulani, "kwa vyovyote itamaanisha kwamba Mungu hawezi kumtangaza mtu yeyote kuwa sahihi; hawezi kumhesabia haki mtu yeyote ajaye mbele ya mahakama yake. Vipi sasa kuhusu mtoza ushuru? Hakika alikuwa amevunja sheria ya Mungu vibaya zaidi ya Farisayo. Basi yawezekanaje Kristo anasema kwamba mtoza ushuru alitoka hekaluni kwenda nyumbani akiwa amehesabiwa haki?"

## Jibu la Sehemu ya pili ya Tatizo letu

Kinadharia kuna njia mbili ambazo tunaweza kuhesabiwa haki na Mungu kwazo. Njia ya kwanza ni kushika sheria yake kikamilifu: hapo Mungu anaweza kututangaza sisi "wenye haki mbele za Mungu." Bali njia hiyo kwa kweli haiwezekani kwetu, kama jinsi tulivyoona. Sote tayari tumeivunja sheria yake.

Njia nyingine ya kuhesabiwa haki ni kwa kulipa adhabu ya kuvunja sheria ya Mungu. Bali kama tungepaswa kufanya hivyo, ingemaanisha kutenganishwa kwetu milele na Mungu. Hivyo tunajikuta kwenye hali mbaya.

Suluhisho la Mungu ni kwamba Mwana wake kama Mwakilishi wa wanadamu amelipa deni kwa ajili yetu kwa kuchukua hukumu ya Mungu dhidi ya dhambi na kufa pale msalabani. Kwa hiyo kama tukiweka imani yetu kwa Yesu, Mungu anaweza kuhesabu kifo chake kama kifo chetu; hivyo basi deni letu linakuwa limeshalipwa na Yesu, Mungu anaweza kutuhesabia haki, hii ina maana kwamba, anatutangaza kuwa wenye haki mbele ya kiti chake cha hukumu.

Biblia inasema:

> *Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aoneshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa; apate kuonesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu.* (Warumi 3:23–26)

Je, hii humaanisha kwamba wanaume kwa wanawake wote wamehesabiwa haki moja kwa moja? Hapana. Tena kufuatana na mfano ule Farisayo hakuhesabiwa haki. Mtoza ushuru ndiye alihesabiwa haki, na hiyo ni kwa sababu, aliposimama mbele ya Mungu, alipigapiga kifua chake kwa uchungu na kukiri dhambi zake, akajishutumu, na kutambua kwamba alistahili kubeba dhambi ya kuvunja sheria ya Mungu. Kisha kwa imani aliomba rehema za Mungu aliposema, *"Mungu nirehemu mimi mwenye dhambi."* Papo hapo Mungu akamhesabia haki, yaani, alimtangaza kuwa mwenye haki mbele ya Mungu, kuwa huru mbali na adhabu ya dhambi. Hapo akapata kuhesabiwa haki sasa na hata milele.

Zaidi Biblia inatuambia kwamba, *"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu"* (Waebrania 9:27). Hiyo inamaanisha kwamba Mungu hatuiti sisi mbele ya kiti chake cha hukumu kila siku katika maisha yetu. Kuna siku moja tu ya hukumu; na siku hiyo huja baada ya kufa kwetu. Katika hukumu moja hiyo, maisha yetu yote yatachunguzwa na hukumu ya Mungu itatangazwa.

Na kitu cha ajabu ni kwamba hatuhitaji kungoja hadi siku ya hukumu ili kujua hukumu itakavyokuwa (taz. pia Yohana 5:24). Mungu anawaambia wale walioweka imani zao kwa Kristo kwamba kifo cha Kristo msalabani kinatosha kulipia maisha yao yote siku ya hukumu. Kwa hiyo, hawapaswi kuogopa. Wanapokuwa wamehesabiwa haki kwa njia ya imani yao kwa Kristo, wanaendelea kuwa na haki daima, na kwa kuhesabiwa

haki kwa njia ya imani, wana amani ya kudumu na Mungu (Warumi 5:1).

Kwa kuhitimisha mawazo yetu hadi hapa: kama tukiuliza, "Kwa hali gani twaweza kuhesabiwa haki mbele ya Mungu?" Jibu tunalopewa na Agano Jipya ni hili: *"Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria"* (Warumi 3:28). Mtu fulani anasema, "Kwa nini basi Agano Jipya linasema pia: *'Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake'*? (Yakobo 2:24). Huu sio utata unaokinzana?"

## Maana ya Kuhesabiwa Haki kwa Matendo ya Sheria

Hapana, huu sio utata. Yakobo anatumia neno 'kuhesabu haki' katika namna nyingine: si **kumtangaza** mtu kuwa mwenye haki, bali **kuthibitisha**, au **kumdhihirisha** mtu kuwa mwenye haki. Ni ukweli dhahiri kwamba mwanadamu anahesabiwa haki na Mungu katika msingi wa imani yake na si katika msingi wa matendo yake. Bali njia pekee ambayo mtu huweza kuwadhihirishia familia na marafiki zake kwamba ana aina hii ya imani, ni kwa namna anavyoenenda, kwa kupitia matendo yake.

Fikiria mtu anawaambia rafiki zake: "Wiki iliyopita nilipokea barua ikiniambia kwamba ndugu yangu ambaye ni tajiri amefariki na kuniachia urithi mkubwa wa fedha. Kitu pekee nilichopaswa kufanya ni kwenda benki na kudai hii zawadi ya kipekee. Niliiamini barua hii, nikaenda kudai zawadi yangu, na sasa mimi ni tajiri mkubwa."

Je marafiki zake wasingekuwa na haki ya kujibu: "Unasema wewe ni tajiri kwa kuiamini barua tu! Basi utuoneshe hayo kwa mabadiliko ya mfumo wa maisha yako kwamba imani na zawadi zako ni za kweli, wala si hadithi tu uliyotunga. Dhihirisha maelezo yako kwa matendo yako." Hivyo basi wale ambao wamehesabiwa haki na Mungu kwa njia ya imani wala si kwa njia ya matendo yao, lazima wathibitishe kuwa imani yao ilikuwa halisi, na bado

inakuwa halisi. Kuna njia moja tu ambayo unaweza kudhihirisha kuwa imani yako ni halisi, na hiyo ni kwa matendo yako, kama vile Yakobo asemavyo.

# Sura 6

## Fidia na Ukombozi

### *Gharama ya Uhuru*

Katika sura hii tutachambua maneno mengine mawili ya Agano Jipya yaliyo muhimu. Nayo ni **fidia** na **ukombozi**. Katika maana yake ya msingi maneno hayo yalikuwa katika matumizi ya kawaida hapo kale, kama ilivyo katika ulimwengu huu. Watu walitekwa na kuzuiwa kwa ajili ya fidia. Familia na marafiki zao walitakiwa kulipa kiasi kikubwa cha pesa ili waachiliwe huru. Magaidi wa kisasa huteka ndege ya abiria na kutishia kuua abiria mmoja baada ya mwingine, ama kulipua ndege yote, iwapo madai yao hayatatimizwa. Inawezakana hawatadai pesa: ila madai yao yanaweza kuwa ni kutaka kuachiliwa kwa magaidi wenzao ambao yamkini walikamatwa na serikali awali na kufungwa gerezani. Kwa hali hii bado tunatumia maneno kama vile 'bei,' na 'gharama,' na 'fidia' lakini bila kumaanisha kiasi cha fedha taslimu. Tunasema kwamba kuwaachilia magaidi ni gharama ambayo serikali inabidi kulipa ili kukomboa maisha ya abiria walioshikiliwa mateka kwenye ndege kusudi wasiuawe, vinginevyo itaipasa serikali kuthubutu kutuma kikosi maalum hatarini kwa ajili ya kuvamia ndege ili kuokoa abiria.

Ni muhimu kutambua kwamba unaweza tu kutumia neno la 'kukomboa' ikiwa unamnunua mtu kutoka gerezani na utumwani, au kutoka kwenye hali ya kutishiwa kufa, kuingia kwenye uhuru. Usingetumia maneno 'fidia' au 'kukomboa' kuelezea shughuli za wafanyabiashara waovu ambao, katika baadhi ya nchi, wako radhi kulipa kiasi kikubwa cha pesa ili kununua wasichana kutoka kwa wazazi wao maskini ili kuwatumia katika biashara ya ukahaba wa watoto. Hapo watakuwa wamewanunua wasichana hao, si kuwaweka huru kutokana na utumwa, bali kuwatumikisha.

Katika hali fulani watu huweza hata kukomboa kitu ambacho ni mali yao wenyewe. Mtu ambaye anahitaji pesa kwa haraka anaweza kuweka rehani saa yake. Mkopeshaji ataichukua saa na kumpa kiasi taslimu anachohitaji. Lakini saa haitakuwa mali ya mkopeshaji mara moja. Kwa kusema ukweli, kwa kipindi fulani saa itabaki kuwa mali ya mwenyewe aliyetoa. Ila kama anahitaji kupata umiliki halisi wa mali yake, inamlazimu kuikomboa katika kipindi hicho, hii ina maana, ainunue tena; na gharama atakayopaswa kulipa hakika itakuwa inazidi sana kiasi kile alichopokea awali kutoka kwa mkopeshaji.

Basi katika mazungumzo ya kila siku, maneno 'fidia' na 'ukombozi' hubeba vidokezo mbalimbali vinavyotofautiana kidogo, baadhi ya vidokozo hivi vinaonesha maana halisi, baadhi ni kama mfano. Vivyo hivyo katika Agano Jipya, kwa mazingira ya kitheolojia, maneno haya daima hutumika katika maana ya mfano. Hakuna wazo lolote la kulipia kwa fedha. *"Nanyi mlikombolewa si kwa fedha au dhahabu"* anasema Mtume Petro (1 Petro 1:18). Ila ukipitia matumizi yake yote katika Agano Jipya kuna maana zifuatazo:

1. Kununua au kukomboa watu toka katika deni, au utumwa, au kufungwa, au tishio la adhabu au kifo.

2. Daima ni Mungu au Kristo anayetajwa kuwa mwenye kununua au kukomboa. Hakuna mtu anayetajwa kujikomboa mwenyewe au kumkomboa mwanadamu mwenzake.

3. Malipo ya bei au fidia. Hapa pia ni Mungu au Kristo tu

anayetajwa kulipa deni au kubeba gharama ya fidia. Watu hawaombwi wala hawaruhusiwi kuchangia chochote katika gharama ambazo zilipaswa kulipwa kwa ajili ya ukombozi wao. Hii inakinzana sana na dini nyingi ambapo watu wanatakiwa kuupata wokovu kwa gharama za jitihada zao au mateso yao wenyewe, au hata kwa kulipa pesa. Pale Yerusalemu makuhani na wauza bidhaa hekaluni walipowashurutisha watu kuwa wangeweza kulipa, hata kulazimishwa kulipa kwa ajili ya wokovu wao, Kristo aliwafukuza wote nje (Yohana 2:13–16).

4. Lengo la ukombozi daima ni kuwaleta watu kwenye uhuru na kuwapatia urithi wa milele.

## Uhuru kutoka kwenye nini?

**1. Uhuru kutoka kwenye hatia ya dhambi zilizopita.** Mtu hawezi kubatilisha wakati uliopita. Mungu mwenyewe hatabadilisha historia. Kilichotendeka kimetendeka. Anachotupatia Mungu kwa njia ya Kristo ni kwamba ametuachilia kutokana na hatia ya dhambi za wakati uliopita. Watu wengi hufuatwa na maisha yaliyopita. Kadiri wanavyojaribu kusahau yaliyotokea, na kujaribu kuanza upya, hawawezi kuondoa hatia ya matendo yasiyofaa waliyotenda awali.

Wengine wasio na dhamiri ya kutosha wanadhani kwamba wanaweza kusahau waliyotenda kirahisi tu, kama mwanamke mzinifu katika Kitabu cha Mithali (30:20) ambaye *"hula, akapangusa kinywa chake, akasema: Sikufanya uovu."* Lakini kutowajibika huko hakuvunji mnyororo wa hatia iliyopo (hapo hatuzungumzii utata wa kisaikolojia ya kujisikia mwenye hatia kila wakati). Miaka kadhaa iliyopita, majambazi walivamia garimoshi huko Uingereza, wakamjeruhi dereva na kumwachia kilema cha maisha, na kutorokea Marekani ya Kusini wakiwa na mamilioni ya pauni za fedha. Huko wakatoa rushwa kwa mamlaka ili wasirudishwe kwao. Huenda leo hii majambazi hao hawahisi kuwa na hatia yoyote kuhusiana na kosa lao. Lakini hiyo haiondoi

ukweli kwamba iwapo wangetia mguu wao Uingereza wangetiwa nguvuni haraka iwezekanavyo na kuhukumiwa kifungo. Siku moja kila mwanamume na kila mwanamke watajikuta kwenye mahakama ya Mungu. Hata miaka ikipita au kumbukumbu ikisahauliwa, hazitafuta yaliyopita. Wasipomruhusu Kristo kuondoa hatia inayowaunganisha na maisha yao yaliyopita, mnyororo wa hatia utabaki hata milele.

Ukombozi huonesha kwamba Mungu anaweza kuvunja minyororo hiyo kwa ajili yetu katika maisha haya ikiwa tutatubu. Kitendo cha kuvunja mnyororo kinaitwa msamaha. Katika Kigiriki cha asili cha Agano Jipya, neno lililotumika zaidi kwa ajili ya msamaha (aphesis) humaanisha 'fungulia' au 'achilia.' Ni neno ambalo hutumika kumfungulia mtu kutoka gerezani, au kumwachia mdeni, au kumweka huru mtumwa. Na gharama ya achilio hilo imelipwa na Kristo, kama lisemavyo Agano Jipya: *"kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi "* (Waefeso 1:7). Hivyo, mnyororo ukiwa umevunjwa hautawekwa tena. Ukombozi alioulipia Kristo ni ukombozi wa milele (Waebrania 9:11–12).

**2. Uhuru katika laana iliyowekwa na sheria ya Mungu.** *"Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu"* (Wagalatia 3:13).

Laana iliyowekwa na sheria ya kimaadili ya Mungu si maneno matupu. Ni tamko la adhabu itakayofuatana kila mara sheria hii inapovunjwa. Baadhi ya watu hupenda kujadili kwamba, kwa kuwa hawamwamini Mungu, hawatambui haki aliyo nayo Mungu ama kutoa amri na makatazo au kutoa adhabu. Hakika hoja hiyo si sahihi. Sheria ya kimaadili ya Muumba imeandikwa katika moyo wa kila mwanadamu (Warumi 2:14–16). Kila wakati tunapomtuhumu mtu kuwa ametenda jambo lisilokubalika kimaadili, kila wakati tunapojitetea kuhusu makosa ya kimaadili tuliyofanya, kila wakati tunapojisemea kuwa inatubidi kuenenda vema na kuahidi kufanya hivyo wakati ujao, tunashuhudia – labda pasipo kukusudia – ukweli kwamba sheria ya Mungu imeandikwa

mioyoni mwetu. Hapo tunakubali mamlaka na thamani yake. Na kwa kutumia picha ya Agano Jipya, ni kana kwamba sheria ya kimaadili ya Mungu iliwekwa mbele yetu ikiwa imeandikwa kwenye hati. Na hapo tunapowashitaki wengine, na tunapojitetea wenyewe, na tunapotamani kufanya vizuri kimaadili, ni ushahidi kwamba tumeweka sahihi ya majina yetu chini ya hiyo hati ya sheria, na hivyo tunakubali mamlaka, matakwa na adhabu yake.

Wale ambao hawatatubu watakuta "hati" hiyo ikiwa na sahihi zao wenyewe, zitakazotolewa kama ushahidi dhidi yao siku ya hukumu ya mwisho. Bali wale ambao wanatubu wanahakikishiwa na Mungu mwenyewe kwamba amefuta hati iliyotufunga kisheria, hati ambayo tulikuwa tumesaini kwa mikono yetu wenyewe kwa kutambua hatia zetu. Hii *"hati iliyoandikwa ya kutushitaki"* Mungu ameigongomea msalabani pa Kristo. Hivyo Mungu ameutangazia ulimwengu wote kwamba, kwa kufa msalabani, Kristo alibeba laana ya torati kwa ajili ya wote ambao hutubu na kumwamini yeye, ili kwamba wawe huru (taz. Wakolosai 2:13–15).

## Gharama ya Ukombozi

Fidia iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu ilikuwa siyo gharama ndogo bali ilikuwa kifo cha Kristo. Kwa kweli, yeye mwenyewe alitangaza kwamba hili ndilo lililikuwa lengo la kuja kwake duniani: *"Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi"* (Marko 10:45). 1 Petro 1:18–19 inasema, *"Mlikombolewa. . . kwa damu ya thamani. . . ya Kristo."*

Ili kupata uzito wa gharama ya fidia, tunahitaji kukumbuka Kristo ni nani:

> *Ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi; naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi. . . vitu vyote viliumbwa kwa njia*

*yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.* (Wakolosai 1:14–17)

Kwa maneno mengine, Mkombozi ndiye Muumba aliyevaa utu, wala si mwingine. Yesu ni Mungu na mwanadamu kwa pamoja. Na hivyo ndivyo alivyoweza kuwa mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, na kujitoa mwenyewe kama fidia kwa ajili ya wote (1 Timotheo 2:5–6). Haikuwa, kama baadhi ya watu wadhaniavyo, kwamba Yesu, hali akiwapenda wanadamu, ilimpasa kulipa fidia hii kwa Mungu asiye na huruma ili kumshawishi asimimine ghadhabu yake juu ya wanadamu wote. Yeye aliyelipa fidia alikuwa Mungu. Na upendo uliomsukuma Kristo kutoa maisha yake kama fidia kwa ajili ya wanadamu ulikuwa ni udhihirisho kamili wa upendo wa Baba kwa wanadamu; kwani Kristo, yeye mwenyewe akiwa Mungu, alikuwa na hata sasa ni mfano sahihi na udhihirisho wa Mungu asiyeonekana. Agano Jipya linasema: *"Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu"* (1 Yohana 4:10).

"Lakini kwa hali hiyo," mtu mmoja anasema, "iwapo Yesu hakulipa fidia kwa Mungu, aliilipa kwa nani? Kwani lazima atakuwa ameilipa kwa mwingine." Ila kuhoji kwa namna hiyo ni sawa na kusahau tulichotambua awali, kwamba neno 'fidia' katika mazingira haya ya Agano Jipya linatumika kama mfano kuelezea gharama ya ukombozi wetu kwa Mungu na kwa Kristo. Gharama haikuwa pesa ambayo mwingine angeweza kupokea. Gharama ilikuwa ni ile ya mateso na hatimaye kifo.

Ebu fikiria mashua ya uokoaji ambayo imepandwa na watu wengi mno na iko hatarini kuzama, na mtu mmoja akajitolea kuruka toka mashuani na kutumbukia kwenye bahari iliyo baridi sana, hali akijua hiyo itamaanisha kifo chake. Vivyo hivyo tunaweza kusema kwamba alilipa bei nzito sana ili kuokoa maisha ya abiria waliobaki. Lakini haitaleta maana kuuliza: "Alilipa fidia hii kwa nani?"

Lakini swali lingine linaibuka. Biblia inafundisha kwamba sisi sote ni viumbe wa Mungu, na kwa hiyo sisi ni mali yake. Kwa nini basi Mungu alipe fidia, au kitu chochote kile, ili kuinunua mali yake mwenyewe? Ni kweli kwamba tumejifunga wenyewe na tabia ya dhambi, na tumejitia kwenye mikono ya Shetani, na kuwa wafungwa wake. Kwa nini Mungu asingeweza kutumia nguvu zake za ajabu, kumwangamiza Shetani, kuvunja vifungo vyetu, na kurudisha wanadamu wote kwake kwa nguvu, pasipo kulipa fidia?

Jibu ni kwamba swali la dhambi ni swali la kimaadili; na huwezi kutatua swali la kimaadili kwa kutumia nguvu. Kuna mambo fulani ambayo hata Mungu Mwenyezi hawezi kufanya. Hawezi kufanya mambo yasiyowezekana kimantiki kama vile kuchora duara iwe mraba. Wala hawezi kufanya mambo yasiyo sahihi kimaadili. Hawezi kusema uongo (Tito 1:2). Hawezi kuvunja sheria yake mwenyewe ya kimaadili. Sheria yake ni udhihirisho wa sifa zake mwenyewe. Akidiriki kuikana, basi amejikana yeye mwenyewe; na hawezi kufanya hivyo (2 Timotheo 2:13). Hakuwa na namna yoyote ya kutufungua toka kifungoni mwa hatia zetu kwa kitendo cha nguvu yake kufuatana na uamuzi wake wa kipekee. Njia pekee ya kufanya hilo ilikuwa ni kwanza kulipa deni ambalo sheria yake mwenyewe ya kimaadili inadai. Na hilo ndilo alilofanya kwetu kwa pendo. Kwa hiyo kuna kulipa gharama; kwa hiyo kuna mateso[1].

## Uhuru kwa ajili ya nini?

Awali tuliona kwamba kama ukimnunua mtu ili kumpeleka utumwani, gharama ambayo umelipa haiwezi kuitwa fidia. Sasa Kristo amelipa fidia ili kuwatoa watu kwenye hatia ya dhambi zao na kuwapa uhuru. Lakini uhuru kwa ajili ya nini? Ni dhahiri kwamba uhuru huo si ruhusa kwamba sasa wanaweza kuendelea

1 Kwa kutafakari tena swali la malipo ya Kristo kwa ajili ya adhabu ya dhambi rejea na sura ya 4 na 5.

kutenda dhambi bila kuadhibiwa. Kwa maana dhambi inaleta hali ya kutawaliwa nayo na huwafanya kuwa watumwa wale ambao wanaitenda mfululizo bila kutubu (Warumi 6:16–23). Basi hapa chini ni kauli inayoeleza jinsi Kristo anavyowakomboa wanafunzi wake **kutoka kwa nini** na **kwa ajili ya nini**:

> *Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na kufunuliwa kwa utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote; na kujisafishia watu wake mwenyewe walio na bidii katika matendo mema.* (Tito 2:11–14)

Tunaachia sura nyingine ya baadaye swali la jinsi Kristo anavyotuhakikishia kwamba njia hii mpya ya maisha itakuwa maisha ya uhuru, siyo ya utumwa wa kidini. Kwa wakati huu, ebu tutambue kwamba Agano Jipya linaeleza vizuri kabisa kwamba hatupewi matunda yote ya ukombozi wetu nyakati hizi. Faida ambazo fidia ya Kristo imepata kwa ajili yetu ni pamoja na *"ukombozi wa mwili wetu."* Ila kwa ajili ya hiyo ni lazima tusubiri hadi ujio wa pili wa Kristo (Warumi 8:18–25; Wafilipi 3:20–21).

Kwa upande mwingine nyakati hizi, Mungu huwapa wale wote wanaotubu na kuweka imani zao kwa Kristo zawadi ya Roho Mtakatifu. Huyo Roho Mtakatifu anawahakikishia waumini wote kuhusu kutegemewa kwa ahadi zote za Mungu, na yeye mwenyewe ni arabuni na ahadi ya urithi kamili ambao wataupokea, siku ile ambapo Mungu atakomboa ahadi zake zote na kujinyakulia mbinguni watu wake ambao hapo nyuma walinunuliwa kwa damu ya Mwanawe (Waefeso 1:13–14; Matendo 20:28).

# Sura 7

## Uzima wa Milele

### *Mahali hapa na Wakati huu*

Mojawapo ya mambo makuu aliyodai Kristo akiwa hapa duniani ni kwamba alikuwa na mamlaka ya kuwapa wanaume kwa wanawake uzima wa milele (Yohana 17:1–3).

Kama tunavyofahamu, dai hilo mara kadhaa limekuwa likidhihakiwa. Baadhi ya wakosoaji walidhania kwamba Yesu alikuwa anawaahidi wafuasi wake kwamba hawatakufa kimwili. Na kisha, kwa misingi ya dhana hiyo, wakafikia uamuzi kwamba Yesu lazima alikuwa mshabiki wa dini aliyepotoka, maana yeye mwenyewe alikufa mapema na wafuasi wake wote pia walikufa tangu wakati huo.

Lakini ukosoaji huu unatokana na mtu kutokujua kabisa kile alichosema Yesu. Ukisoma kwa ufupi kabisa Agano Jipya utaona kwamba Yesu si tu aliwaonya wanafunzi wake kwamba angesulubiwa baada ya muda mfupi, bali pia aliwaambia kwamba baada ya kuondoka kwake aliwataka wajiweke tayari kuyapoteza maisha yao kwa ajili yake (Luka 9:22; 12:4; Yohana 16:1–3). Je, madai ya Yesu kwamba angeweza kuwapa wafuasi wake uzima wa milele yangemaanisha nini? – Haikumaanisha kwamba wasingeonja mauti ya kimwili.

Aidha, kwa upande mwingine, wakosoaji wamedai kwamba 'uzima wa milele' ulioahidiwa na Yesu ni kitu ambacho watu wote wema wametakiwa kupata baada ya kuiaga dunia hii: kwa maneno mengine, 'wanakwenda mbinguni wanapokufa'. Kwa madai haya, wakosoaji wanabeza imani nzima ya uzima wa milele kuwa ni hatari na ni hadithi isiyosadikika. Wanasema kwamba, kama wanaume kwa wanawake wenye njaa wanavyoota ndoto za kula nyama choma; vivyo hivyo maskini na wanaonyanyaswa, waliokata tamaa na walio wagonjwa, wanavyobuni mbingu ya kimawazo ili kupunguza uchungu wa maisha yao na kuondoa dhiki zao. Wakosoaji wanaendelea kudai kwamba wanaokana kuwepo kwa Mungu (*atheists*) hawana haja na 'dawa hizo za kulevya'. Wanadai wana ujasiri na maarifa ya kupambana ili kuboresha maisha yao. Mwishowe hukabili uhalisia usiokwepeka wa kifo bila kulewesha akili zao na tumaini la mbingu ya kimawazo katika siku zijazo.

Basi ni kweli kabisa kuwa Agano Jipya linafundisha kwamba wanaoamini "huenda mbinguni baada ya kifo," ingawa linapendelea kuuweka katika namna tofauti: *"wanakwenda zao wakae na Kristo" au "kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana"* (Wafilipi 1:23; 2 Wakorintho 5:8). Bali madai ya wakosoaji ni upotofu wanaposema kwamba tumaini la mbingu ijayo linadumaza, au hata kuharibu jitihada za watu kuyatumia vizuri maisha yao hapa duniani. Agano Jipya limefafanua vizuri kabisa kwamba uzima wa milele si kitu tunachopata baada ya kufa na kwenda mbinguni. Ni uzima tunaoweza kupokea na kufurahia tukiwa hapa duniani sasa – kabla ya kufa na kwenda mbinguni. Hii ni maisha ya aina nyingine kabisa, zaidi na juu ya maisha ya kimwili, ya kihisia, ya kiuzuri, na maisha ya kutumia akili ambayo kiasili mwanadamu hufurahia. Ni maisha ambayo Kristo aligusia aliposema, *"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"* (Mathayo 4:4).

Kama unaweza, ebu fikiria ndoa ambayo mahusiano yake ni katika mambo ya kimwili tu, ndoa ambayo mume na mke

hawasemezani, hawashirikishani mawazo yao ya ndani zaidi, matumaini yao, furaha zao, hofu na huzuni zao, mapenzi yao kwa mfano kwenye muziki na ngoma, na wala hawafahamiani. Ndoa hiyo isingekuwa tofauti sana na jinsi wanyama wanavyojamiiana. Ingepungukiwa na hali ya uanadamu. Ndivyo ilivyo, mwanadamu ambaye anawiwa kufurahia maisha ya kimwili, ya kihisia, ya uzuri na ya kiakili, bila kujali chochote kuhusu ushirika wa kiroho na Mungu na hivyo kukosa maisha ya hali ya juu kabisa kwa sasa. Aidha, yuko katika hatari kubwa ya kukosa uzima wa milele katika dunia ijayo vilevile. Agano Jipya liko wazi na linasema: *"Amwaminiye Mwana, ana uzima wa milele."* Kitenzi 'ana' kinatumika katika wakati uliopo na kinaonesha, anao uzima huo hapa na sasa. Kwa upande mwingine, Agano Jipya linaongeza onyo: *"Yeye asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia"* (Yohana 3:36).

Basi hapa tunahitaji kutambua utofauti mwingine: uzima wa milele unaozungumziwa kwenye Agano Jipya si sawa na kuwepo milele. Wanadamu wote wataishi baada ya kifo cha miili yao; wote watakuwepo milele. Bali baadhi yao wataishi katika hali ya kiroho ambayo Biblia haiiti, kuwa 'uzima wa milele', bali 'mauti ya pili' (Ufunuo 20:11–15; tutasoma mada hii kuelekea mwishoni mwa kitabu hiki).

Hapo baadhi ya wakosoaji labda watasema kwamba mazungumzo yote kuhusu uzima wa milele unaoweza kufurahiwa katika maisha haya ni aina ya kujidanganya wenyewe (*psychological self-deception*). Watasema ni maelezo ya kibinafsi (*subjective*) tu yasiyotoa majibu ya uhalisia wa moja kwa moja kama ulivyo (*objective*). Ila suala hilo hilo lingeweza kusemwa pia kwa mfano wa mtu aifurahiaye kazi ya sanaa na kuikubali; na furaha hiyo ingekuwa uongo vilevile. Kwa kweli, kuna watu ambao wanaweza wakaangalia picha nzuri ya sanaa na wasione kitu zaidi ya rangi kwenye mbao. Watu wasioona (vipofu) hawawezi kuelewa mambo ya sanaa yalivyo, hiyo haimaanishi kwamba kazi ya sanaa haipo, wala kwamba kufurahia picha ya

msanii ni kujidanganya kiakili. Wapo vipofu wa macho, kwa hakika, ambao hata hawatamani kuona. Niliwahi kumfahamu mtu aliyekuwa akiona kidogo alipokuwa mtoto, ambaye baadaye alipoteza uwezo wa kuona na kuwa kipofu kabisa. Mara kadhaa aliniambia kwamba asingetaka kuona hata kama angejitokeza mtu wa kumpa macho. Alikuwa amejikubali jinsi alivyo. Alikuwa anaogopa kama angepata kuona angechanganywa na mambo maelfu ambayo angeweza kuona, na maisha yake yangekuwa magumu. Alipendelea urahisi wa maisha bila kuona.

Vivyo hivyo, kuna wengi ambao wanahisi kwamba maisha yangekuwa magumu sana, na yangewahusisha kwenye mabadiliko mengi, kama wangekubali kuwa Mungu yupo na kuwa wangeweza kupokea uzima wa milele. Wanapendelea urahisi wa kutoamini kuwepo kwa Mungu. Na hivyo wanadai kwamba 'Mungu' na 'uzima wa milele' ni mambo ya kimawazo. Hata hivyo madai yao hayathibitishi kwamba ndivyo ilivyo; zaidi inaonesha kwamba watu hao ni vipofu wa kiroho.

Basi, kuwa na uzima wa milele ina maana gani?

**1. Kuwa na uzima wa milele ina maana ya kushiriki uzima wa Mungu.** Kwa maneno ya Agano Jipya, watu ambao hawajaingia kwenye uhusiano binafsi na Mungu na kumjua yeye, ni wafu – si kimwili bali kiroho.

Habari za Mwana Mpotevu ni mfano maarufu wa kuonesha maana ya matumizi ya neno 'mfu'. Akiongea na mwanawe mkubwa baada ya kurudi kwa yule mpotevu, baba alisema: *"ilibidi kusherehekea na kushangilia kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana"* (Luka 15:32).

Mwana mpotevu alimwasi baba yake, akaondoka nyumbani, na kwenda nchi ya mbali. Hakuwa na upendo, wala haja, na baba yake. Hakuwasiliana naye; hakutaka kujali mambo wala maisha ya baba yake. Kwa mujibu wa baba yake, mwana huyo alikuwa amekufa.

Mwana mpotevu 'aliurejea uzima' baada ya kutubu, kurudi

nyumbani na kupatana na baba yake. Vivyo hivyo, watu waliompuuza Mungu na kuwa wafu kiroho, wanapotubu na kupatanishwa na Mungu, wanaanza kuishi kiroho.

Lakini kuna zaidi ya hilo. Watu wanapotubu na kumgeukia Mungu, sio tu kusema kwamba wanamtambua Mungu, kama mtu anavyoweza kuitambua kazi ya sanaa ambayo hakuwa akiijua. Watu wanapotubu, kumgeukia Mungu, na kuweka imani zao kwa Kristo, Mungu anaweka ndani yao maisha mapya ambayo hawakuwa nayo kabla. Kwa kutumia maneno ya Agano Jipya kwa mara nyingine, Mungu '*aliwafanya kuwa hai*.' Huweka ndani yao pumzi yake ya uhai wa kiroho, kama vile baba anavyopitisha uzima wa kimwili kwa mtoto anayemzaa.

> *Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alitufanya kuwa hai pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema.* (Waefeso 2:4–5)

Angalia mfano huu: Balbu ya umeme, iliyofungwa kwenye kasha lake haitoi mwanga. Itoe kwenye kasha lake, iunganishe kwenye soketi ya taa ndogo, na iweke taa ndogo kwenye chumba ambacho tayari kina mwanga wa kutosha kutokana na taa kubwa kutoka juu. Balbu itakuwa imezingirwa na mianga mikubwa ya taa ya juu; lakini bado haiwaki yenyewe; bado 'imekufa'. Na itaendelea kuwa 'mfu' hadi taa ndogo itakapounganishwa pia kwenye mkondo wa umeme unaowasha taa ile kubwa. Litakapotokea hilo, na mkondo wa umeme ukawasha balbu – tazama jinsi balbu 'inavyofanywa kuwa hai', yaani inavyotoa nuru.

**2. Zawadi ya uzima wa milele huleta mahusiano ya karibu kati ya mpokeaji na Mungu.** Kompyuta ya kisasa inaweza kujifunza namna ya kutambua sauti ya mtu anayeitumia. Kitu atakachohitajika kufanya anayetumia kompyuta hiyo ni kusema tu maneno akiwa karibu na kompyuta yake. Kompyuta itanakili yale yote anayosema mtu na kuandika kimaandishi kwenye karatasi.

Lakini kompyuta hiyo haiwezi kumjua mtu huyo anayeitumia kama anavyojulikana kwa mwanawe au mkewe; haitampenda kama anavyopendwa na vijana na binti zake. Kompyuta haina uzima wa kibinadamu. Bali mtu alipozaa watoto na kuwapitishia uzima wake, pamoja na uzima huo watoto walipokea uwezo wa kutambua na kumpenda baba yao na kufurahia uhusiano wa karibu naye. Vivyo hivyo, Mungu anapopitisha pumzi yake ya uhai kwa watu, na kuwafanya hai na kuwazaa upya, anatengeneza mahusiano kati yake nao; na wanamjua na kumpenda. Hiyo ndiyo maana Agano Jipya linasema kwamba *"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (Yohana 17:3), na kushiriki uzima ule wa Mungu kwa njia ya Kristo (1 Yohana 1:1–4).

3. Uzima wa milele ni zawadi iliyopo na ni umiliki wa milele. Hii inaelezea namna uzima wa milele unavyoweza kuwa, kama linavyojieleza jina lake 'wa milele'. Mungu anapofanya ushirika huu wa kiroho na mtu na kushirikisha uhai wake mwenyewe kwa mtu huyo, uhusiano huo kwa hakika ni wa milele. Mauti ya mwili wa sasa haiwezi kuusitisha, na wala kuuharibu. Mungu anapofanya uhusiano wa karibu na mtu kwa njia ya uzima wa milele, atabaki kuwa mwaminifu kwa mtu huyo na kuendeleza uhusiano huo daima. *"Nami nawapa* [kondoo wangu] *uzima wa milele"*, asema Kristo, *"wala hawatapotea kamwe"* (Yohana 10:28). *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"* (Yohana 3:16).

Basi uzima wa milele hauathiriwi na kufa kwa mwili. Mwili wa mwanadamu, kama tunavyoufahamu hapa duniani, unafananishwa katika Agano Jipya na hema, ambalo linatufaa kwa muda tu, katika safari yetu hapa duniani. Hema hii huvunjika kirahisi, huanguka kirahisi na huweza kubomolewa. Walakini, wakati wa ufufuo kila mwamini atapokea mwili wa utukufu, uliotengenezwa ili kuonesha nafsi yake iliyokombolewa na kukamilishwa, kama inavyofafanuliwa katika Agano Jipya kuwa

*"jengo litokalo kwa Mungu, nyumba. . . iliyo ya milele mbinguni"* (2 Wakorintho 5:1).

Aidha, uzima wa milele utakwenda sambamba na mambo mengine ya milele ambayo Mungu huwapa wote ambao wako tayari kumpokea Kristo. Hivyo Agano Jipya linaeleza kwamba wokovu huo ni wa milele (Waebrania 5:9); ukombozi na matokeo yake ni ya milele (Waebrania 9:12); urithi ulioahidiwa kwa wale wanaomwamini Mungu ni wa milele (Waebrania 9:15); na vivyo hivyo utukufu ule utakaotokana na uzoefu wa maisha na uvumilivu wa mateso kwa wale wanaompenda Mungu ni wa milele (2 Wakorintho 4:17). Na jambo la ajabu kuhusu hili ni kwamba uzima wa milele ni zawadi ya bure, wanayopewa wale wote ambao, kwa toba na imani ya kweli, wamemkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao: *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu"* (Warumi 6:23).

## Uwezekano wa Maendeleo ya Uzima wa Milele

Uzima wa milele, sawasawa na uzima wa kimwili, si kitu kisichobadilika. Mara baada ya kuzaliwa, mtoto huwa na uzima wa kimwili; bali ndani ya wiki, miezi, ama miaka kadhaa mbele atajifunza kujiendeleza katika uwezekano wa maendeleo yake. Ndivyo pia ilivyo kwa uzima wa milele: umejaa uwezekano, na kwa hiyo siku zote kuna matumaini kwa baadaye. Wale waliopokea uzima wa milele wanaaswa na Agano Jipya 'washike' uzima wa milele ambao Mungu amewaitia, kama ambavyo kijana mwenye uwezekano wa kuwa mwanariadha bora duniani anavyoweza kutiwa moyo ili asitelekeze kipaji chake, bali kukitumia kikamilifu (1 Timotheo 4:7–8; 6:11–12). Na thawabu kubwa ya kuendeleza uwezekano wa maendeleo ya uzima wa milele, ni kufurahia maisha hayo zaidi na zaidi. Kama lisemavyo Agano Jipya, *"Yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele"* (Wagalatia 6:8). Kadiri mwanariadha anavyokimbia ndivyo anavyojiimarisha moyo,

mapafu, misuli, na pumzi yake; na kadiri anavyojiimarisha, ndivyo anavyofurahia kukimbia kwake.

Kwa hakika, mazoezi ya hali ya juu yatamlazimisha mwanariadha awe na nidhamu, kujikana, kunia mamoja, na kujituma. Na kama mwanariadha ana tumaini la kushinda medali kwenye michuano ya michezo, lazima azingatie kanuni za mchezo. Kama hatazingatia kanuni hizo, hatapoteza maisha yake, bali kwa hakika hatashinda taji lolote. Na ndivyo ilivyo pia kwa uzima wa milele. Kuimarisha uwezo wake na kuvuna thawabu za juu kabisa, wale walio nao lazima wajiandae *"kuweka kando kila mzigo mzito, na dhambi ile iwazingayo kwa upesi; na wapige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yao"* (Waebrania 12:1). Lazima wawe tayari kujikana, kuchukua msalaba wao kila siku na kumfuata Kristo. Na lazima wajifunze kujitawala nafsi na 'kuzingatia kanuni za mchezo'. Vinginevyo watakataliwa na kukosa tuzo (1 Wakorintho 9:24–27; 2 Timotheo 2:5).

Na jambo la kutia moyo kuhusu uzima wa milele ni hili: huwawezesha wale walio nao kuishi kwa namna ambayo hata uzoefu, majukumu, raha na mateso ya dunia hii ipitayo yanapewa umuhimu wa milele na hivyo kuleta thawabu ya milele (Yohana 12:25; 2 Petro 1:5–11).

**Uwezekano wa kujua kwamba tuna uzima wa milele:** baadhi ya watu, wakiwemo wenye dini, hushikilia kwamba haiwezekani kuwa na uhakika katika maisha haya kwamba tunao uzima wa milele. Kwa hiyo, ni vema kusikia maelezo dhahiri ya Agano Jipya juu ya mada hii. Tutaichambua kwa undani katika sura inayofuata baadaye; ila hapa, kwa kuanzia, ni maelezo yenyewe:

> *Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.* (1 Yohana 5:11–13)

# Sura 8

## Toba

### *Ni Zaidi ya Majuto*

Hadi kufikia hatua hii, tumeshajifunza maneno ambayo yametumika kwenye Agano Jipya kufafanua alichokifanya Mungu ili kupatanisha, kuhesabia haki, kufidia, kukomboa, na kuufanya upya utu. Sasa tunalazimika kuanza kujifunza maneno yanayoelezea tunacholazimika sisi kufanya ili kufaidi kitu ambacho Mungu amefanya, anafanya na bado ataendelea kufanya.

Neno la kwanza kati ya haya ni **toba**. Tangazo la kwanza kabisa la Kristo kwa watu wote lilikuwa ni hili: *"Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili"* (Marko 1:15).

Kwa mujibu wa Kristo, toba ni tukio la furaha kubwa. *"Nawaambia, Vivyo hivyo kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye"* (Luka 15:10). Toba pia ni jambo zuri kwa jumla. Kama mvua ilainishavyo ardhi na kuruhusu mbegu kumea na kukua, ndivyo toba inavyofungua njia ya maisha ya kiroho: *"Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima,"* ndivyo jinsi Agano Jipya linavyofafanua (Matendo 11:18).

Hata hivyo, toba ni jambo lenye sehemu mbalimbali. Ili toba iwe kweli, imara, na yenye matokeo, inahitaji kuwa na sehemu zake zote. Toba kamili, kwa mfano, inaweza kuhusisha huzuni njema pia. *"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletayo wokovu isiyo na majuto"* (2 Wakorintho 7:10). Kwa upande mwingine, huzuni isiyo na toba ndani yake sio tu haina uwezo wa kuongoza wokovuni na uzimani, bali pia huleta mauti na uharibifu. *"Huzuni ya dunia hufanya mauti"* (2 Wakorintho 7:10).

Mfano ulio wazi kuhusu hili ni Yuda aliyemsaliti Kristo. Alipoona kwamba Yesu alikuwa ameshitakiwa, 'alijuta', yaani alighairi. Alijaribu kufuta jambo baya alilokuwa amefanya, ila ikashindikana. Kwa kweli, angeweza kukimbilia msalabani na kumlilia Yesu ili ampe rehema na msamaha jinsi alivyofanya yule mwizi mautini. Bali la, hakufanya hivyo! Aina yake ya toba haikuwa kamilifu wala imara kulingana na Agano Jipya linayotuagiza. Ilikuwa ni huzuni na masikitiko ya kawaida tu. Haikumwongoza uzimani wala kwenye wokovu wake. Kinyume chake — Yuda aliondoka zake na kwenda kujinyonga (Mathayo 27:3–5).

Katika hatua za kutafsiri na matumizi ya kawaida, maana ya toba kwenye Agano Jipya mara kadhaa imebatilishwa na hivyo basi itatubidi kuichunguza kwa makini sana. Kwenye Kigiriki halisi cha Agano Jipya maneno mawili yanatumika kumaanisha **toba**:

1. *Metanoia* na kitenzi cha neno toba, *metanoeo*: Maana ya kimsingi ya maneno haya ni "badiliko la nia". Dukuduku na hisia mbalimbali zinaweza, au zisiweze, kutuelekeza na kutufikisha kwenye badiliko. Badiliko la nia linasababisha hisia hizo. Bado badiliko hilo hasa ni badiliko la kiakili. Yaani ni jambo la uamuzi kimaadili.

2. *Metamelomai* na kitenzi kingine *metamelei*. Vitenzi hivi viwili pia vinatumika kuelezea wazo la toba; lakini vinatia msisitizo zaidi katika huzuni ya kuwa umefanya jambo fulani.

Basi, kimsingi toba ni badiliko la nia, yaani ni vile mtu anavyoenda kinyume cha mtazamo wake wa awali wa kimaadili,

kwa kukana mwenendo wake wa awali. Ndani yake kuna mambo hasi. Hivyo Agano Jipya huzungumza juu ya toba kutoka katika mambo yasiyofaa na maovu; kwa mfano, toba juu ya *"kazi zisizo na uhai"* (Waebrania 6:1). Lakini pia kuna mambo chanya: toba kwa Mungu (Matendo 20:21). Tambua jinsi aya ifuatayo inavyosisitiza mambo ya utambuzi wa kiakili katika toba (mawazo yetu na mawazo ya Mungu), mambo hasi (mtu kuacha njia zake mbaya) na mambo chanya (kurudi kwa Bwana).

> *Mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA, naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa. Maana mawazo yangu (mawazo ya Mungu) si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA.* (Isaya 55:7–8)

## Toba katika maeneo matatu

Kuna maeneo makuu matatu ambayo kwayo tumeitiwa tutubu:

1. Kumhusu Mungu: Ni dhahiri kuwa, ikiwa sisi tunamkana Mungu, toba itamaanisha kubadilika na kutelekeza ukanaji wetu na kukubali kuwepo kwa Mungu. Walakini sio wasiomwamini Mungu tu wanaohitaji toba mbele za Mungu. Inawezekana kuamini katika kuwepo kwa Mungu, lakini usimtilie maanani katika matendo, wala kuzingatia amri zake zote zinazoelekeza kutubu ili kuokolewa, kudharau sheria yake na kuishi kana kwamba hayupo. Kwa njia moja au nyingine, huu umekuwa ndio ukweli unaotuhusu sisi sote. *"Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe"* (Isaya 53:6). Neno 'toba' halina maana nyingine zaidi ya hii ifuatayo: kumgeukia Mungu na kuziacha sanamu (jambo lolote tunaloweka mahali pa Mungu Mmoja wa Kweli) ili kumtumikia Mungu aliye hai, na wa kweli (1 Wathesalonike 1:9).

2. Kuhusu sisi binafsi: Agano Jipya linatumia hatua mbili

tofauti za toba. Kwa kuwa ni rahisi kutogundua jambo hili, tunaanza kwanza kufafanua tofauti kati ya hatua hizo mbili.

Mtu mwenye miaka hamsini hajisikii vizuri. Anamwendea daktari. Baada ya uchunguzi wa kina, daktari anamwambia kwamba chanzo cha maradhi yake ni uvutaji mno wa sigara. "Ndiyo, natambua hilo sasa," anasema yule mtu, "na ninatubu kwa ajili ya hilo. Tafadhali nipe kitu kitakachonisaidia kuiacha."

Vema, mtu yule ametubu kwa dhambi yake ya kuvuta sigara. Lakini daktari akasema, "Vema, ni jambo la busara kwako kuacha uvutaji wa sigara, lakini kuacha kuvuta sigara hakuwezi kukuokoa. Picha zinaonesha mapafu yako yameharibika, na moyo wako pia umeharibika sana. Jambo pekee linaloweza kukuokoa ni kuruhusu daktari bingwa wa upasuaji akupandikize moyo na mapafu mengine ambayo hayajaathirika."

Sasa swali muhimu ni: Je, mtu huyu atakuwa radhi kutubu pia katika hatua hii ya msingi zaidi? Yaani, je, atakubaliana na daktari kwamba hali yake ni mbaya kiasi kwamba kitendo cha kuacha uvutaji sigara pekee hakiwezi kumwokoa: ila tu moyo mpya na mapafu mapya ndivyo vinavyoweza kumwokoa?

Ebu fikiria mtu huyo akikataa agizo la daktari na kusema: "Hapana, mimi si tayari kufanyiwa upasuaji huu mkubwa. Siumwi kama jinsi unavyosema. Nina hakika kwamba kama nitaacha uvutaji sigara, nitakuwa mzima." Je, kitatokea nini? Atakufa baada ya muda mfupi!

Kwa upande mwingine, ikiwa atatubu katika hatua hii, na kukubaliana na uchunguzi wa kina uliofanywa na daktari, akakubali upasuaji, na hivyo kupokea moyo na mapafu ya mtu mwingine, bado itakuwa muhimu kwake kutubu kwa dhambi yake ya uvutaji sigara. Hakika, daktari akishamfanyia upasuaji anaweza kumwambia mgonjwa wakati anaondoka hospitalini: "Ninasisitiza kwamba sasa uache kabisa uvutaji wa sigara na ikiwa umeshindwa katika majaribu na kuvuta sigara tena, njoo kwangu mara moja na ninaweza kukupa kitu kitakachokusaidia kudhibiti jaribu hilo."

Hivyo ndivyo ilivyo na kwetu. Hukumu ya Mungu ni kwamba tuna hali mbaya kiasi kwamba kutubu dhambi moja moja, ingawa ni muhimu sana, haiwezi kutuokoa. Tunahitaji toba halisi au toba ya msingi. Hii humaanisha kukubaliana na hukumu ya Mungu siyo tu kuhusu dhambi zetu, bali pia kuhusu hali yetu wenyewe. Siyo suala la tumefanya nini tu, bali pia jinsi tulivyo. Uamuzi wa Mungu sio tu kwamba tulitenda dhambi hapo mwanzo na kwamba hata sasa bado tunapungukiwa na utukufu wake (Warumi 3:23), bali pia kwa asili yetu sisi ni *"watoto wa hasira"* (Waefeso 2:1–3, taz. 3). Asili yetu imejaa dhambi ambayo ni chukizo kwa Mungu. Hata hivyo hii haimaanishi kwamba kila kitu chetu ni kibaya kabisa. Ila ina maana kwamba hakuna sehemu yoyote ndani yetu isiyoguswa na uharibifu uliosababishwa na dhambi.

Mti hauwi mchungwa kwa kuzaa machungwa. Unazaa machungwa kwa sababu tayari kiasili ni mchungwa. Chuma machungwa yote yaliyo kwenye mti, bado utaendelea kuwa mchungwa! Kuzikiri dhambi zetu tu, ziwe nyingi au chache, ni sawasawa na kuchuma machungwa kutoka kwenye mti. Haigusi wala kushughulika na tatizo la asili jinsi tulivyo ndani mwetu. Ukweli ni kwamba sisi ni, kama Yohana Mbatizaji alivyoeleza, *"miti isiyozaa matunda mazuri"* ambayo inastahili *"kukatwa na kutupwa motoni"* (Mathayo 3:10).

Hata hivyo, kwa hatua hii, watu wengi hukataa kukubali hukumu ya Mungu. Wanakataa kutubu. Wako tayari kukiri kwamba wametenda mambo mabaya, huenda hata matendo maovu ya kikatili. Wako tayari hata kukubali kwamba kuna sehemu za giza kwenye tabia zao. Lakini wanang'ang'ania wazo la kwamba wanachohitaji kufanya tu ni kutubu kwa ajili ya matendo yao maovu yaliyopita, na kuutafuta msaada wa Mungu kuvunja tabia zao mbaya. Wanatumaini kwamba hiyo itawafanya kuwa watu wema kama walivyojihisi kuwa tangu mwanzo; yaani watu wema wenye nafasi nzuri ya kustahili waifikie mbingu ya Mungu.

Lakini huku ni kujidanganya, kama Kristo mwenyewe alivyoeleza: *"Kwa maana hakuna mti mzuri uzaao matunda*

*mabaya, wala mti mbaya uzaao matunda mazuri; kwa kuwa kila mti hutambulikana kwa matunda yake; maana, katika miiba hawachumi tini, wala katika michongoma hawachumi zabibu"* (Luka 6:43–44). Haina maana kwa mti wa miiba kusema: "Ninakiri kuwa nimezalisha miiba michache. Lakini kimsingi mimi sio mti wa miiba: kimsingi mimi ni mtini."

Kwa hiyo, toba halisi na ya msingi humaanisha kuacha mtazamo wetu juu ya maisha yetu na kukubaliana na hukumu ya Mungu kwamba kutubu dhambi zetu mojamoja hakuwezi kutuokoa. Tunahitaji maisha mapya ya kiroho yatokanayo na chanzo kisicho ndani yetu. Chanzo hicho ni Kristo, aliyekufa kwa ajili yetu, na sasa anaishi ili kuwa Mwokozi wetu.

Kwa kweli, hii ndiyo maana ya kihistoria wa ubatizo wa Kikristo. Ubatizo, kama unavyoelezwa na Agano Jipya (Warumi 6:3–4), ni mfano wa mazishi, ambapo mtu huungama hadharani kwamba amekubali hukumu ya Mungu kuwa kitu anachostahili tu ni kuuawa na kuzikwa. Sio upasuaji wa kimiujiza ambao sehemu ya mabaya ya tabia ya mtu huoshwa na kuacha sehemu za wema kukua na kustawi. Katika ubatizo mtu huzikwa mzimamzima, kama jinsi ilivyo duniani ambapo mtu aliyeua anapohukumiwa kifo, mtu huyo hunyongwa mzimamzima na kuzikwa; wala siyo tu sehemu za hasira yake mbaya ama wivu uliomsababisha aue. Vivyo hivyo, mtu anaponyongwa kwa ajili ya mauaji, kifo hicho kinakomesha maisha yake yote. Siyo tu kwamba inafuta maisha yake yaliyopita hadi wakati uliopo, na kumwacha aishi maisha yake yaliyosalia kwa uzuri kadiri awezavyo. Hapana, amefikia mwisho. Maisha yote yamekwishwa kabisa. Kifo hakihitaji, wala hakiwezi, kutokea tena kwake.

Hivyo Kristo alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, alikufa mara moja, wala hatakufa tena, kwa kuwa hatahitaji kufa tena (Warumi 6:8–11). Kifo chake mara moja kililipa deni lote kwa ajili ya dhambi za wale wanaomkubali kama Mwokozi, kwa ajili ya dhambi za maisha yao yote — yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Kwa hiyo, mtu anapobatizwa, papo hapo anaapa kwamba amemkubali Kristo

kama Mbadala na Mwokozi aliyetolewa na Mungu kwa ajili yake. Na kwa kumkubali Kristo amekuwa mmoja pamoja naye, kama mume na mke wanavyokuwa wamoja wanapooana (1 Wakorintho 6:15–17). Kwa hiyo, mbele za Mungu, Kristo alipokufa, mwamini akafa pia, Kristo alipozikwa, naye pia akazikwa; na kwamba kihalali huo ndio mwisho wa nafsi yake ya dhambi milele. Mwamini anasema pamoja na Mtume Paulo: *"Nimesulubiwa pamoja na Kristo"* (Wagalatia 2:19–21).

Hivyo basi, ubatizo pia ni alama ya ufufuo. Unaonesha kuwa kama jinsi Mungu alivyomwinua Kristo kutoka kwa wafu, ndivyo Mungu anavyompa kila mtu anayemkubali Kristo, maisha mapya kabisa ya kiroho. Siyo kwamba maisha ya kale yameshaboreshwa kwa namna fulani, bali amepewa maisha mapya ambayo hakuwa nayo hapo kabla. Siyo kingine bali ni maisha ya Kristo mwenyewe. Hatimaye mwamini anaweza kusema kiukweli kabisa (ili kukamilisha neno la Mtume Paulo):

> *Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.* (Wagalatia 2:20)

Kwa kweli, inatosha kusema kwamba ubatizo ni alama tu. Alama ya ubatizo inaashiria kifo na ufufuo, bila kusababisha kifo wala ufufuo. Ni alama sawa na pete ya ndoa. Mwanamke ambaye hajaolewa angeweza kuvaa pete ya ndoa, lakini hiyo isingemaanisha kwamba sasa ameolewa. Pete itakuwa na maana pale tu atakapoamua kumkubali mwanamume kama mume wake. Hivyo inabidi mtu atubu kwa toba yenye maana halisi ya kimsingi ambayo tumeijadili na yeye binafsi kumkubali Kristo kama Mwokozi kabla ya kubatizwa. Vinginevyo ubatizo utakuwa ni alama-hewa, inayowakilisha kitu ambacho si kweli.

3. Eneo lingine ambalo tunaitiwa kutubu **linahusiana na dhambi zetu**. Mtu ambaye ametubu kweli kweli, na kumpokea

Kristo sasa yuko huru kisheria. Hahitaji tena kuhangaika kujiboresha mwenyewe ili kupata kukubaliwa na Mungu: tayari ameshakubaliwa. Lakini hasa kwa sababu Mungu amemkubali kwa ajili ya Kristo, anatarajiwa kufuata njia ya kweli ya Kikristo. Hiyo inamaanisha asome Neno la Mungu ili agundue mitazamo na matendo gani ambayo Mungu anazihesabu kuwa ni dhambi, na kisha kuzitubu, na atafute nguvu na uwezo wa Kristo kuziondosha. Aangukapo kwenye udhaifu na majaribu, kama inavyomtokea mara kwa mara, anatakiwa kuungama kwa Mungu. Ahadi ni hii: *"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote"* (1 Yohana 1:9). Basi, aina hii ya toba ni kazi ya maishani mwote. Itahitajika kurudiwa kila siku (Ufunuo 2:5, 16, 21; 3:3).

## Baadhi ya Sifa zaidi za Toba ya Kweli

**1. Toba si suala la maneno rahisi tu.** Toba itaonekana katika mwenendo ambao unadhihirisha na kuwa halisi. Yohana Mbatizaji alisema, *"Basi zaeni matunda yapasayo toba"* (Mathayo 3:8).

**2. Hata hivyo, toba peke yake haitunukishi wala kumpatia mtu wokovu.** Msamaha wa dhambi hautegemei kiwango cha huzuni yetu juu ya dhambi, wala hauwezi kupatikana kwa matendo yoyote ya kitubio. Msamaha unabaki kuwa zawadi inayotolewa bure kabisa na isiyotolewa kama mshahara. Msamaha unatolewa kwa wenye dhambi wasio na kitu cha kujivunia na hupokelewa kwa njia ya imani tu. Hiyo ndiyo maana *"kumtubia Mungu"* kunahitaji kuambatana na *"kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo"* (Matendo 20:21).

**3. Toba ni ya muhimu na isicheleweshwe.** *"Mungu sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu"* (Matendo 17:30). Kristo mwenyewe alituhimiza: *"Lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo"* (Luka 13:3, 5).

# Sura 9

## Imani

### *Siyo kuthubutu kuruka bila kuwa na uhahika wa wapi kutua*

Katika sura iliyopita, tumeona kwamba ili kufaidika na mambo yote Mungu aliyotenda kwa wanadamu, anayoendelea kutenda na atakayotenda, ni lazima hatua yetu ya kwanza iwe **toba** mbele za Mungu. Lakini kuna hatua ya pili, ambayo ni **imani** katika Bwana wetu Yesu Kristo (Matendo 20:21).

Kwa mujibu wa Agano Jipya, masharti ya ukombozi ni: (*a*) *"Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana"* (yaani kwa kumkiri kuwa ni Mwana wa Mungu na kwa kumkiri kuwa ni Mwokozi wako), (*b*) *"na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka"* (Warumi 10:9). Swali linaloibuka ghafla ni hili: Je, imani hiyo inakuja vipi basi?

### Matatizo kuhusu Imani: Imani na Elimu ya Sayansi

Siku hizi watu fwengi husikika wakitoa maoni yao: "Tungependa kumwamini Mungu na Kristo, bali sisi inatuwia vigumu sana kuamini. Imani inaonekana kama jambo lisilo na maana kwangu. Kwenye sayansi unaweza kuwa na ushahidi pamoja na uthibitisho,

wala huhitaji kuwa na imani. Bali katika Ukristo unapaswa tu kufanya maamuzi ya kuamini bila ushahidi wala uthibitisho wowote. Ni sawa na kurukia nje kupitia dirishani katikati ya giza totoro, macho yako yakiwa yamefumbwa, huku ukitumaini kwamba utatua salama mahali fulani."

Wengine wanahisi kwamba imani ni namna fulani ya kipaji cha kiusanii: unachoweza ukawa nacho ama usiwe nacho, wala hakuna uwezalo kufanya kuhusu hilo.

Kati ya mitazamo hii hakuna ulio wa kweli. Zaidi pia sio kweli kwamba wazo la sayansi halihusishi imani. Ukweli ni kwamba imani ni muhimu katika jitihada ya kisayansi. Mwanasayansi mahiri, Albert Einstein (1879–1955), aliwahi kusema: "Sayansi inaweza kuundwa tu na watu wenye shauku na nia ya kutafuta ukweli na ujuzi. Chanzo cha hisia hizi zinatoka katika eneo la dini. Eneo hili linajumlisha pia imani kwamba ulimwengu wa vitu vilivyopo unaweza kueleweka kwa akili ya mwanadamu na kwamba kanuni zinazoutawala ni za kimantiki. Siwezi kufikiri kama yupo mwanasayansi wa kweli asiyeshiriki imani hii kwa undani. Tueleze jambo hili kwa kutumia picha: Sayansi bila dini ni kiwete, dini bila sayansi ni kipofu."[1]

Hata hivyo, kumekuwepo wanasayansi na wanafalsafa ambao wamehoji iwapo ulimwengu ambao wanasayansi wanadai kuuelezea, kama kweli upo. Wanapendekeza kwamba, ulimwengu huo upo tu kwenye mawazo ya wanasayansi na kanuni zao za kisayansi. Wanadai kwamba nadharia za wanasayansi hazilingani na ukweli halisi nje ya fikra zao. Lakini ni wazi kwamba, mtazamo huu unasadikiwa na watu wachache sana.

Idadi kubwa ya wanasayansi huamini kwamba ulimwengu wanaouchunguza, ama moja kwa moja au kwa kupitia ala zao, kwa kweli upo. Hawauundi ulimwengu kwa kuangalia, kwa kupima, kwa nadharia tete, kwa nadharia, kwa majaribio na tafsiri zao.

1 *Science and Religion* (1941); *Science, Philosophy and Religion, A Symposium*, New York: The Conference on Science, Philosophy and Religion in Their Relation to the Democratic Way of Life, Inc., 1941; later published in *Out of My Later Years* (1950).

Wanakubali kuwepo kwa ulimwengu kuwa ni ukweli wa kimsingi. Kweli, wamegundua mambo mbambali, kwa mfano, chembe ndogondogo za elementi, ambazo awali hawakufahamu kama zipo. Lakini mambo haya ya ndani yamekuwepo hata kabla ya uvumbuzi wao. Basi, mwanasayansi hauundi ulimwengu kwa tafiti zake – bali anajaribu tu kuufahamu. Na kwa kusudi hilo, anaweka fikra zake chini ya ushahidi unaoonekana katika ulimwengu; hivyo anapima ukweli wa nadharia zake kutokana na jinsi zinavyoweza kuthibitishwa kwa jaribio ili kuelezea ushahidi.

Basi Biblia inasema kwamba ulimwengu upo kwa sababu Mungu aliuweka ili uwepo. Aliuumba. Alitamka ili uwepo kwa Neno lake lenye kuumba (Mwanzo 1; Yohana 1:1–4; Waebrania 11:3). Ni ufunuo wa nia ya Mungu, maelezo ya fikra zake za kiuumbaji. Mwanasayansi anapotafiti ufunuo huu, awe anaufahamu au la, ajue anafikiria mawazo ambayo Mungu alikwisha waza kabla yake. Ndivyo alivyosema mwanasayansi Johannes Kepler (1571–1630).[2]

Vivyo hivyo Biblia inasema kwamba Mungu yule yule aliyejidhihirisha kwa njia ya uumbaji, kwa namna ileile amejidhihirisha kwetu kwa njia ya Mwana wake Yesu Kristo. Kristo hakuundwa na kanisa wala kubuniwa na mawazo ya kidini au ya kitheolojia. Katika Biblia Kristo anaitwa 'Neno la Mungu' kwa sababu katika yeye Mungu amejidhihirisha na kusema nasi, wanaume kwa wanawake, moja kwa moja na kwa upana zaidi ya alivyoweza kwa njia ya uumbaji. Katika uumbaji, Mungu ametuambia kuhusu uweza na ukuu wake. Katika Kristo, Neno la Mungu, amesema yaliyo moyoni mwake. Kwa hiyo jukumu letu ni kutafiti ushahidi unaotolewa na ufunuo wa Mungu mwenyewe katika Kristo, sawa na mwanasayansi anavyotafiti ushahidi unaopatikana kwenye ufunuo wa Mungu mwenyewe katika uumbaji.

Basi ni dhahiri kwamba wanasayansi wanajihadhari kutoa maelezo ya kisayansi yaliyo mepesi mno. Wamejifunza kutokana

2 Kwa kujisomea zaidi kuhusu maelezo ya Johannes Kepler kuhusu Mungu na utafiti wa kisayansi taz. *Harmonices Mundi* (*The Harmony of the World*). Trans. E. J. Aiton, A. M. Duncan na J. V. Field. American Philosophical Society, 1997.

na uzoefu kwamba mambo yasiyotarajiwa yanaweza kujitokeza ulimwenguni tena na tena. Hali hizo zinaweza kuelezwa tu kwa namna inayopingana na ufahamu wa kawaida. Hata hivyo hawakatai moja kwa moja maelezo haya magumu. Badala yake wapo tayari kuamini maelezo ya uvumbuzi wao na sio kufuata ufahamu wa kawaida. Imani yao inathibitishwa mwishoni kuwa ya kweli wanapopanga majaribio ya nadharia zao, na kujikuta zinafanya kazi.

Ndivyo ulivyo ufunuo wa Mungu mwenyewe kwa mwanadamu kwa njia ya Yesu Kristo. Kama tunavyofahamu, Agano Jipya linadai kwamba Kristo ni Mungu na mwanadamu pia. Kwa wengi, kauli hii inaonekana kutofautiana kabisa na ufahamu wa kawaida. Watu wanapokuta kwamba hata Biblia yenyewe haitoi maelezo kikamilifu juu ya namna Mungu anavyoweza kuwa mtu na wakati huohuo kuwa Mungu, wanafikia hatua ya kuiita kauli hiyo hadithi ya kale. Lakini ni vigumu wazo hili kuwa mwitikio wa kisayansi, kama tulivyoona sasa.

Wale waliokutana na Yesu Kristo wakati alipokuwa hapa duniani, awali ya yote waligundua kwamba, kwa hakika, alikuwa mwanadamu halisi. Kwa wakati huohuo, waligundua kuwa alijawa na sifa za kipekee ambazo zilidhihirisha kwamba alikuwa zaidi ya mwanadamu. Maelezo ya Kristo yalikuwa hivi: yeye alikuwa mtu na pia Mungu kwa wakati mmoja. Na kama tukijiuliza namna tunavyoweza kuamini maelezo haya, Agano Jipya linatuelekeza kwenye uchunguzi na majaribio tunayoweza kufanya ili kuthibitisha kuwa maelezo haya ni ya kweli (Yohana 7:16–17; 20:30–31). Hakika, Agano Jipya linasema kwamba Yesu Kristo hakuwa mtu mashuhuri wa kihistoria tu: alifufuka kutoka kwa wafu, naye ni nafsi hai ambaye tunaweza kukutana naye.

## Je, kwa nini tusome Agano Jipya?

Basi katika hili mtu anaweza kupinga: "Hainisaidii kitu kusoma Agano Jipya. Kwani, ili liwe faida kwangu, itanibidi kwanza kuliamini,

hata kabla ya kulisoma, kuliamini kwamba linachokisema ni kweli. Na kwa vile siliamini kuwa ni kweli, hakuna maana kwangu kulisoma." Lakini upinzani huu unatokana na kutoelewa, kwani mtu hana haja ya kuamini kwamba Agano Jipya ni kweli kabla ya kulisoma. Kwa upande mwingine, kama hujawahi kulisoma Agano Jipya kwa umakini zaidi, huwezi kulifahamu kwa usahihi wala kisayansi kwamba si kweli, kabla hujalisoma. Huwezi kuchukua mtazamo huo kuhusu, tuseme kwa mfano, magazeti. Kwa kuwa umesoma magazeti mengi, unafahamu kwamba magazeti yanaweza kuwa na baadhi ya taarifa ambazo si sahihi.

Lakini huwezi kukataa kusoma magazeti kwa sababu hiyo. Unasoma magazeti ukiamini kwamba unaweza kutofautisha ukweli na uongo; na ikiwa kwa wakati huo huwezi kufanya hivyo, unaahirisha uamuzi wako kwa baadaye. Soma Agano Jipya hivyohivyo; na baada ya kulisoma ndipo uamue iwapo Yesu alinena ukweli au uongo. Imani katika Yesu isingekuja kamwe bila kwanza kusikiliza anachokisema. Kukataa hata kumsikiliza, si dalili ya uwezo bora wa akili: bali ni upinzani wa elimu.

Kwa kweli masuala yanayojadiliwa ni makubwa zaidi kuliko unaposoma taarifa kwenye magazeti. Hakika, kama tulivyoona mwanzoni, kigezo cha kwanza cha wokovu, kama Agano Jipya linavyosema, ni kumkiri Yesu kama Bwana! Kwa kweli, hii inahusisha kumkubali Yesu kama Bwana na Kiongozi, na kuwa tayari kumkiri yeye hivyo mbele ya dunia. Na pia inahusisha zaidi ya hilo. Katika Agano la Kale Mungu anasema, *"Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi"* (Isaya 43:11). "Bwana" ni jina jingine la Mungu Muumba. Kama Yesu asingekuwa Bwana huyo, kama asingekuwa Mungu katika maumbile ya binadamu, basi asingeweza kumwokoa mtu yeyote. Madai hayo yana mvuto unaostaajabisha; pia Agano Jipya hakika halitatutaka kuliamini bila kutupa ushahidi ambao kwao tutaweka msingi kwenye imani hiyo. Kwa hiyo swali linabaki, kuna ushahidi gani wa kutuongoza kuamini kwamba Yesu ni Bwana katika maana hiyo?

## Ushahidi wa maelezo ya Kristo mwenyewe

Imani hiyo inaweza kuonekana kana kwamba imepitwa na wakati, lakini sababu kuu ya kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu ni kwamba yeye mwenyewe alisema kuwa ndiye. Hali hii inaibua swali kuhusu ukweli wake. Ni sawa kabisa kuuliza hivyo. Kwani hata pale ambapo ushahidi wote umeelezwa unaoonesha kwa hakika Uungu wake, swali la mwisho ambalo nafsi ya mwanadamu inalazimu kuamua inapokabiliwa na Yesu Kristo ni hili: Je, yeye ni mkweli? Je, ananena ukweli? Tunaweza kuweka thamani gani kwenye maneno yake yanayojirudiarudia akisema, *"Amini, amini, nawaambieni."* Hali ni vivyo kwa Mungu pia. Swali kuu la mwisho siyo "Je, Mungu yupo?" bali "Je, Mungu ni kweli? Anapaswa kuaminiwa?" Mtume Yakobo anataja kwamba hata mashetani nayo yanaamini kuwepo kwa Mungu mmoja (Yakobo 2:19). Lakini hawamtumaini wala kumtii yeye. Vivyo hivyo watu wengi wanaoamini kwamba Mungu yupo, hawamtumaini, wala hawako tayari kuyakabidhi maisha yao hapa duniani ama katika zamani zijazo kwenye ukweli wa neno lake. Wanajisikia hawawezi.

"Lakini huwezi kututazamia kuamini," asema mtu fulani, "kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, eti kwa sababu alisema hivyo mwenyewe. Hoja hiyo haitoshi." Watu wa wakati wa Kristo nao waliibua swali kama hilo kwa kusema *"Wewe unajishuhudia mwenyewe,"* na kutokana na hilo waliamua, *"ushuhuda wako si kweli,"* maana yake ni kwamba, hauna uhalali (Yohana 8:13).

Mara moja Kristo alipinga hitimisho hilo lisilo na msingi: *"Mimi ningawa ninajishuhudia mwenyewe,"* alisema *"ushuhuda wangu ndio kweli; kwa sababu najua nilikotoka na niendako; lakini ninyi hamjui nilikotoka wala niendako"* (Yohana 8:14). Kwa kweli alikuwa anamaanisha mbinguni kama mahali alikotoka na ambapo punde atakuwa anarudi. Alisema kwa mamlaka ya uzoefu wake binafsi. Ilikuwa haina msingi kabisa kwao kuamua kwamba ushuhuda wake Kristo kwa vyovyote usiwe halali, kwa sababu ni yeye peke yake aliyeweza kuwaambia mambo haya.

Ebu tutumie mfano huu: Watu ambao waliishi kwenye bonde la Mediterania mnamo miaka elfu tatu iliyopita walidai kwamba kama ukisimama huku ukiangalia jua la mchana wa saa sita, ni ukweli usiopingika kwamba jua lilikuwa upande wa kusini likiwa limechomoza asubuhi kushoto kwako na baadaye lingezama kulia kwako. Sasa fikiri siku moja angefika mtu mmoja peke yake kutoka Afrika Kusini, wa kwanza kabisa kutoka nchi hiyo kutembelea bonde la Mediterania. Angeweza kusema kwamba kwenye nchi aliyotokea, kama ukisimama ukilikabili jua la mchana saa sita, ni ukweli usiopingika kwamba jua lilikuwa upande wa kaskazini likiwa limechomoza asubuhi kulia kwako na lilitarajiwa baadaye kuzama kushoto kwako. Swali: Je, watu wa asili wa Mediterania watakuwa sahihi kumwamini? Kile ambacho amekisema ni kinyume kabisa na walivyozoea, na kwenda kinyume na sayansi na elimu yao ya ulimwengu wa wakati ule. Nao pia wangeweza kusema: "Ni wewe peke yako unayetuambia hilo. Hatuwezi kuliamini, eti kwa sababu umesema hivyo. Ushuhuda wako si halali. Hatuwezi kuamini kwamba kuna nchi kama hiyo ambapo jua linaenda kama unavyosema."

Kisha anaweza kujibu: "Hata kama ni mimi peke yangu ninayewaambia haya, bado ushuhuda wangu ni halali. Najua nchi nitokayo na ambayo punde nitarejea. Ninyi hamwijui nchi hiyo." Na atakuwa sahihi. Ushuhuda wake ulikuwa halali, na kama wangeuamini, wangekuwa wanaamini ambacho ni sahihi kweli.

Kwa kweli, inawezekana ikawa vigumu kwa watu wa Mediterania kumwamini mgeni kutoka Afrika Kusini; kwani palikuwepo na hadithi nyingi zilizoitwa "hadithi za wasafiri" ambazo zilieleza kuhusu watu waliodai kuwahi kufika katika miisho ya dunia na kuona mambo makubwa yenye kustaajabisha. Lakini hakuna hadithi yoyote miongoni mwa hizo iliyokuwa kweli. Zote zilikuwa ni ubunifu tu. Je, ni vipi basi wangeweza kutofautisha hadithi hizo za wasafiri na kile ambacho mtu kutoka Afrika Kusini alisema? Je, ni kwa njia ipi tunaweza kutofautisha kati ya hadithi za kale za kidini na za kiushirikina na yale ambayo alisema Kristo?

Kristo mwenyewe alijibu maswali hayo kwa kuonesha kwamba, ingawa maelezo yake mwenyewe yalikuwa halali hata bila matendo, palikuwa na ushahidi wa ziada uliothibitisha madai yake: na huo ulikuwa ni miujiza yake (Yohana 5:36). Alisema, alifanya mambo hayo muhimu pasipo mwingine aliyewahi kuyafanya (Yohana 15:24). Kwa haya inatupasa kurejea katika sura yetu inayofuata.

# 10 Sura

## Imani

### *Kuitikia Ushahidi uliopo*

Tulihitimisha sura iliyotangulia kwa kusema kwamba maelezo za Kristo yanathibitishwa na miujiza aliyotenda. Agano Jipya linaiita miujiza yake ishara kwa sababu inaonesha ukweli wa madai yake kuwa Mwana wa Mungu:

> *Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake.* (Yohana 20:30–31)

### Ushahidi wa Miujiza ya Kristo

Mtu mmoja anasema, yote sawa, lakini tuna ushahidi upi kwamba miujiza iliyoandikwa katika Injili ilitokea kweli? Hatukuwepo kuishuhudia ilipotokea. Tunaweza vipi kuwa na uhakika kwamba maandiko haya ni ya kweli? Na miujiza hii ilikuwa na maana gani hasa? Je, si kusema kwamba Biblia inadai kuwa watu wengine, kama vile Eliya, walifanya miujiza pia? Lakini hayo

hayakuthibitisha kwamba yeyote kati yao alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ni vipi basi miujiza ya Yesu ithibitishe kuwa yeye ndiye?

Kwa ushahidi wa kihistoria usemao kwamba Yesu kweli alitenda miujiza, tunategemea shuhuda za mitume wa Kikristo. Hatuna sababu ya msingi kutoamini hizo, kwa kuwa fikra kwamba miujiza haiwezekani haijathibitishwa kisayansi; kwani katika mitazamo fulani (ingawa si yote), fikra hiyo ni wazo ambalo halijathibitishwa wala haliwezi kuthibitishwa.

Basi swali hili si la kisayansi bali la kihistoria: Je, shuhuda za mitume ni za kutegemewa?

Awali ya yote, tunaweza kuwa na hakika kwamba mitume hawakuwa waongo wa makusudi. Mtume Yohana anaelezea kama ukweli thabiti kwamba *"hapana uongo wowote utokao katika hiyo kweli"* (1 Yohana 2:21). Kwa mtazamo wake, uongo haukukubalika hata kama ni kwa nia ya kueneza ukweli mkuu, na kwa vyovyote haupatani na yeye aliyesema kwamba yeye ndiye Kweli (Yohana 14:6), na ambaye alikataza ushuhuda wa uongo kwa nguvu zote (Mathayo 5:33–37). Kwa hiyo, Yohana anapotuambia kwamba yeye na mitume wenzake walimwona Yesu akitenda miujiza mbele ya macho yao, ni wazi anaamini kwamba anaandika matukio halisi ya kihistoria.

Pili, inatubidi kutambua maelezo ya Yohana anapoandika miujiza ya Yesu, si kwamba alikuwa anakariri masimulizi fulani. Yeye na wanafunzi wenzake walikuwa mashahidi wa kwanza. Miujiza wanayotaarifu ilifanyika mbele ya wanafunzi wake (Yohana 12:37).

Lakini cha tatu, na muhimu zaidi, inatubidi kutambua asili ya miujiza ya Kristo. Haikuwa matukio ya kihistoria tu. Inatuletea aina nyingine ya ushahidi unaotupa hata leo changamoto yenye umuhimu kushinda matukio mengine katika historia. Agano Jipya (katika Kigiriki chake) linatuarifu kuhusu hili. Linasema, miujiza ya Kristo haikuwa kazi ya uweza maalum tu (Kigiriki: *dynamis*), wala maajabu makuu tu (Kigiriki: *teras*) ambayo yaliwavuta watu waangalie: pia yalikuwa ni ishara (Kigiriki: *sēmeion*) zilizoelekeza

kwa jambo muhimu zaidi kuliko tendo la mwujiza wenyewe.

Kwa mfano, tukichukua mwujiza wa kulisha watu elfu tano (Yohana 6). Katika hatua ya kwanza ya maana yake, Kristo aliutenda kutokana na huruma zake kwa njaa za kimwili za watu. Lakini hiyo haikuwa sababu yake pekee, wala sababu yake kuu. Katika hali ya kawaida, watu walipata njaa hata siku iliyofuata. Lakini maandiko yenyewe yanatuambia kwamba walipomwendea Yesu wakitaka aurudie huo mwujiza, alikataa kuurudia. Kwa nini? Kama alikuwa na nguvu hizi za miujiza, kwa nini hakuendelea kuzitumia siku baada ya siku hadi njaa ya kimwili itoweshwe kabisa duniani? Na kwa nini haendelei kuifanya leo? Alisema, kwa sababu walishindwa kuona au kwa makusudi hawakujali maana kuu ya umuhimu wa ishara hii ya mwujiza (Yohana 6:26). Mwujiza uliwajulisha ukweli kwamba Yesu alikuwa Muumba wao katika maumbile ya binadamu, na zaidi kwamba yeye alikuwa ameshuka kutoka mbinguni kujitoa kwao kama Mkate wa Uzima ili kukidhi njaa yao ya kiroho. Tumbo, kama sehemu ya mwili, linaweza kushibishwa na vitu vya kimwili. Bali roho ya mwanadamu, kwa kuwa inatokana na Mungu ambaye ni roho, haiwezi kushibishwa na vitu vya kimáwili wala na raha za uzuri wa kisanaa na changamoto za kiakili. Roho ya mwanadamu inahitaji ushirikiano na mwingine, na huyo Mwingine ndiye Muumba wake. Pasipo yeye, roho ya mwanadamu imeshahukumiwa kubaki na njaa ya kudumu, ambayo hata miujiza elfu kumi haiwezi kuishibisha.

**Kwa hatua hii sisi wenyewe tunaweza kuupima ukweli wa simulizi kuhusu mwujiza huo.** Habari hii inatambua hitaji fulani la binadamu. Inasema tuna njaa ya kiroho, ikiwa tunafahamu au hatufahamu tuna njaa kwa ajili ya nini (au ya nani). Hii ni kweli? Tunaijua mioyo yetu wenyewe; kila mmoja wetu anaweza kuamua iwapo utambuzi huo ni kweli.

Kwa kweli watu wengi wamefundishwa na kuelezwa kudhibiti njaa zao za kiroho. Baadhi yao wamefanikiwa na kutoka moyoni mwao watadai kwamba hawasikii uchungu wa njaa ya kiroho. Lakini hiyo inaweza kuwa dalili ya onyo la hatari. Tunaambiwa

kwamba watu wanapokuwa na njaa ya kimwili bila chakula chochote, mwanzoni huwa inauma sana. Lakini baada ya muda fulani uchungu unatoweka na haurejei hadi kifo kinapowakabili bila kuepukika. Inawezekana ikawa hivyo pia kwa njaa ya kiroho hadi mpaka hatua yake ya mwisho, yaani mauti ya pili.

Lakini kwa wale wanaotambua njaa yao ya kiroho, Kristo anajitoa kwao kama Mkate wa Uzima. Je, wanaitamani sehemu hii ya kiroho ya maisha yenye ushirika wa milele na Mungu, ambayo huanzia hapa duniani na kuendelea mbali zaidi ya kaburi hadi mbinguni kwa Mungu? Kristo anatuhakikishia kwamba anaweza kutupa hayo (Yohana 6:28–58). Je, wanapenda roho zao ziwekwe huru kutoka katika kivuli cha laana kilichowekwa juu yake kwa ajili ya hatia na utumwa wa dhambi? Kristo anaweza kuwapa hilo pia kwa njia ya kifo chake (Yohana 8:31–36).

Ni vipi basi tunaweza kujua kwamba yeye ni kweli, kwamba yeye ni Muumba wetu katika maumbile ya binadamu, kama alivyosema? Ni kwa njia ileile tunayojua kuwa kipande cha mkate kinaweza kukidhi njaa zetu za kimwili kwa kuujilia, kuuamini, kuuchukua na kuula. Hivyo anavyosema Kristo kwa wale wanaokubaliana naye kuwa njaa yao ya kiroho kweli ipo: *"Mimi ndimi mkate wa uzima. Anayekuja kwangu hataona njaa; anayeniamini hataona kiu kamwe"* (Yohana 6:35, Habari Njema). Wale wanaomfuata na kumwamini wanagundua kwamba yeye ni kweli.

Lakini sasa tunageukia ushahidi wa aina nyingine unaotofautiana na ule ulioletwa na miujiza ya Kristo.

## Ushahidi unaoletwa na Kifo cha Kristo

Kwa mujibu wa Agano Jipya, Mungu hakupanga kwamba miujiza ya Kristo iwe njia pekee ya kutuvuta tumwamini wala kwamba isiwe njia kuu. Bali zaidi ni kifo cha Kristo msalabani:

> *Wayahudi wanataka ishara (hiyo ni miujiza), na Wagiriki wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulubiwa. . . Maana naliazimu*

*nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, na yeye aliyesulubiwa. . . ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu. . . Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu.* (1 Wakorintho 1:22–23; 2:2, 5; 1:18)

Ni kwa vipi basi msalaba wa Kristo unatuvuta kuamini kwamba yeye ni Muumba wetu aliyefanyika mwili, Mwana wa Mungu Aliye hai? Inakuwa hivyo kwa sababu **msalaba wa Mwana wa Mungu unadhihirisha wazi namna Mungu alivyo.**

Kwa kweli, ikiwa siku moja mioyo yetu itamwamini, kumpenda na kumtegemea Mungu, inatubidi kwanza kujua moyo wa Mungu ukoje. Basi falsafa haiwezi kutuambia hilo. Inaweza kukisia kuhusu Mungu, lakini haiwezi kutuambia yaliyo moyoni mwake. (Haiwezi hata kutuambia kinachoendelea moyoni mwa jirani yetu.) Hata uumbaji wa Mungu hauwezi kutuambia. Unatuwezesha kuona uweza wake; bali hauwezi kutuonesha kwa uwazi kabisa moyo wake. Ili kwa hakika tupate kujua mtazamo wa moyo wa Mungu kwetu, Mungu alihitaji kuchukua hatua ya kwanza na kujidhihirisha mwenyewe. Alihitaji kufanya hivyo kwa namna ambazo sisi wanadamu tungeweza kuelewa. Hivyo, Neno la Mungu alifanyika mwili.

Basi hapa ndipo, tuseme, Mungu alikuwa na tatizo; na lilikuwa ni tatizo ambalo Kristo alieleza kwa watu wa wakati wake. Watu hao, bila moyo mweupe, walipendekeza kwamba ili apate kuaminika na kuungwa mkono na umma alilazimika kutafuta kujitangaza kwa hali ya juu na kuonesha mlolongo mrefu wa miujiza ya kushangaza. Lakini hawakuelewa shida ya kimsingi. *"Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi," alisema, "bali hunichukia mimi, kwa sababu mimi naushuhudia ya kuwa kazi zake ni mbovu"* (Yohana 7:1–7, hasa 7). Ushuhuda wake haukutokana na kiburi cha kujiona bora wala katika mawazo finyu ya kutowapenda watu wa dini tofauti. Alikuwa ni chapa kamili ya Mungu, alikuwa ni mawasiliano ya Mungu mwenyewe kwa njia ya kibinadamu. Kwa

hiyo, alidhihirisha utakatifu wa Mungu kwa kiwango ambacho kilikuwa hakijawahi kuonekana kabla. Na jinsi alivyozidi kufanya hivyo, ndivyo alivyozidi kuifunua hali ya wanadamu kuwa wenye dhambi, ndivyo pia watu walivyozidi kuchukizwa naye na kuzidi kupinga maelezo yake kuwa Mwana wa Mungu.

Hiyo inaeleweka. Kwa mfano, kama rafiki yako akisema kwamba jambo fulani ulilofanya lilikuwa ovyo, tendo baya kupitiliza, mwanzoni unaweza pia kuchukia usemi wake; lakini baada ya muda, unaweza kujifariji kwa kudhani kwamba hayo yalikuwa maoni yake tu. Kwani yeye ni nani? Kwa hiyo ukaamua kutojali na kuendeleza urafiki wako naye. Lakini kama mtu atakuambia kwamba wewe ni mtenda dhambi unayestahili hukumu ya Mungu, na kisha akaongeza, "Nami nikuambiaye haya ndimi Mwana wa Mungu." Kama kawaida kwanza ungeitikia kwa kubeza madai yake ya kuwa Mwana wa Mungu. Kisha akiendelea kusisitizia jambo hilo, ungelikataa kwa nguvu zote. Maana kama angekuwa sahihi, unabaki kuwa mwenye hatia.

Mshairi wa kale wa Kilatini, Lucretius (99–55 K.K.), alitunga shairi katika vitabu sita virefu na vizuri, akieleza nadharia ya awali ya Kigiriki ya atomi na hata nadharia ya wakati wake ya mageuzi (*evolution*) kwa manufaa ya Warumi wenzake. Humo anakiri katika utangulizi kwa nini nadharia hizi zilimvuta kwa nguvu.[1] Awali ya yote zilionekana kwake kuthibitisha kwamba mwisho wa kila jambo ni kifo: hakuna chochote baada ya kufa; na kisha wazo hili lilimwondolea matarajio yote na hofu ya adhabu kwa dhambi zake katika maisha yajayo. Kwa hiyo alihubiri nadharia hizi kama mwinjilisti wa hali ya juu.

Bado iko hivyo kwa watu wengi. Wanapokubali madai ya Kristo ya kuwa Mwana wa Mungu, kwa ghafla wanajihisi kupatwa na hofu ya Mungu Mtakatifu, ya hukumu ya mwisho, na adhabu kwa dhambi. Kwa hiyo, wanayakataa maelezo hayo na kukataa kushawishika na madai yake. Kwa hali hiyo, kama Kristo

1 *De Rerum Natura*, Kitabu cha 1.

angefanya mlolongo wa miujiza yenye kuonesha uwezo usio wa kawaida, ingeongeza hofu ya watu, kuimarisha upinzani wao, na kuwasukuma kutafuta maelezo mbadala ya nguvu za Kristo. Kwa hiyo basi, Mungu alitegemea msalaba wa Kristo zaidi kuliko miujiza yake kwa kupata mioyo ya wanadamu. Kristo mwenyewe alituliza uhasama wa wapinzani wake waliochukizwa na jinsi alivyozifunua dhambi zao. Basi Yesu akawaambia, *"Mtakapokuwa mmekwisha kumwinua* (yaani, kumsulubisha) *Mwana wa Adamu, ndipo mtakapofahamu ya kuwa mimi ndiye* (Mungu, Muumba, na Bwana wenu)*; na ya kuwa sifanyi neno kwa nafsi yangu, ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo"* (Yohana 8:28).

Kwa kweli Mungu huifunua dhambi yetu kwa njia ya msalaba wa Mwana wake. Wala si kuifunua tu bali anaionesha mbele ya uso wa ulimwengu mzima. Mioyo ya wanadamu imejitenga na kumwasi Mungu kiasi kwamba, walipopewa nafasi ya Mungu kufanyika mwili, wanadamu waliweza kumsulubisha Muumba wao, na hata wamefanya hivyo kweli. Kwa kweli Mungu pia aliudhihirisha utakatifu wake usiopungua kwa njia ya msalaba wa Mwana wake. Dhambi haiwezi kufanya chochote zaidi ya kupokea hukumu ya machukizo yake yasiyobatilika. Ni lazima dhambi iadhibiwe.

Lakini sambamba na hilo, na zaidi ya jambo liwalo lote, Mungu huelezea habari zote za moyo wake kwa viumbe wake kwa njia ya kifo cha Mwana wake. Ingawa wamedanganywa na Shetani, na dhambi imewafanya kuwa maadui wake, Mungu anaendelea kuwa mwema kwao. Anawapenda kwa upendo ambao Muumba pekee ndiye anayeweza kuwa nao kwa viumbe wake. Hataki kwamba yeyote kati yao aangamie, bali kwamba wote waweze kufikia toba (2 Petro 3:9). Badala ya wanadamu kuangamizwa katika adhabu ya dhambi, Mungu alilipa adhabu hiyo kwa gharama ya mateso ya Mwana wake mwenyewe. Hivyo kwa haki aweze kutoa ukombozi kamili na wa milele kwa wote.

Msalaba unatangaza kwamba Mungu anataka watu wote waokolewe na wapate kuujua ufahamu wa kweli, yaani, kutambua

jinsi Mungu alivyo na kwa jinsi anavyojisikia moyoni juu yao. Ili kuionesha dunia jinsi moyo wa Baba ulivyo, Mwanawe amejitoa kuwa fidia kwa ajili ya wote, ili kumwezesha Mungu kufaulu katika nia ya pendo lake (1 Timotheo 2:3–6). Pendo lake kamili lina hamu ya kuitupa nje hofu yetu yote (1 Yohana 4:18).

Hivyo, msalaba wa Kristo ni kielelezo kamili cha upendo wa Mungu tangu mwanzo na hata milele. Hakuna raha iwayo yote ya mbinguni itakayoelezea pendo la Mungu kikamilifu zaidi kuliko hatua ya kumtoa Mwana wake pale Kalvari. Kwa hali hiyo huu ni ujumbe wa mwisho wa Mungu; hana mivuto mingine mingi yenye uweza na utukufu wa kutushawishi tumwamini na kumpenda.

Swali ni je, tunaweza kutambua upendo wa Mungu mara tunapouona? Pamoja na kuwa viumbe wapole, kondoo wanaweza kutumia silika kutambua upendo na huduma ya mchungaji halisi pindi wanapokutana naye. *"Mimi ndimi mchungaji mwema,"* asema Kristo. *"Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo"* (Yohana 10:11). *"Katika hili tumelifahamu pendo,"* asema Mtume Yohana, *" kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu"* (1 Yohana 3:16). Tena Kristo asema, *"Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi. . . Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo. . . Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu"* (Yohana 10:14–17).

Kwa hiyo swali ni: "Je, huyu Yesu aliyesulubiwa na kufa msalabani kwa ajili yetu (kama alivyosema) – je, huyu Yesu ni Mwana wa Mungu?" Swali hili ni la kipekee. Hakuna kiongozi mwingine wa dini ama mwanzilishi wa dini za dunia atakayesimama mbele yako, akijieleza mwenyewe moja kwa moja kwako kwa kusema: "Mimi ndimi Muumba wako. Na kwa kuwa mimi ndimi Muumba wako, nakupenda jinsi ulivyo, pamoja na dhambi zako. Na ushahidi ni huu hapa: Mimi mwenyewe nilikufa kwa ajili yako."

Basi, maelezo ya Kristo ni ya kustaajabisha. Lakini bado kuna ushahidi zaidi wenye kuonesha kuwa ni ya kweli.

## Ushahidi unaoletwa na kufufuka kwa Yesu

Inafahamika kote kwamba kufufuka kwa Yesu Kristo ni nguzo kuu ya Ukristo. Pia Agano Jipya linasema wazi kwamba kufufuka kwa Kristo na kupaa kwake mbinguni hazikuwa dhana ngumu za kitheolojia ambazo Wakristo wa zamani wangehangaika kuamini. Yalikuwa ni matukio mawili makuu yaliyofungulia uwezo ambao uliwabadili wanafunzi wa kale kutoka kuwa watu wenye hofu hadi kuwa wahubiri wa injili wasiotishika. Badala ya kupunguza imani yao, kufufuka kwa Kristo kulizidisha hiyo imani mara elfu. Wanafunzi hawa waliona matukio ya kweli ya Mungu aliye hai kwa jinsi ambayo hawakuwahi kujua hapo awali. Sikia jinsi ambavyo walisema:

> *Kupitia kwake (Kristo) mmekuwa wenye kumwamini Mungu, aliyemfufua katika wafu akampa utukufu; hata imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu.* (1 Petro 1:21)

Tumaini lao pia liliongezeka sana. Bila Mungu, kifo ni hitimisho la tumaini lote, heshima yote ya mwili ikiwa imetoweka. Mwishoni watu wanaacha kucheka na wanakata tamaa kwa kuwa mahangaiko yote ya maendeleo yanasitishwa. Lakini kufufuka kwa Kristo kulibadili yote hayo. Kama anavyosema Mtume Petro:

> *Mungu. . . ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.* (1 Petro 1:3–4)

Mapema sana Wakristo wakaona kwamba kufufuka kwa yule mwanadamu, Yesu Kristo, kulifungua milango ya utukufu wa milele kwa watu wote waliokombolewa. Kwa hiyo kufufuka kwa Yesu kulikuwa ni limbuko na ahadi ya ufufuo wao wenyewe (1 Wakorintho 15:20–23).

Zaidi, ufufuo wa Kristo ulileta hali ya pekee: Wakristo wa kale, hata wale ambao hawakumwona Yesu, hakika walimpenda. Sikiliza jinsi walivyonena:

> *Naye* [Yesu Kristo] *mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamumwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana; kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu.* (1 Petro 1:8)

Kama ye yote angesema, "Nampenda Lucky Dube" ungemchukulia kuwa anamaanisha "napenda muziki wake," wala si "nampenda Lucky Dube mwenyewe." Hakuna ambaye atashikilia msimamo wa pili, hautaleta maana. Lucky Dube alishafariki; huwezi kumpenda mtu aliyekufa. Hata mjane kwa kawaida husema: "Nilimpenda mume wangu," na wala sio "Ninampenda mume wangu."

Lakini hivyo ndivyo Wakristo wote wanavyozungumza kuhusu Kristo. Yesu kwao sio tu mtu fulani wa kihistoria, wala mwalimu mwema aliyeishi awali – ni mtu anayeishi. Ijapokuwa hawajawahi kumwona, wanampenda, wanazungumza naye (kwa njia ya maombi), wanamsikiliza akizungumza nao moja kwa moja (kwa njia ya Biblia), wanamwimbia, wanamwabudu, na wanaishi maisha yao kwa uweza wake ili kumpendeza yeye. Hiyo ni aina ya imani inayoletwa kutokana na ukweli wa ufufuo.

"Lakini si lazima iwe kweli," asema mtu fulani. "Uzoefu huu wote hutokea kwa watu ambao awali ya yote hudhania kwamba ufufuo wa Kristo ni tukio la kihistoria. Wanajishawishi wenyewe kwamba Yesu yuko hai, na kuunda picha nzuri juu yake katika fikra zao, na kupenda picha hiyo. Kwa hakika hii ni hali ya mawazo yaliyobuniwa tu moyoni mwa mtu. Kuna ushahidi gani wa kihistoria, usio wa upendeleo, kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu?"

Jibu ni kwamba: kuna mkusanyiko wa ushahidi wa aina nyingi, wenye uwezo wa kuthibitisha, na unaotokana na vyanzo mbalimbali vya kihistoria. Vielelezo na matukio yafuatayo yanathibitisha hayo.

**1. Ushahidi wa kaburi tupu**: Ni dhahiri kabisa kutoka kwenye maandiko ya Agano Jipya kwamba watu wa kwanza kulitembelea kaburi la Kristo, Jumapili baada ya kuzikwa, walitegemea kuukuta mwili wa marehemu ukiwa bado kaburini. Walikuja na manukato ili kuipaka maiti, hatua iliyodhamiriwa kuitunza maiti kwa muda mrefu kadiri wawezavyo. Walipotoa taarifa kwa mitume kwamba walikuta kaburi likiwa tupu, mitume nao walipatwa na mshangao mkubwa; kisha Yohana na Petro kwa haraka walikimbia kwenda kwenye pango la kaburi kujaribu kuelewa nini hasa kilikuwa kimetokea (Yohana 20:1–10). Wametuambia walichokikuta. Kaburi halikuwa tupu kabisa. Mwili wa marehemu haukuwepo, lakini sanda iliyokuwa imefunika maiti baada ya taratibu za mazishi ya Kiyahudi ilikuwa bado pale mahali ambapo mwili ulikuwa umelazwa, isipokuwa tu kwamba sasa ilikuwa tupu. Kitambaa ambacho kilikuwa kimezungushiwa kichwani kilikuwa pembeni kidogo mwa nguo zingine, kwa juu ya mwegemeo uliokuwa umechongwa kama mto wa kuegemezea kichwa cha maiti.

Wanafunzi hawa wawili wanatuambia kwamba huu ulikuwa ushahidi wa kwanza uliowafanya kuamini kwamba Yesu lazima atakuwa amefufuka kutoka kwa wafu: mwili ulitoka kwenye sanda pasipo kuivuruga. Maelezo gani mengine yangepatikana pale? Walijua kwamba hakuna yeyote kati ya mitume wengine aliyeuondoa mwili. Wala hawakuweza kumfahamu mtu awaye yote aliyefanya hivyo, kwa sababu mamlaka ya Kirumi ilikuwa imeweka askari kulilinda kaburi kwa kusudi hili la kuzuia yeyote asiuibe mwili na kudanganya kuwa amefufuka.

Ilikuwa ni askari hao ambao, baada ya kutokuta mwili pale ulipolazwa, wakaanza kuzunguka mitaani na kueneza uvumi kwamba wanafunzi walikwenda na kuuiba mwili walipokuwa wamelala (Mathayo 27:62–66; 28:11–15). Lakini uvumi huo unaonekana wazi kutokuweza kuaminika – waliweza vipi kuona kilichotokea ikiwa walikuwa wamelala? Lakini kwa undani zaidi, ni vigumu kuamini kwamba baadhi ya wanafunzi waliwavuka walinzi, wakaondoa jiwe kubwa lililokuwa limewekwa mlangoni

mwa kaburi, wakaiba mwili, wakauficha, na kisha wakapanga uongo kwamba Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Ni vigumu kuamini hivyo kutokana na sababu hizi mbili zifuatazo.

2. Mwenendo wa mitume wakati wa misukosuko ya kutetea imani yao: Charles Colson alikuwa mmoja wa wasaidizi wa marehemu Rais Nixon aliyepanga njama ya kutengeneza hadithi ili kuficha kitendo cha jinai cha Rais cha kuvamia ofisi za wapinzani wake wa kisiasa – ya kile kilichoitwa "Kashfa ya Watergate". Kwa muda fulani wanaume hawa wakakamavu walishikilia msimamo kwenye hadithi yao ya uongo. Lakini msukumo ulipoongezeka na tishio la adhabu kali kutolewa, mmoja baada ya mwingine akawasaliti wenzake na kukiri ukweli. Waliona wasingeweza kuvumilia mateso kutokana na uongo ambao wao wenyewe waliutengeneza.

Kutokana na uzoefu wake mwenyewe Colson alifikia hitimisho hili. Ukiwaangalia mitume utaona, walikuwa ni wanaume ambao hawajaimarika kisiasa na kidiplomasia. Kama maelezo yao kuhusu ufufuo yalikuwa ya uongo uliotokana na njama zao, basi pale waliposhinikizwa na msukumo mkubwa uliowakabili baada ya muda mfupi wasingeweza kuendelea kushikamana: mmoja baada ya mwingine miongoni mwao angeweza kuvunja kiapo na kukiri kwamba suala zima lilikuwa udanganyifu. Lakini hakuna yeyote kati yao aliyefanya hivyo: ama hata pale walipoona watu wengi wakiteswa na hata kuuawa kwa kuamini ushuhuda wao wa ufufuo kwa moyo mweupe, au hata pale wao wenyewe walipoteseka na kuuawa kwa ajili ya huo.

Hata kama tukikubali ya kwamba Mitume wangejitahidi kukazana mshikamano wao kwa wao waliposhinikizwa na kutishiwa, ushuhuda wao ungemshawishi vipi mtu kama Sauli wa Tarso?

3. Ushuhuda wa Sauli wa Tarso: Mara kadhaa imekuwa ikisemwa kwamba ushahidi wa kufufuka kwa Kristo unadhoofishwa kwa hoja kwamba unatoka kwa Wakristo. Hivyo inadaiwa kwamba hakuna asiye Mkristo ambaye amewahi kushuhudia kwamba

Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Ila siyo hivyo. Wote ambao sio Wakristo wakishaondoa mashaka kuhusu kufufuka kwa Yesu kwa kawaida kinachofuata kwamba wanakuwa Wakristo. Lakini jambo la kuzingatia ni kwamba hawakuwa Wakristo kabla ya kushawishika kusadiki ufufuo wake; na ilikuwa ni kufufuka kwake kulikowashawishi.

Mfano mashuhuri hapa ni Sauli wa Tarso. Kabla ya kuongoka kwake siyo tu kwamba alikataa kumwamini Yesu na habari za kufufuka kwake: bali pia alitumia nguvu nyingi kuwatesa wote ambao walimwamini. Basi tukio la kubadilishwa kwa Sauli wa Tarso ni la kihistoria na lisilo na utata. Dunia bado ina alama za matokeo yake. Basi, nini kilisababisha kubadilishwa kwake? Sauli mwenyewe anasema, Kristo aliyefufuka na aliye hai ambaye hapo kabla alimfikiria kuwa alikuwa amekufa na kuzikwa, alimtokea akiwa njiani kwenda Dameski (Matendo 9).

Mtu anaweza kudai kuwa Sauli alikuwa ni mfano maalum. Lakini hakuwa mfano pekee wa mtu aliyeshawishika kusadiki ufufuo kwa njia ya Kristo aliye hai kujifunua kwake mwenyewe .

**4. Mwenendo wa wanawake Wakristo wa kale**: Watu wa kwanza kutembelea kaburi la Kristo siku ya tatu, walikuwa ni wanawake Wakristo kadhaa ambao walikuja kuupaka mwili mafuta. Kama wangeachiwa wenyewe, bila shaka wangebadilisha kaburi kuwa mahali patakatifu na mahali pa kuhiji, kama ilivyofanywa kwa viongozi wengine wengi wa dini, kama ilivyofanyika pia baadaye na baadhi ya watu wenye mtazamo wa ushirikina ndani ya utamaduni wa Kikristo. Lakini wanawake hao hawakufanya hivyo. Wao, na Wakristo wote wa kale, walilitelekeza kaburi. Kwa nini? Kwa sababu walilikuta likiwa tupu, na kisha wakakutana na Bwana Yesu mwenyewe, aliyefufuka kutoka kwa wafu. Hakuna anayefanya mahali patakatifu kwa kumkumbuka aliye hai! (Mathayo 28:1–10; Yohana 20:11–18).

**5. Ushuhuda wa waliomwona kwa macho yeye aliyefufuka**: Waraka wa kwanza kwa Wakorintho ni mojawapo ya barua za mwanzo kabisa za Paulo. Kwenye sura ya 15 (aya ya 3–8)

alieleza injili kwa kifupi. Ilijumuisha siyo tu tangazo la kwamba Kristo alifufuka kutoka kwa wafu mnamo siku ya tatu, bali pia orodha ya mashahidi ambao kweli walimwona Kristo baada ya kufufuka kwake. Orodha hii haimaanishi kuwa imejitosheleza; lakini inaonesha kwamba watu mbalimbali walimwona kwa macho. Mazingira ambayo walimwona Kristo pia yalitofautiana: baadhi walikuwa peke yao; baadhi walikuwa kwenye vikundi vidogo; wengine walikuwa kwenye kundi la watu zaidi ya 500. Vinginevyo tunajifunza kwamba Kristo alijitokeza kwa baadhi ya watu jioni, milango ikiwa imefungwa kwa hofu (Yohana 20:19–23), kwa wengine mchana kweupe kwenye ukingo wa mlima (Mathayo 28:16–20), na kwa wengine asubuhi ufukoni mwa bahari wakiwa kwenye mitumbwi yao ya uvuvi (Yohana 21), na kwa wengine wakiwa safarini (Luka 24). Ingekuwa vigumu kudai kwamba watu hawa wote tofautitofauti walikuwa wenye kuota ndoto (*hallucination*) au kushikwa kwa pamoja kwa kupumbazwa akili (*hypnotism*).

Basi kuna ushahidi mwingi zaidi wa kihistoria kama huo ambao ungeweza kunukuliwa. Lakini tunahitaji kuangalia kipingamizi kingine: "Kufuatana na Agano Jipya, ilibidi mitume wamwone Kristo aliyefufuka kwa macho na kumgusa kwa mikono yao, kabla ya kuwa tayari kusadiki ufufuo wake. Hivyo unawezaje kutegemea kwamba niamini, bila hata mimi mwenyewe niweze kumwona na kumgusa?"

Pingamizi linaeleweka; lakini halina sababu kama linavyoweza kuonekana kwanza. Ebu tutumie mfano. Fikiria kwamba nimetokea katika eneo duni sana na sijawahi kuona umeme. Nikakutembelea nyumbani kwako nawe ukaniambia: "Bonyeza hiyo swichi kwenye ukuta wa chumba chako na mwanga utatokea." Nikakuuliza: "Hilo linawezekanaje?" Nawe ukajibu: "Mwanga unatokana na umeme unaotokea kwenye mitambo iliyoko kilomita kadhaa toka hapa." Mimi nauliza: "Je, umewahi kuuona umeme huu?" Unajibu: "Hapana." "Umewahi kuona kituo cha mitambo ya umeme?" Unakiri: "Sijawahi kufika huko." Nami naendelea kuuliza:

"Kwa nini basi unaiamini mitambo hii na umeme huu?" Kwa utulivu unanielezea: "Tulipohamia katika nyumba hii, kuna mtu alitutembelea na kujitambulisha kuwa anatoka kwenye shirika la umeme. Alitueleza kwamba nyumba yetu kwa wakati huo ilikuwa imekatiwa umeme, lakini alikuwa anaenda kwenye kituo cha mitambo ya umeme na kutuunganisha. Kisha umeme ungefika; na kama tungebonyeza swichi, mwanga ungetokea. Tukamwamini alichosema, tukabonyeza swichi, na mwanga ukatokea. Sasa basi, nawe pia nenda chumbani mwako, kabonyeze swichi na mwanga utatokea."

Fikiria kama ningekujibu hivi, "Hapana, siko tayari kufanya hivyo. Naweza kuwa najidanganya mwenyewe kwa kudhani nimeona mwanga ukitokea. Nasisitiza, inanipasa nami kumwona mtu aliyetoka kwenye kituo cha kusambaza umeme kwanza, kama ilivyotokea kwako, kabla sijabonyeza swichi yako."

Ungeweza kufikiri kuwa nilikuwa mwendawazimu.

Basi, mitume wanatuambia kwamba, kabla ya kifo chake na baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwaambia kwamba kwa hakika angewaacha. Alikuwa anarudi kwa Baba mahali alipotoka, ili kwamba aweze kumtuma Roho Mtakatifu kwao (Yohana 16:7–14, 28). Walihitajika kusubiri Yerusalemu kwa siku kadhaa na kisha wangempokea Roho Mtakatifu. Kisha akawaacha na kupaa mbinguni (Matendo 1:4–9). Waliyaamini maneno yake, wakasubiri kama walivyoambiwa, na kisha wakapokea Roho Mtakatifu, na katika yeye walipata mwanga, amani, na uweza wa kuishi maisha ya kushirikiana na Mungu kila siku.

Kisha waliwaambia watu wa siku zao kuwa wakiwa wanatubu dhambi zao na kumwamini Kristo, nao watampokea Roho Mtakatifu pia (Matendo 2:38). Hawakuweza wala wasingeweza kumwona Roho Mtakatifu mwenyewe; lakini waliweza kukutana na nuru na uweza wake. Mitume wanatuambia hivyohivyo kwetu leo. Wao wenyewe walipaswa kumwona Kristo aliyefufuka ili kuweza kuihakikishia dunia kwamba alikuwa ni Yesu yuleyule ambaye waliishi naye kwa miaka mitatu (Matendo 1:21–22).

Lakini sisi hatuhitaji kumwona "mtu kutoka kwenye kituo cha umeme," yaani Kristo kujifunua mwenyewe kwetu. Tunaweza kugundua kuwa Kristo yu hai kweli bila kufanya hivyo. Bonyeza swichi ya toba na imani, na mwanga na uweza wa Roho wake utamulika ndani ya mioyo yetu.

Tuna ukingo mwingine dhidi ya hatari ya kuchukua ufufuo kama udhanifu kuliko tukio la kweli. Ufufuo wa Yesu haukuwa kufufuka kwa mtu yeyote tu. Maandiko ya Agano la Kale yalikuwa ni kitabu cha maelekezo ya Mungu kilichowaambia watu matendo waliyoweza kutegemea Mwokozi kuyafanya mara atakapokuja. Kwanza angekufa na kuwa dhabihu iliyopangwa na Mungu kwa ajili ya dhambi ya dunia. Kisha Mungu angethibitisha dhabihu hiyo kwa kumfufua kutoka kwa wafu (Isaya 53:4–6, 10–12). Yesu alieleza kwa dhati kwamba alikuwa Mwokozi huyo. Hiyo ndiyo sababu injili ya Kikristo haiishii na maelezo ya kwamba Kristo alikufa na kufufuka. Ni kwamba "*Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko. . . na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko*" (1 Wakorintho 15:3–4). Soma Maandiko hayo; na kisha thibitisha kwa matendo sahihi kwamba injili hii ni ya kweli.

# Sura 11

## Imani

### *Unamwamini Nani?*

Mpaka hapa katika mfululizo wa sura zinazohusu dhana ya imani tumekuwa tukizingatia misingi inayotutia moyo kuamini ukweli kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu. Biblia inatutahadharisha dhahiri kwamba kuamini ukweli huu yaweza kuwaletea waaminio mateso mengi. Hivyo, mtu ambaye anaamini anahitaji kujua wazi anaamini nini. Kama Yesu kweli ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Mwanzilishi wa ulimwengu, Muumba na Mmiliki wa mambo yote, basi hasara au mateso yoyote tunayopata kwa ajili yake si kitu ukilinganisha na kile tulicho nacho katika yeye. Kwa upande mwingine, kama Yesu si Mwana wa Mungu, tungekuwa wapumbavu kupata mateso au hasara yoyote kwa ajili yake.

Tena, kwa mfano, baadhi ya watu watasema, "Tunamwamini Kristo na dini nyingine zote pia." Lakini fikra za kuamini yote kwa mtindo huu ni wazo potovu lisilo na mantiki. Kama linenavyo Agano Jipya, imani katika Kristo inamaanisha kuamini kwamba *"Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe*

*kuwa ukombozi kwa ajili ya wote"* (1 Timotheo 2:5–6). Ina maana ya kuamini kwamba *"hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine. . . litupasalo sisi kuokolewa kwalo"* (Matendo 4:12). Inamaanisha kuamini kwamba dhabihu yake kwa ajili ya dhambi yatosha kabisa. Hakuna dhabihu nyingine inayoweza kutosheleza, wala hakuna nyingine tena inayohitajika (Waebrania 10:11–12). Madai ya kumwamini Kristo kama Mwokozi na kwa wakati huohuo kumwamini mwokozi mwingine yeyote siyo imani (wala si akili) bali ni kutoamini.

Imani ya Kikristo kweli haimaanishi kuamini ukweli fulani tu: bali inamaanisha kuamini, kutegemea na kujitoa kikamilifu kwa Mtu ambaye ni Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa bahati mbaya wapo watu wengi ambao wanasadiki ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na Mwokozi wa dunia, ambao hata hivyo hawajajitoa kikamilifu kwake ili awaokoe. Ajabu ni kwamba hilo ni jaribu ambalo linawavuta hasa watu wa dini (ingawa kwa kweli siyo wao peke yao).

Baadhi ya watu hawana haja ya kujitoa wenyewe kwa Kristo. Wana ujasiri kwamba jitihada zao za dhati kushika sheria ya Mungu ipasavyo na desturi yao ya kushiriki mara kwa mara sakramenti za kanisa zitawafikisha salama. Wanaonekana hawatambui onyo kali la Mungu kwamba wale wote wanaotegemea matendo ya sheria wako chini ya laana (Wagalatia 3:10–12).

Baadhi yao wanahofia kujitoa kwa Kristo tu kwa ajili ya wokovu. Wanahisi kwamba Kristo anatenda sehemu yake kutuokoa sisi, lakini tunatakiwa kuchangia ipasavyo ili kujiokoa. Wanaona hii ni kazi ngumu sana, na hata hivyo hawana uhakika kabisa kwamba itajitosheleza kuwaokoa mwishoni. Wanahitaji kusikia tena maneno ya Agano Jipya yanayoweka huru.

> *Basi, twaona ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria. . . Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki.* (Warumi 3:28; 4:5)

Mwokoaji wa kuogelea (*lifeguard*) anapomkaribia mtu ambaye yuko katika hatari ya kuzama majini ili kumwokoa, hatajaribu kumwokoa mtu huyo mara tu anapomfikia. Sababu ni kwamba mtu huyo akiwa katika hali ya kuchanganyikiwa ataendelea kuhangaika kujiokoa mwenyewe, atamkamata -na kumng'ang'ania mwokozi na hivyo kufanya zoezi la uokoaji lishindikane. Hivyo mwokozi ataogelea kwa kumzunguka kwa umbali kidogo kutoka alipo, hadi mtu huyo atakapochoka na kuacha kuhangaika kujiokoa mwenyewe. Kisha katika hatua hiyo mwokozi atamkaribia na kumwokoa. Mara nyingi inambidi Kristo kufanya hivyo pia. Anasubiri mpaka watu watakapogundua kwamba hakuna wawezacho kufanya ili kujiokoa wenyewe; na kisha anajitoa kwao kama Mwokozi ambaye anafanya wokovu wote.

Watu wengine wana tatizo la tofauti. Wakitambua kwamba wokovu unapatikana kwa imani, wanajitahidi kuamini kwa nguvu zote. Lakini pamoja na jitihada zao zote kuamini, wanajisikia kwamba imani yao haiko imara vya kutosha; na hivyo hawana uhakika wa wokovu. Kosa lao ni kwamba, ama kwa kujua au kutojua, wanaichukulia imani kama kazi inayostahili sifa, ambayo itakidhi kuleta wokovu iwapo tu imani ina nguvu ya kutosha. Lakini wokovu ni zawadi halisi. Imani haistahili kuupokea. Imani ni sawa na kitendo cha fukara asiye na kitu akinyosha mikono yake huku akitetemeka ili kupokea zawadi ambayo hajaifanyia kazi wala hastahili kuipokea (Waefeso 2:8–9).

Mtoto mdogo atafurahi kusinzia akiwa mikononi mwa mama yake, akiamini kuwa mama yake atamtunza salama. Imani ya mtoto kwa mama yake haina thamani kwa malezi ya mama yake wala haisababishi hayo, wala mtoto hahitaji kujibidiisha ili kufurahia usalama ambao upendo wa mama yake unatoa bure.

Kwa upande mwingine, imani siyo jambo la kujiamini mwenyewe tu. Kwa mfano, baadhi ya watu watasema: "Nina imani kubwa kwamba kama nitafanya vizuri kadiri ninavyoweza, mwishowe Mungu atanirehemu na kunitunukia wokovu." Lakini

imani ya aina hiyo siyo ambayo inamaanishwa kwenye Agano Jipya, kwani misingi ya kujiamini kwake haiko kwa Mungu wala yale anayonena Mungu, bali ni katika mtazamo wa msemaji mwenyewe. Kwa kweli, ujasiri huo umewekwa mahali penye hatari.

Fikiria mama akimnunulia dawa mtoto wake. Maelezo yanasema kwamba dawa ni lazima itumike kwa kupakwa nje ya ngozi tu: yaani kwamba ni sumu ikimezwa. Lakini mama hajali kusoma maelezo na akamnywesha mtoto wake kijiko kikubwa cha dawa. Akaamini kwamba dawa itamponya mtoto. Lakini je, itamponya? La hasha. Mtoto anaweza kufariki. Hivyo, imani inakuwa na maana pale tu misingi yake inapokuwa kwa Mungu, na kwa yale Mungu anayosema.

Na huu hapa ni utofauti mwingine muhimu: imani siyo hisia. Watu wengi (ijapokuwa si kila mmoja) wanapomwamini Kristo kwa mara ya kwanza na kupokea msamaha kamili wa dhambi na kuhakikishiwa wokovu, wanapata uponyaji mkubwa wa hisia zao, na wanasisimuka kwa furaha. Hiyo ni sawa kabisa. Lakini baada ya muda hisia hizi zinapungua. Katika hatua hiyo, kama imani yao inategemea hisia badala ya Kristo, wanaweza kufikiri kwamba huenda wamepoteza wokovu wao, ama huenda hawakuwa nao kabisa. Hivyo, hatupaswi kabisa kuchanganya imani na hisia. Imani katika Mungu kwa kweli inaweza kutusababishia hisia za huzuni na uchungu wakati mwingine, hasa kwa mfano neno la Mungu linapotutia hatiani kutokana na mienendo yetu miovu na uharibifu iliyousababisha. Au pale tunapogundua kwamba Mungu anatutaka kuacha matendo yasiyo na maadili ambayo tumefanya ili kujipatia pesa, au wakati tunapokabiliana na matusi au mateso kwa sababu ya kuwa waamini. Kwa hiyo ni lazima tulifanye neno la Mungu, na wala siyo hisia zetu, kuwa kiongozi wetu mkuu.

Ebu fikiria msichana anayeishi kwenye nyumba ya kupanga, ghorofa ya tano ya jengo. Nyumba yake ikawaka moto. Mara askari wa zimamoto anatokea nje dirishani kwake kwa ngazi ndefu.

Anaingia ndani na kumwambia inamlazimu kumruhusu ambebe ili amshusha chini kwa njia ya ngazi. Anaafiki na kujiaminisha kwake. Lakini pindi anapotazama chini na kuona ardhi ikiwa umbali mrefu, anajawa na hisia za hofu. Ila hisia zake haziathiri usalama wake. Askari wa zimamoto anamshika thabiti kwa mkono wake, na kumshusha kwa usalama zaidi. Hivyo, tunapoweka imani yetu kwa Kristo kama Mwokozi, ni nguvu na uaminifu wake ambazo zinatuhakikishia wokovu wetu. Hisia zetu hazihusiki na usalama wetu.

## Imani inahusisha pia kufanya Uamuzi wa Kimaadili

Mtu anaweza kusema: "Kama nikimwamini Kristo kunihakikishia uzima wa milele, nitajuaje kwamba nimeupata?" Hili hapa ni jibu la Agano Jipya kwa swali lake:

> *Tukiupokea ushuhuda wa wanadamu, ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi; kwa maana ushuhuda wa Mungu ndio huu, kwamba amemshuhudia Mwanawe. Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake. Asiyemwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuuamini huo ushuhuda ambao Mungu amemshuhudia Mwanawe. Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.* (1 Yohana 5:9–13)

Kifungu hiki cha Neno la Mungu mwenyewe kinatuambia kwamba anayemwamini Kristo anaweza kuwa na hakika kuwa anao uzima wa milele, kwa mambo mawili ya msingi.

**1. Kwa sababu Mungu ananena hivyo!** Na kutomwamini Mungu anapotuambia jambo inaashiria kwamba yeye ni mwongo.

Neno la Mungu ni wazi, rahisi, na linaeleweka:

> *Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe.* (1 Yohana 5:11)

Neno hili lazima liondoe shaka kwa kila mtu anayeamini.

Ebu fikiria nilipokutana na wewe kwa mara ya kwanza nikakuuliza jina lako ni nani, nawe ukajibu "Elizabeti." Na tazama kwa muda huohuo mtu mwingine akanijia na kuniuliza "Huyo mama anaitwa nani?" Nami nikajibu: "Sijui. Amesema anaitwa Elizabeti. Lakini siwezi kujua kwa uhakika." Ungejisikia vipi? Ungeweza kushitushwa na kukasirika sana, kwani kwa kukataa kuamini kile ulichoniambia, ningekuwa naashiria kwamba wewe ni mwongo. Ningekuwa natilia mashaka tabia yako. Hiyo ingeweza kuwa jambo zito; lakini uzito wake haukaribiani hata kidogo na suala la kukataa kuamini asemacho Mungu na hivyo kutilia mashaka tabia ya Mungu. Kwa hiyo, anayemwamini Mungu anahitaji kuwa na uamuzi kuhusu uadilifu wake Mungu: Je, anaaminika? Anasema ukweli?

Matatizo yote ya wanadamu yalianzia pale kwenye bustani ya Edeni, Shetani alipomdanganya mwanadamu kiujanja kwa maswali na kumshawishi aanze kudadisi na kutilia shaka neno la Mungu na hivyo utengano wake na Mungu ukaanza (Mwanzo 3:1–7). Utengano huo unaondolewa mara mwanadamu anapotubu na kuamini na hivyo anaweka tumaini lake lote kwenye neno na sifa ya Mungu asiyeweza kusema uongo.

2. Kwa sababu ***"yeye amwaminiye Mwana wa Mungu anao huo ushuhuda ndani yake"*** (1 Yohana 5:10). Ebu fikiria ulikuwa unaumwa, na daktari akakuandikia dawa za kutumia na kusema: "Chukua dawa hii, na itakuponya." Ingekubidi kwanza kuamua kumwamini au la. Je, alifuzu fani yake kihalali? Je, ungeweza kuwa na hakika kwamba kile alichokupa kilikuwa dawa nzuri wala siyo sumu? Lakini fikiria umeamua kwamba alikuwa ni daktari aliyefuzu vema na ni mtu wa kuaminika kutokana na sifa zake. Basi ungemeza dawa; na kama dawa itakuwa na matokeo mazuri na kukuponya, ungekuwa na ushahidi ndani

yako mwenyewe kwamba daktari yule alikuwa mkweli na dawa ilikuwa nzuri.

Mungu anatupatia uzima wa milele kama zawadi kwa jinsi iyohiyo. Tukimwamini, tutatambua kwamba tunayo zawadi hii, kwanza kwa sababu Mungu anatuambia hivyo, lakini pia kwa sababu ya mabadiliko halisi yanayotokea ndani yetu.

## Maisha ya Imani

Mapema kwenye sura hii tulijifunza kwamba, pindi tunapowaza kuhusu kuupokea wokovu, imani ni kinyume cha matendo: "kwa imani" inamaanisha "si kwa matendo." Sasa yatupasa kujifunza kwamba imani ya kweli inaelekea kuleta na kuzalisha matendo. Hakika, imani isiyozalisha matendo siyo imani halisi. Kama unafikiri wazo hili linajipinga, zingatia mfano ufuatao.

Mkulima ana moyo mdhaifu kiasi kwamba hawezi kufanya kazi tena. Daktari bingwa wa upasuaji wa moyo, ambaye ni rafiki yake, anajitolea kumfanyia upasuaji na kupandikiza moyo mwingine bila malipo. Upasuaji na moyo mpya kwa pamoja inabidi vipokelewe kama zawadi ya bure kwake. Mkulima anamwamini mpasuaji, anajitoa kwake, upasuaji unafanyika, na moyo mpya unapandikizwa kwa mafanikio. Matokeo yake, mkulima anajikuta akiwa na maisha yanayobubujika nguvu na ari mpya, na kwa furaha anafanya kazi, si kwa ajili ya kupata moyo mpya, bali kwa sababu tayari ameshapata.

Vivyo, hivyo Mungu anampa kila mmoja ambaye anamwamini Kristo zawadi ya kiroho ya moyo mpya. Ni zawadi ya bure kabisa, wala siyo malipo kwa ajili ya kazi. Lakini moyo mpya unaleta pia maisha mapya, nguvu, malengo, mikakati, na ari yanayofurahiwa kutumika katika huduma ya Kristo (taz. Ezekieli 11:19–20). Hakika hili ndilo lengo la wokovu, kama Paulo anavyowaambia wafuasi wake. Katika aya ambazo anawakumbusha kwamba wameokolewa kwa imani wala si kwa matendo, zinafuatwa na aya anapowaambia: *"Tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo*

*tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo"* (Waefeso 2:8–10, hasa 10).

Vivyo pia, kila hatua katika safari ya maisha itakuwa wito kuendela na zoezi la imani; na imani itaimarika zaidi kwa mazoezi kama ilivyo kwa misuli. Imani itamwezesha mwamini kuishi na kutenda kazi kwa kuzifuata amri za Kristo. Imani itampa nguvu kufuata mifano ya mashujaa wakubwa wa imani wa karne zote, waliofanya kazi kubwa, au waliovumilia mateso makuu kwa ajili ya Mungu (taz. Waebrania 11).

Aidha, Mungu ataruhusu imani kujaribiwa, wakati mwingine kwa mateso makali, ili kudhihirisha imani timilifu. Kwa hivyo inasafishwa kama dhahabu inavyoyeyushwa kwa moto ili kuondosha takataka, na kuifanya dhahabu yenye thamani zaidi (1 Petro 1:6–7). Lakini anayeamini anahakikishiwa kwamba Mungu hatamwacha ajaribiwe kupita awezavyo (1 Wakorintho 10:13). Hakika Kristo kwa kumwombea atatunza imani yake, na ikiwa itakapoanguka, ataiongeza, kama alivyomfanyia Petro siku nyingi zilizopita (Luka 22:31–32; Waebrania 7:25).

Imani pia itamwezesha anayeamini kushika mafundisho ya msingi ya Ukristo ambayo Agano Jipya linayaita "Imani." Kama alivyoandika Paulo, inatubidi *"kupiga vita vile vizuri vya imani"* (1 Timotheo 6:12–16). Na kwa hakika imani itavuna zawadi yake ya mwisho:

> *Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.* (2 Timotheo 4:7–8)

# 12 Sura

## Utakaso

### *Mtoto wa Simba ni Simba*

Katika sura hii tunajifunza neno **utakaso**. Neno hili linamaanisha hatua anazochukua Mungu kuwabadilisha watu wenye dhambi kuwa watakatifu. Kwa wasomaji wa Agano Jipya ambao bado hawajalifahamu neno hili, basi kwao ni neno lililojaa maajabu. Sehemu ambayo neno hili linastaajabisha zaidi ni kwenye matumizi yake ya neno 'mtakatifu'. Katika matumizi ya kawaida ya lugha, neno 'Mtakatifu' linatumika kama neno la heshima likihusishwa na mitume wa Kikristo, Mt. Petro, Mt. Paulo, n.k.; na pia linatumika kwa watu ambao wanadhaniwa kuwa wamefikia kiwango kikubwa cha utakatifu wakati wa uhai wao.

Lakini matumizi ya Agano Jipya ni tofauti sana na wazo hili. Kwenye maandiko ya asili (vichwa vya habari vya Injili na Nyaraka sivyo vya asili: viliongezwa baadaye), haikutokea, hata mara moja, mitume kutambuliwa kama Mt. Petro, au Mt. Paulo, n.k. Ingawa mitume na manabii kwa ujumla mara kadhaa wanatambulishwa kama *"mitume watakatifu na manabii"* (Waefeso 3:5; 2 Petro 3:2). Kwa upande mwingine, Wakristo **wote** kwa ujumla wanaitwa watakatifu. Kwa mfano, inaposemwa kwenye Matendo 9:32 kwamba Petro alikwenda kuwatembelea *"watakatifu waliokaa*

*Lida"* haimaanishi kwamba alikwenda kuwatembelea wateule wachache tu kati ya Wakristo: neno *'watakatifu'* hapa ni namna ya kawaida ya Agano Jipya kutumia neno hili kumaanisha Wakristo wote katika eneo fulani.

Cha kustaajabisha zaidi, waraka wa Paulo kwa kanisa la Korintho unaonesha kwamba mienendo ya waamini wengi haikustahili sifa. Hata hivyo, bado kwenye maneno yake ya utangulizi anawaita watu wote kama *"wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu"* (1 Wakorintho 1:2).

Aidha, lugha hiyo siyo ya kujifanya, wala kumsifu mtu kwa kumbembeleza, kama mithali isemavyo: 'kumpaka mtu mafuta kwa mgongo wa chupa'. Wazo la utakaso linabubujika toka kwenye kiini cha injili. Baadhi ya waamini wa Korintho awali waliishi katika uasherati wa kupindukia; wote walikuwa watenda dhambi; wengi wao walikuwa bado wanyonge na wachangakiroho. "*Lakini,*" kama asemavyo Paulo, "*mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu*" (1 Wakorintho 6:11). Kwa kusema hivi, Agano Jipya halimaanishi kwamba watu ambao wametakaswa na kuwa watakatifu hawahitaji tena kupiga hatua katika utakatifu wao wa kila siku. Lakini inaeleza kwamba hiyo ndiyo faida ya dhabihu ya Kristo kwamba wote wanaoweka imani zao kwake papo hapo wanatangazwa na Mungu kuwa wametakaswa kweli na kwa haki wanaitwa watakatifu.

Ili kuona jinsi hili linavyowezekana, ebu tueleze maana ya 'utakatifu'. Utakaso unaonekana kwa pande mbili:

1. Kwa upande wa kwanza, inahusisha kutengwa kutoka kwenye uchafu na unajisi, au kwa maneno mengine kusafishwa. Utakatifu una maanisha kwamba tunaamua kukwepa matendo kadhaa.

2. Kwa upande wa pili, utakatifu unamaanisha kutengwa ili mtu awepo kwa Mungu na kwa huduma yake, au kwa maneno mengine, kuwekwa wakfu. Utakaso unatutaka tuamue kutenda matendo mengine.

Maana zote mbili zinaelezwa kwa ufasaha zaidi katika Waebrania 9:13–14. Hapa mwandishi anatofautisha kati ya njia za utakaso za Kiyahudi za zamani na zile za Kikristo. Anahusisha utakaso kwanza na kusafishwa kutoka unajisi na pili na kuwekwa wakfu kwa huduma ya Mungu.

> *Kwa maana, ikiwa damu ya mbuzi na mafahali na majivu ya ndama ya ng'ombe waliyonyunyiziwa wenye uchafu hutakasa hata kuusafisha mwili; basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na dosari, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?* (Waebrania 9:13–14)

Kinachofuata inatubidi kutambua kwamba Agano Jipya hunena juu ya 'utakaso' upatikanao kwa kufuata hatua tatu: hatua ya awali, endelevu na hitimisho. Kwanza tutaangalia hatua ya utakaso wa awali unavyofanyika. Kisha tutaangalia hatua ya pili na ya tatu katika sura inayofuata.

## Utakaso wa Awali

Kwanza, tutambue jinsi utakaso wa awali unavyopatikana:

**1. Kwa kutolewa kwa mwili wa Kristo**:

> *Kwa hiyo (Kristo) alipokuja ulimwenguni, alisema, Dhabihu na matoleo hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari. . . Ndipo niliposema, Tazama, nimekuja. . . niyafanye mapenzi yako, Mungu. . . Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.* (Waebrania 10:5, 7, 10)

Basi, hatujifanyii utakatifu kwa juhudi zetu wenyewe ama kwa kushika sheria ya Mungu au kufanya yaliyo mapenzi yake. Juhudi zetu zote kwa lengo hilo zisingetosha kabisa kwa chochote Mungu anachokitaka yaani usafi, utakatifu na kujitoa kwake. Habari

njema kwetu ni kwamba tunafanywa watakatifu na kukubalika kwa Mungu kutokana na kile ambacho Mtu mwingine – yaani Kristo – amefanya. Yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kwamba atoe mwili wake kama dhabihu isiyo na dhambi badala yetu; na alifanya hivyo mara moja tu alipojitoa nafsi yake kwa Mungu pale msalabani. Ni dhabihu hiyo, na wala si juhudi zetu, inayotufanya kukubalika kwa Mungu, ingawa twakosa kwa mambo mengi.

2. Damu ya Kristo: (taz. Waebrania 9:13–14 hapo juu). Hakuna awezaye kukubalika kumtumikia Mungu aliye hai ikiwa dhamiri yake imenajisiwa kwa hatia. Hatia inafunika kama kivuli na inatoa harufu ya kuoza na ya mauti kwa mtu na yote yale anayoyafanya. Hatuwezi kusambaratisha unajisi huo kwa kuongezeka jitahada zetu za kidini. Hata ibada za kidini na kutawadha haziwezi (taz. Mathayo 15). Lakini sisi tusichoweza kufanya, damu ya Kristo inaweza: kwani *"damu yake Yesu* [Kristo], *Mwana wake* [Mungu], *yatusafisha dhambi yote"* (1 Yohana 1:7). Inasafisha dhamiri zetu na kutuweka huru kumtumikia Mungu aliye hai.

Basi damu ya Kristo inatekeleza upande wa kwanza wa utakaso, yaani usafishaji kutoka kwenye unajisi. Ni nini basi hutekelezwa upande wa pili wa utakaso, ambao ni, kuwekwa wakfu kwa ajili ya Mungu?

Kwa upande wa Mungu, hatua hii inatekelezwa na kazi ya Roho Mtakatifu mioyoni mwetu, akituhakikishia kwamba tuna dhambi, na kutuleta kwa Mwokozi, na kutufunulia njia ya wokovu ya Mungu, na kupandikiza wokovu ndani yetu. Pia analeta uweza wake wa kutufanya tuzaliwa mara ya pili, yaani uzima utokao kwa Mungu wenye nguvu ya kukuza maisha ya kiroho.

> *Mungu. . . alituokoa. . . kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu.* (Tito 3:4–5)

> *Kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mkapata kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo.* (1 Petro 1:2)

Kwetu sisi pande zote mbili za utakaso zinatekelezwa katika mioyo yetu kwa imani:

> *Na Mungu, ajuaye mioyo ya watu, akawashuhudia, akiwapa Roho Mtakatifu vilevile kama alivyotupa sisi; wala hakufanya tofauti kati yetu sisi* [Wayahudi] *na wao* [Mataifa]*, akiwasafisha mioyo yao kwa imani.* (Matendo 15:8–9)

Utakaso huu hutokea pale tunaporuhusu kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu na kuacha kujiamini wenyewe katika kujipatia wokovu. Hapo tunaweka imani yetu yote kwa Mungu na kwa dhabihu ya Kristo, hali hii inaleta mabadiliko makubwa ndani ya mioyo yetu. Utengano na uadui wetu wa zamani dhidi ya Mungu unatoweka. Kujitegemea kwetu na kutomzingatia Mungu kunatoweka. Badala yake, Roho Mtakatifu anatufanya kulitambua pendo la Mungu kwetu: "*kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi*" (Warumi 5:5). Anatufunulia kwamba sasa tumekuwa watoto wa Mungu, tukishiriki uzima na tabia ya Baba yetu ili kwamba, kwa hiari yetu na kwa asili yetu tumwite Aba, yaani Baba (Warumi 8:14–17). Hivyo tunaonja wajibu na uwezekano wa kuwa watakatifu kama Baba yetu alivyo mtakatifu (1 Petro 1:14–16).

Sambamba na hilo tunagundua kwamba *"kwa yeye* [Kristo] *sisi sote* [kwa maana ya Wayahudi na wasio Wayahudi kwa pamoja] *tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja"* (Waefeso 2:18). Kwa kweli hii haikuwa hivyo daima. Katika karne zilizotangulia kuzaliwa kwa Kristo, kuishi na kufa kwake, enzi hizo dhabihu ambazo Waisraeli walitoa kwa ajili ya dhambi zao zilikuwa ni ishara tu. Hazikuweza kuziondoa dhambi zao, kwani hakika hazikulipa deni la dhambi hizo. Na matokeo yake, Mwisraeli wa kawaida aliruhusiwa kuingia kwenye ua wa nje tu wa hekalu. Makuhani waliingia Mahali Patakatifu lakini si ndani zaidi ya hapo. Ni Kuhani Mkuu pekee aliyeruhusiwa kuingia Patakatifu pa Patakatifu ambapo Kiti cha Enzi cha Mungu kiliwekwa.

Lakini sasa baada ya Kristo kuja na kujitoa kuwa dhabihu timilifu kwa ajili ya dhambi, yote hayo yamebadilika. Kristo amewakamilisha hata milele wale wote waliotakaswa (Waebrania 10:14). Kwa hiyo, wote wanaoamini, wala si wachache tu walioteuliwa rasmi – hata sasa, hapa duniani – wana haki ya kuingia kiroho Patakatifu pa Patakatifu pa uwepo wa Mungu mbinguni, na hivyo kuwa na ujasiri wa kuingia na kusogea karibu na Mungu. Katika Waebrania 10:19–22 yanaelezwa jinsi hayo yanavyoweza kutokea: Yesu amewafungulia njia kwa damu yake, na kila aaminiye, moyo wake umenyunyizwa kwa damu hiyo ili kuusafisha kutokana na dhamiri ya hatia, na mwili wake, kwa lugha ya kimfano, ni sawa na kuoshwa kwa maji safi (linganisha na Yohana 13:6–11).

Wakibaki na furaha ya kuukaribia uwepo wa Mungu, wanaoamini hatimaye wanagundua kwamba wote wamefanyika makuhani kwa Mungu na kuwekwa wakfu kwa huduma ya Mungu kwa damu ya Kristo (Ufunuo 1:5–6; 5:9–10). Hivyo ndivyo Mtume Petro anavyowaambia waamini wenzake wote:

> *Ninyi nanyi. . . mmejengwa muwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo. . . Ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema bali sasa mmepata rehema.* (1 Petro 2:5, 9–10)

Yote haya yanawasababisha waamini kujenga upendo wa ndani zaidi kwa Mungu. Kama asemavyo Mtume Yohana, *"sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza"* (1 Yohana 4:19). Hii inakuwa changamoto kwa waamini kutoa kwa furaha maisha yao nyumbani, shuleni, kiwandani na ofisini, au shambani, kwa kazi ya Mungu. Mtume Paulo anasema, *"Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu*

*iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu"* (Warumi 12:1–2).

Wito huu una misingi katika mantiki isiyokwepeka. Aya kadhaa kwenye Agano Jipya zinaeleza hili wazi. Huu hapa mfano mmoja:

> *Maana, upendo wa Kristo watuongoza; maana tumehukumu hivi, ya kwamba mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote; tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao.* (2 Wakorintho 5:14–15)

Aya nyingine inaongeza sababu nyingine ya kuishi maisha matakatifu:

> *Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.* (1 Wakorintho 6:19–20)

Hapa tunatambua mantiki ileile ya mwanzo: aaminiye amekombolewa kwa gharama ya damu ya Kristo. Kuanzia sasa na kuendelea, mwamini mwenyewe wala mwili wake si mali yake tena. Vyote ni mali ya Kristo. Lakini zaidi: kwa njia ya ukombozi wa Kristo mwili wa mwamini umefanywa kuwa hekalu la Roho Mtakatifu, kwani alipoamini, Mungu aliweka Roho Mtakatifu ndani yake. Kwa hiyo kuwepo huko kwa Roho Mtakatifu kwenye mwili wa mwamini kunaufanya kuwa mtakatifu na kunauweka wakfu kuwa makao ya Mungu. Ni ukweli huu wa ajabu unaomfunga mwamini na jukumu la kumtukuza Mungu katika mwili wake, na kuepuka kuchafua kile ambacho sasa kimekuwa hekalu la Roho Mtakatifu.

Mtiririko wa matukio hapa kwa pamoja yanaonekana wazi na yanajieleza. Anayeamini haambiwi kwamba kama akisafisha ipasavyo maisha yake kwanza, huenda Roho Mtakatifu atakubali kuja na kuufanya mwili wake kuwa hekalu lake. Ni kinyume cha hilo. Kristo, kwa dhabihu na damu yake, tayari amesafisha na kutakasa mwili wa mwamini na ameufanya kuwa hekalu la Roho Mtakatifu. Kwa kuwa tayari huo ndiyo ukweli, mwamini sasa anawajibika, na anakuwa na moyo wa kujiepusha na mwenendo unaoweza kunajisi mwili wake.

Ngoja tujumlishe yale tuliyojifunza hadi hapa. Utakaso wa awali, kama tulivyouita, si kitu tunachohitaji kufikia au kutekeleza kwa juhudi zetu wenyewe ili tuweze kuishi maisha matakatifu. Ni kitu ambacho Mungu ameweka ndani yetu kuanzia pale tulipoanza kuweka imani yetu kwa Kristo:

> *Bali kwa yeye* [Mungu] *ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi.* (1 Wakorintho 1:30)

Utakaso huu wa awali unamfanya kila mwamini kuwa mtakatifu. Unampa kila mwamini njia ya papo hapo na moja kwa moja kufika kwa Baba. Unamweka wakfu kila mwamini kuwa kuhani wa Mungu, anayetoa kwa Mungu dhabihu za kiroho na kuwaambia wengine upendo na neema ya ukombozi wa Mungu. Utakaso unaufanya mwili wa kila mwamini kuwa hekalu takatifu ambamo Roho wa Mungu hufanya makazi. Unatengeneza ufahamu kwa kila mwamini kwamba sasa yeye ni mtoto wa Mungu, na uhai wa Baba yake mwenyewe uko ndani yake, na pia akiwa na kila kitu kinachohitajika ili awe mtakatifu kama Baba alivyo mtakatifu. Aidha, unamjengea mwamini upendo na moyo wa shukrani kwa Mungu na kwa Kristo ambavyo humpa hamasa ya kuishi maisha ya kujitoa kwa Mungu, Baba, Mwana na Roho. Na sio tu pendo kwa Mungu na Kristo, bali pia pendo kwa wale wote, wa rangi au taifa liwalo lote, ambao pia wamezaliwa na Baba yuleyule (1 Yohana 5:1).

Mara moja hapa mtu anaweza kupinga kwa kusema: "Hii inaufanya utakaso uonekane rahisi sana. Kwa nini basi Biblia yenyewe inaonesha maisha ya Kikristo kama maisha ya kupambana, kuhangaika na vita?" Ndiyo, ni kweli Biblia inaonesha hivyo, na tutachunguza hilo katika sura yetu inayofuata.

# 13
# Sura

## Utakaso

### *Uwana Wala Si Utumwa*

Katika sura yetu iliyopita tulisoma kuhusu utakaso wa awali; sasa tunahitaji kuchunguza Agano Jipya linamaanisha nini kwanza kuhusu utakaso endelevu na kisha utakaso hitimisho.

### Utakaso Endelevu

Jambo la kwanza kutambua hapa ni ukweli ulio wazi: Biblia inasisitiza kwamba watu wakiwa wanatakaswa na kufanywa watakatifu halisi punde wanapoweka imani yao kwa Kristo (kama tulivyoona kwenye sura yetu iliyopita), baada ya hapo bado wanahitaji kuendelea kujitakasa nafsi zao kutoka kwa uchafu wote wa mwili na roho, huku wakitimiza utakatifu katika kumcha Mungu (2 Wakorintho 7:1). Tukitambua hili tunaepukana na kosa la wengi. Hakika Biblia inafundisha kwamba mtu anahesabiwa haki kwa imani, kwa neema bure ya Mungu wala sio kwa misingi ya matendo yake au ya hali yake ya kiroho ama kabla au baada ya kuokolewa (Warumi 3:19–28). Lakini hiyo haimaanishi kwamba, kama wengi walivyodhania kimakosa, mtu anapohesabiwa haki kwa neema yuko huru kuishi maisha ya dhambi. Sikiliza Paulo

anavyopinga hili mara mbili mfululizo:

> *Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha!. . . Ni nini basi? Tufanye dhambi kwa sababu hatuwi chini ya sheria bali chini ya neema? La hasha!* (Warumi 6:1–2, 15)

Aidha, Paulo anaweka wazi kwamba Kristo anapoamua kutuokoa, si kwamba anasamehe dhambi zetu tu, bali pia anakazana kutufanya watakatifu zaidi na zaidi. Badiliko la kweli, kama anavyowakumbusha wafuasi wake (Waefeso 4:17–24), lilihusisha kukubaliana na Kristo toka mwanzo *"kuuvua utu wa kale,"* ambao ni mfumo wa maisha ya dhambi yaliyotangulia, na *"kuuvaa utu mpya,"* ambao ni mfumo wa maisha ambao Mungu mwenyewe ameukusudia kwa ajili ya wale waliopatanishwa naye. Hii inamaanisha kuwa "kuvua" na "kuvaa" kunaendelea kwa siku zote za maisha ya mtu. Kwa maneno mengine, utakaso endelevu sio hiari kwa mtu ambaye ametakaswa kwa imani kwa neema ya Mungu tu wala si kwa matendo yake. Kwa mujibu wa Agano Jipya, utakaso ni lazima. Hakika anayekataa jukumu hili sio mwamini wa kweli.

Sasa tuangalie ni kwa namna gani utakaso huu endelevu unavyopatikana.

Kimsingi kuna njia mbili za kuupata. Njia zote zinahitaji matendo thabiti na uvumilivu kwa upande wetu. Lakini njia moja si sahihi, na njia nyingine ndiyo sahihi. Njia moja ni njia ya mtumwa; hii haifanyi kazi na inasababisha kuvunjika moyo na kukata tamaa (taz. Warumi 7:7–25). Njia nyingine ni ile ya kufanyika watoto wa Mungu waliowekwa huru. Njia hii inawaongoza kwenye ushirikiano kamili na Baba yao na katika kufanana zaidi na zaidi na namna ya fikra na mwenendo wake (taz. Mathayo 5:43–48). Imefupishwa vizuri kwenye Warumi 8:13–17:

> *Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali kama mkiyaua matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi. Kwa*

> *kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*

Tatizo la njia isiyo sahihi ni hili: inatambua kwamba sheria ya Mungu ni takatifu, ya haki, na njema; kwamba amri zake zinaleta maana; na kwamba faida zote zinazotokana na kushika sheria zinapendeza (Warumi 7:12). Lakini kutoka hapo inahitimisha haraka kwamba njia ya Agano Jipya kuhusu utakaso endelevu ni hivi: "Hii hapa sheria ya Mungu; hizi hapa ni amri zake kumi; haya hapa mafundisho ya Kristo kwa watu wote; hii hapa hotuba ya Kristo mlimani; fanya uamuzi, imarisha nia yako, fanya juhudi kuyatunza, na utakuwa mtakatifu zaidi na zaidi."

Hata hivyo, mtazamo huu hautilii maanani mambo muhimu matatu:

1. Wanadamu wameharibiwa, wamedhoofishwa, na kupotoshwa sana na dhambi, kiasi kwamba hawawezi kuitii sheria ya Mungu hata wanapojaribu sana. Wanaweza kuifurahia sheria ya Mungu, kuitumikia kitaalamu, na kujitahidi kwa nguvu zao zote kuitunza, kama Mtume Paulo anavyokiri kuwa alifanya hivyo awali (Warumi 7:15, 18–19, 22, 25). Lakini sawa na Paulo watajikuta mara zote kuwa wameshindwa kuitekeleza kikamilifu kivitendo. Hakika, watagundua kwamba ndani yao kuna upinzani wenye nguvu unaopiga vita dhidi ya utiifu kwa sheria ya Mungu; upinzani uliojiimarisha kwa nguvu za kijeshi kuendeleza utawala wa dhambi (Warumi 7:23).

2. Katika hali hii, sheria ya Mungu, pamoja na uzuri iliyo nao, haiwezi kumsaidia mtu. Kama inavyoelezwa kwenye Biblia, haina uwezo wa kuleta mafanikio, kwa sababu ya udhaifu wa mambo ya mwili (Warumi 8:3). Hakika, mtu anapowaza tu juu ya matendo

yake ya dhambi mara nyingi anayaongeza (Warumi 7:7–8); na anaposisitiza makosa yake ya mara kwa mara, anadhoofisha nguvu zake za kuyakabili (Warumi 7:21–24).

3. Na kisha kuna jambo la tatu, ambalo huwa tunalisahau kwa urahisi. Sheria ya Mungu inaelekeza jinsi tunavyohitaji kuenenda, lakini inaenda zaidi ya hapo. Ni amri **pamoja na adhabu kwa ajili ya kushindwa** au kutotii; na adhabu yake ya mwisho ni kukataliwa na Mungu. Mtu akianguka mara moja tu hana nafasi tena hata kama akifanya mema kwa kiwango kikubwa namna gani hakitaweza kufidia kushindwa kwake au kufuta adhabu. Mfumo unaodai ukamilifu mara zote hauna nafasi kuongeza matendo mema ili kufidia hali ya kutokukamilika.

Ili kusaidia kuelewa matokeo ya jambo hili yana maanisha nini, ebu tuunde mfano. Fikiria hospitali ya magonjwa ya kifua kikuu inapatikana kwenye bonde lililojitenga. Kwenye ukingo wa mbali wa bonde hilo kuna kituo cha umeme za kinyuklia na kimeanza kuvujisha miali ya mnururisho usioonekana lakini unaoweza kusababisha vifo. Kwa hiyo serikali ikashauri wagonjwa wakimbie kwa ajili ya kuokoa maisha yao. Kwa bahati mbaya njia pekee ya kutokea bondeni inapitia milima minne yenye urefu unaofikia mita 4,000; na serikali ikawaarifu wagonjwa kwamba kama wasipovuka safu yote ya milima hawatakuwa salama na hatari ya mnururisho.

Kwa kweli ushauri wa serikali una maana; mtu yeyote mwenye ufahamu mzuri angetaka kuufuata. Lakini inatokea hivi kwamba serikali haiwezi, au haitoi msaada wa aina yoyote kwa wagonjwa ili kuvuka safu ya milima: hakuna helikopta, hakuna mabasi, hakuna farasi wala punda. Wagonjwa wanapaswa kufanya jitihada zao tu kutembea. Wakisukumwa na hofu ya mnururisho uletao kifo wangeweza kujitahidi kutoroka kwa nguvu ya kishujaa. Ila ugonjwa wao utapunguza kasi ya kutembea kwao hadi ikawa dhahiri kwamba wamebaki bila tumaini lolote la kuvuka milima kabla ya kufa kwao ama kwa ugonjwa wao, au hali ya hewa, au madhara ya mnururisho.

Lakini ebu fikiria zaidi serikali itawaambia kwamba ni lazima waivuke milima yote minne ndani ya siku tatu. Yeyote ambaye angechukua muda mrefu zaidi ya siku tatu mwilini mwake angebeba kiwango kikubwa cha mnururisho wa nyuklia kiasi cha kuhatarisha watu wengine. Kwa hiyo angepigwa risasi punde tu anapojitokeza. Wagonjwa katika hali ya udhaifu wao wangegundua kwamba ingewachukua zaidi ya muda wa siku tatu zilizoruhusiwa kuvuka milima miwili ya kwanza. Basi kusingekuwa na maana kwao kuhangaika kuvuka milima miwili mingine, kama mwishowe, pamoja na jitihada zao zote, wasingekuwa na budi kukabiliana na adhabu ya kifo.

Kila sehemu ya utu wetu inapinga kwamba Mungu hawezi kuwa wa namna hii; na kwa kweli hayuko hivyo! Njia yake ya kupata utakatifu endelevu sio kwa kuwapa watu sheria yake tu na kuwaamuru kujitahidi kwa nguvu zao zote kuifuata. Kama ingekuwa hivyo, hatima yao isingekuwa bora zaidi ya ile ya wagonjwa wale kwenye mfano wetu. Upendo wa Mungu na hata ufahamu wake wa yale yawezekanayo vimemsukuma kutoa njia tofauti kabisa.

Hatua yake ya kwanza ili kuvunja shinikizo kubwa la dhambi juu ya maisha ya watu ilikuwa ni kuondoa daima adhabu yao ya kushindwa kuifuata sheria yake kikamilifu. *"Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema"* (Warumi 6:14). Kristo kwa kifo chake alilipa deni hilo kwa ajili yao daima (Warumi 6:6–11). Basi, hivyo wako huru. Kama wangekuwa bado 'chini ya sheria' na kukabiliwa na adhabu yake, kosa moja, anguko moja au dhambi moja tu ingetosha kupata adhabu. Kwa namna hiyo jitihada zote za kuendelea ili kujitakasa zisingekuwa na maana. Kwa namna hiyo dhambi ingekuwa imeshinda kufunga njia za watu za kukwepa utawala wake.

Bali sasa njia ya kuendelea zaidi kujitakasa kweli ina maana. Ingawa pamoja na jitihada zao wanatenda dhambi na kuanguka, wanaweza kutubu dhambi zao kwa Mungu, na Yeye ni mwaminifu na wa haki hata awaondolee dhambi zao, na kuwasafisha na

udhalimu wote (1 Yohana 1:9). Na kwa kuwa hawana deni la kulipa sasa wala baadaye, wako huru kuinuka tena na kukazana katika njia ya utakatifu endelevu.

Hatua ya pili ambayo Mungu amechukua kuvunja utawala wa dhambi ni kutoa msaada na uweza ambazo sheria isingeweza kutoa. *"Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati* [sheria]*, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu* [ambaye ni Kristo]*, kusudi tumzalie Mungu matunda"* (Warumi 7:4). Tunarejea, si kwamba sheria ya Mungu ni mbaya, au kwamba maagizo yake yanaweza kupuuzwa. Lengo la Mungu ni kwamba tutimize maagizo ya sheria yake (Warumi 8:4). Lakini sheria yenyewe haiwezi kutupatia uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, jibu la Agano Jipya kwa tatizo hili ndilo ambalo tunaweza kuita, kwa lugha ya kimfano, "ndoa na Kristo," au kama aya yetu inavyosema *"mpate kuwa mali ya mwingine"* (taz. pia 1 Wakorintho 6:16–17).

Mwanamke anaweza kujisomea vitabu vingi kuhusu maumbile yake na kusubiri kwa muda mrefu kupata mtoto; lakini asingekuwa na tumaini lolote la kupata mtoto asipokuwa na mume. Hivyo Kristo, akiwa amefufuka kutoka kwa wafu, akawa mume aliye hai, mwenye upendo, na wa kiroho kwa wale wanaomwamini yeye, anawagawia uhai na uweza ulio muhimu, kusudi "wamzalie Mungu matunda" kwa njia ya utakatifu endelevu.

Ni dhahiri kwamba Agano Jipya halichukulii uhusiano huu kana kwamba utu wa mwamini unakandamizwa, kama vile pia mwanamke aliyeolewa asivyofananishwa na mashine tu. Mwamini anaendelea kubaki kuwa mtu anayewajibika. Ni yeye anayehitaji kuwa makini kupiga hatua kwenye utakatifu (2 Petro 1:1–11), ni yeye ambaye anahitaji kuishi kwa kumpendeza na kumtumikia Mungu. Lakini si suala la kusoma tu maelekezo yaliyoandikwa kwenye kitabu, au maneno kwenye vipande vya mawe kama zilivyokuwa Amri Kumi, na kisha kujitahidi kuzifuata. Hiyo ingekuwa sawa na kinachoitwa katika aya ifuatayo kama "*kutumika katika hali ya zamani ya andiko*":

> *Bali sasa tumefunguliwa katika torati. . . ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko.* (Warumi 7:6)

Roho Mtakatifu wa Mungu, aliyeandika sheria za Mungu kwenye Biblia hivyo kuwa dhihirisho la sifa takatifu ya Mungu, sasa akiwa ndani ya mwamini anamwezesha mwamini aishi kulingana na sheria hizo, akifanya kazi kupitia kwa mwamini. Anatenda kazi ndani ya mwamini kuyafanya upya mawazo yake, kubadilisha mitazamo yake, kuandaa upya jinsi anavyothamini maadili yake, kutia nguvu mapenzi yake, kuonesha njia mpya kwa nia yake, kupinga tamaa zake mbaya. Tunaambiwa kwamba Roho inaleta nguvu kubwa *"kushindana na mwili. . . hata hamwezi kufanya mnayotaka"* (Wagalatia 5:16–24, hasa 17).

Hata hivyo uhusiano huu kati ya mwamini na Kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu si suala la mawazo yasiyo wazi, wala maono ya hewani, yasiyoeleweka wala kuelezeka. Kristo ataelekeza mawazo ya watu wake daima kwa Neno la Mungu. Agano Jipya linasema kwamba alipowaombea wanafunzi wake kwa Baba yake waendelee kutakaswa, akasema: *"Uwatakase kwa ile kweli, neno lako ndiyo kweli"* (Yohana 17:17). Kwa kweli, mwamini bado anaweza kuchagua kati ya *"kupanda kwa mwili"*, au *"kupanda kwa Roho"* (linganisha Wagalatia 6:8). Lakini katika chaguo lake halazimishwi tena kama mtumwa aliye chini ya kiboko, yaani hofu ya adhabu ya sheria ya Mungu, lakini anaongozwa na Roho ambaye anamwezesha kufahamu kwamba yeye ni mtoto wa Baba, akiwa na upendo, uzima na tabia ya Baba ndani yake (Warumi 8:14–17). Na kama ilivyo kwa msukumo unaotokana na diragiro (dira maalum ya kuongoza ndege) inavyosaidia ndege kufuata njia yake, ndivyo ilivyo katika maombezi ya Roho Mtakatifu. Pamoja na shauku ya mwamini mwenyewe, Roho anamwendeleza katika njia iliyowekwa na Mungu kwa ajili yake, njia inayopitia katika kuitwa na kuhesabiwa haki kwake hadi kwenye lengo la mwisho la kutukuzwa kwake (Warumi 8:26–30).

Biblia haitoi ahadi ya uongo kwamba maendeleo katika njia hiyo ni tambarare na hayana shida. Mtoto wa Mungu anapoacha njia hii, kama itakavyokuwa kwa watoto, au akihitaji kusukumwa kuendelea kwenye njia, Mungu kama Baba yake hatasita kumrudi. Nidhamu hii inaweza kuwa inaumiza, lakini inatolewa kwa upendo na hekima za Baba ili kwamba mwamini aweze kushiriki vema zaidi utakatifu wa Baba (Waebrania 12:1–13). Mwisho wa njia hii ni hakika na salama. Kuanzia mwanzo wa njia, mwamini anahakikishiwa kwamba, kwa kuhesabiwa haki kwa imani, ataupata utukufu wa Mungu (Warumi 5:1–2).

## Utakaso Hitimisho

Mara kwa mara, baadhi ya watu wamejenga fikra kwamba Wakristo wanaweza kuwa wakamilifu wasiotenda dhambi katika maisha ya hapa duniani. Biblia inakataa hilo. Kwa kadiri tunavyoishi katika dunia hii inatubidi kukubaliana na Paulo:

> *Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.* (Wafilipi 3:12)

Utakaso wa mwamini utakamilishwa wakati wa kuja kwa Kristo kwa mara ya pili. Kisha mwamini atafananishwa kimwili, kimaadili na kiroho na Kristo. Na Biblia inatuambia ni kwa vipi itafanyika:

> *Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini tunajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo.* (1 Yohana 3:2)

# 14 Sura

## Hukumu ya Mwisho

### *Kutaka Haki Itendeke*

Ni ukweli unaovutia sana kwamba watoto, hata katika umri mdogo, wanajenga hisia kali juu ya nini kilicho cha haki na sawa, na nini si sawa. "Mnanionea," mtoto anasikika akisema pale mdogo wake anapochukua mdoli wake halafu wazazi wake wakamruhusu mdogo kukaa nao na kuuchezea. "Si halali," mwanafunzi anasema mwalimu anapomshutumu na kumwadhibu kwa jambo ambalo, kwa kweli, hakulifanya.

### Ufahamu wetu wa asili kuhusu Haki

Pengine kwa kadiri tunavyokua na kuwa watu wazima ndivyo tunavyopunguza ukali tunapoona haki haitendeki, kwa sababu tumeshuhudia matukio mengi ya kutokutenda haki, kiasi kwamba tumekuwa na mioyo migumu na tunaamini kwamba watu ni wachoyo siku zote. Hata hivyo, bado tunashitushwa, kwa mfano, tunapomwona mtu anatajirika mno kwa kuuza mali za umma na kutia mapato mfukoni mwake. Pengine tunakata tamaa na ukweli ni kwamba tunashindwa kufanya chochote kuhusu hilo; lakini bado tunadai: "Si haki." Lawama yetu inabeba ndani mwake, kwa

kusema au kutokusema, madai kwamba mtu fulani anawajibika kuchukua hatua fulani kuhusu hili: asiruhusu kukosekana kwa usawa kuendelea; asiwaache wadanganyifu, waongo, wauaji, na wote wengine watendao uovu kukwepa bila kuadhibiwa.

Hata hivyo historia, na uzoefu wa maisha yetu, zinatuonesha kwamba hayo ndiyo yanayotokea mbele ya macho yetu. Hata serikali zile ambazo kimsingi wajibu wa watumishi wake ni kuwaadhibu wakosaji, mara nyingi wao wenyewe wamejikuta na hatia ya rushwa na wakati mwingine ufisadi wa kupinduka. Mwishoni kifo kinaonekana kuwaondoa wote bila kubagua, wanaofuata na wanaovunja sheria, vilevile watakatifu na watenda dhambi. Je, hivyo tuhitimishe tu kwamba makosa ya jinai na dhambi, na kutokutenda haki kwa hali ndogo na kubwa, hazitaadhibiwa? Je, tuchukue kwamba hisia zetu juu ya yaliyo haki na yasiyo haki ni ndoto za abunuwasi, kwamba tumaini letu la kuona haki litavunjika daima?

La hasha! Biblia inasema, Mungu mwenyewe ni mwasisi wa ufahamu wetu wa yaliyo haki na yasiyo haki. Muumba ameandika sheria yake mioyoni mwetu (Warumi 2:14–15); na dhamiri yetu ni msimamizi wake wa ndani anayetuonya tusivunje sheria hiyo, na akitushuhudia pale tunapoivunja kuwa tunafanya vibaya, na baada ya kutenda maovu, anatujaza na hisia za hatia.

Agano Jipya linatuhakikishia kwamba, siku moja Mungu atathibitisha sheria yake. Hapo itakuja hukumu ya mwisho, ambayo ni mada ya sura hii. Kutokana na hiyo neno lingine pia linatumika, 'Mauti ya Pili.' Neno hili linagusa hali ya milele itakavyokuwa kwa wale ambao watahukumiwa katika hukumu ya mwisho.

> *Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao*

*wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, kulingana na matendo yao.*

*Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.* (Ufunuo 20:11–15)

## Wakati Hukumu ya Mwisho itakapotokea

Hukumu hii ya mwisho inamhusu kila mtu binafsi nayo itafanyika baada ya kifo: "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu" (Waebrania 9:27). Lakini kama tukiuliza ni kwa muda gani baada ya kifo cha mtu ndipo hukumu ya mwisho itakuja, jibu ni: Hukumu ya mwisho huja baada ya mbingu na nchi kutoweka mara, huo ni wakati wa mwisho wa dunia au baadaye.

Kwa hiyo ni rahisi kuona kwa nini hilo lazima litokee. Dhambi, ikiwa imetendwa, inaweza kuwa na matokeo yanayoendelea hata baada ya kifo cha mtu aliyetenda dhambi hiyo. Kwa mfano baba wa nyumba kwa njia ya ukali wake na utovu wa upendo, anaweza kumsababishia mwanawe tatizo la kisaikolojia. Mwanawe akiwa katika hali ya kuugua kisaikolojia anaweza kuwa na tabia ya ukatili kwa mkewe, watoto wake, ndugu zake, na wafanyakazi wenzake, ambao pia wanaweza kumtendea vibaya.

Kadhalika uharibifu na uonevu uliofanywa na watawala wa kiimla wakubwa kwa mamilioni ya watu haukukoma pale madikteta hao walipokufa; umeendelea kusambaa kama mawimbi bwawani. Haitawezekana kukisia kwa hakika na ukamilifu jinsi kila dhambi ilivyosababisha mambo magumu mpaka wakati wa mwisho wa dunia tutakapoona historia ngumu ya wanadamu

na kuelewa yaliyo nyuma yake.

## Utimilifu wa Hukumu

Aya iliyonukuliwa hapo juu kutoka katika Agano Jipya, inasema: "*vitabu vikafunguliwa. . . na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu*" (Ufunuo 20:12). Hatuhitaji kufikiri kwamba vitabu vya kumbukumbu vya Mungu vinafanana na vitabu tulivyo navyo duniani: neno 'vitabu' hapa ni msemo lakini neno hili linatukumbusha kwamba Mungu ana kumbukumbu ya kila jambo ambalo kila mtu amewahi kufikiria, kusema na kutenda. Uwezo wa Mungu kutunza kumbukumbu hizo usionekane kuwa jambo la kushangaza kwetu. Wanadamu wenyewe siku hizi wanaweza kutengeneza kompyuta zikiwa na uwezo wa kuweka kumbukumbu zinazokaribia kutokuwa na mipaka.

Agano Jipya pia linatukumbusha kwamba baada ya kifo watu wanaendelea kuwepo, lakini pia wataweza kuyakumbuka maisha yao yaliyopita, labda kwa undani zaidi kuliko walivyoweza katika maisha ya sasa (Luka 16:25). Mungu hatahukumu matendo ya nje tu, bali pia siri za wanadamu (Warumi 2:16). Kwa jinsi tunavyoweza kuyarekodi matendo yetu kwenye video na kisha kuyacheza, ili tuweze kuona leo mambo tuliyosema na kufanya miaka iliyopita, ndivyo Mungu atakavyoweza kuonesha tena mbele ya macho ya watu fikra zao za siri na matendo yao ya wazi ya miaka, na hata karne, zilizopita.

Kwa hiyo hukumu itakuwa ya haki kabisa, maana kila mtu, kama aya yetu inavyosema, atahukumiwa kwa kadiri ya matendo yake. Hakuna atakayeadhibiwa, wala kuzawadiwa, kwa kilichotendwa na mtu mwingine. Kadhalika Hakimu (ambaye hatakuwa mwingine ila Bwana wetu Yesu Kristo: taz. Yohana 5:22, 27–29), atazingatia ujuzi gani watu waliyokuwa nao au wasiyokuwa nao kuhusu mema na mabaya. Yeye mwenyewe anaeleza hivi:

> *Na mtumwa yule aliyejua mapenzi ya bwana wake, asijiweke tayari, wala kuyatenda mapenzi yake, atapigwa sana. Na yule asiyejua, naye amefanya yastahiliyo mapigo, atapigwa kidogo.* (Luka 12:47–48)

Mtu asiyestaarabika anaweza vilevile kuua kwa sababu amelelewa kuanzia utotoni katika kabila lisilo na elimu ambalo limemfunza kwamba kumwua mtu wa kabila lingine ni jambo jema na lenye utukufu. Anachotenda ni dhambi kwa Mungu; lakini hatatendwa kwa uzito sawasawa na mwuza madawa ya kulevya kwenye nchi yenye ustaarabu, ambaye licha ya kuelewa vizuri kwamba uuaji ni dhambi, lakini hata hivyo anawaua kwa makusudi wale wa kundi lingine la wauzaji wa madawa ya kulevya.

Hakimu, yaani Yesu, ameelezea kanuni nyingine itakayoongoza hukumu yake:

> *Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi.* (Luka 12:48)

Mtu mwenye akili nzuri na afya njema ambaye anatumia vipawa vyake kwa ubahili ili ajilimbikizie utajiri bila kujali mateso ya maskini, wala hajajaribu hata kidogo kuwapenda jirani zake kama nafsi yake, huyu atashughulikiwa kwa uzito zaidi ya yule maskini, asiyekuwa na kipaji, na ambaye umaskini wake umemzuia kumsaidia jirani yake (Luka 16:19–31).

## Mwisho wa wote kwa Wasiotubu na Wasioamini

Basi **adhabu** itakayotolewa itatofautiana kati ya mtu na mtu. Kwa upande mwingine, **mwisho** wa wote wasiotubu na wasioamini utafanana. Unaelezwa kwenye Ufunuo 20:11–15 kama *'mauti ya pili'* na *'ziwa la moto.'*

(*a*) **Mauti ya Pili:** Mauti ya pili inaitwa hivyo ili kutofautisha na mauti ya mwili kama tujuavyo hapa duniani. Mauti ya

mwili ni mlango ambao mwanadamu hupitia kwenda mahali pasipoonekana kwetu, ambapo kwenye aya yetu pameitwa Kuzimu (neno la Kigiriki *Hades* likimaanisha 'Pasipoonekana'). Mahali hapo pasipoonekana ndipo zinapofungiwa na kuzuiwa roho za wasiotubu na wasioamini zikisubiri siku ya hukumu ya mwisho, kwa jinsi ileile kama ilivyo kwa mkosaji hapa duniani anapotiwa nguvuni, na kuwekwa rumande hadi atakapofikishwa mahakamani kujibu mashtaka mbele ya hakimu (linganisha Yuda 6).

Ili kuandaa roho hizi kujibu mashtaka, hukumu ya mwisho itatanguliwa na Ufufuo, na roho zitafunguliwa kutoka kizuizini na kuunganishwa tena na miili yao iliyofufuliwa. Katika Ufunuo 20:13 hayo yanaelezwa hivi: *"Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake."* Miili ya wale waliozama baharini (au ya wale ambao majivu yao yalisambazwa kwenye mawimbi) itafufuliwa; na roho zao, hali zimefunguliwa kutoka kwenye kifungo chao cha muda, zitaunganishwa tena na miili yao. Kwa kweli huu ni mfano mmoja tu wa wote ambao walikufa kwa njia nyingi na kwenye sehemu mbalimbali.

Nini kitatokea basi kwa wale watakaokutwa na hatia siku ya hukumu ya mwisho? Watahukumiwa kwenda kuyaonja mauti ya mwili tena? Hapana! Mauti ya mwili, mlango walioupitia kutoka kwenye dunia ya sasa kwenda mahali pasipoonekana, haitakuwa na kazi ya kufanya tena. Badala yake, kutakuwa na mauti ya namna tofauti, ambayo kwenye aya yetu imeitwa Mauti ya Pili. Na kifo hicho kitakuwa cha namna gani?

1. Kwa mtu mmoja mmoja, itakuwa ni hali ya mauti ya kimaadili na kiroho. Angalia tena nini tulichojifunza katika sura yetu iliyopita. Agano Jipya linatangaza kwamba kila mtu asiyezaliwa upya tayari amekufa katika maisha haya, ufahamu wake umetiwa giza, na ametengwa na uhai wa Mungu kwa sababu ya kuufanya moyo kuwa mgumu. Kila mmoja amekufa kiroho, akili zimepotoshwa, na kufishwa kihisia (Waefeso 2:1–3; 4:17–19). Maisha katika dunia

hii yanatupa nafasi ya kutubu, kupatanishwa na Mungu, kuzaliwa upya kiroho, na kuushiriki uhai wa Mungu tukiwa hapa duniani na baadaye. Lakini kama mtu anaitupilia mbali nafasi hiyo, akapitia mauti ya mwili kwenda dunia ya milele, na kuhukumiwa kuwa na hatia siku ya hukumu ya mwisho, basi Mauti ya Pili itamfunga daima katika hali ya utengano mbali na uhai wa Mungu. Haitakuwa maangamizo na kutokuwepo tena; bali itakuwa hali mbaya ya kiroho inayodumu milele, isiyosaidiwa kwa rehema ya Mungu inayotoa uhai wala kwa tumaini lolote la kupunguziwa adhabu.

2. Lakini itakuwa ni mauti ya kiroho sio tu kwa mtu mmoja mmoja, bali kwa jamii (umati) nzima alimokuwa anaishi. Dhambi si ugonjwa wa kiroho ambao mtu anaweza kuugua akiwa ametengwa kutoka kwa watenda dhambi wote wengine. Inajionesha pia kwa jinsi mtu anavyowatazama wengine na katika mwenendo wake akiishi na wengine. Watu ambao katika maisha haya hapa walikuwa wameona wivu, au wenye husuda, au wenye tamaa mbaya, au wadanganyifu, au wakatili, au wenye majivuno, au wenye kutumia mabavu; watu hao hawatabadilika ghafla na kuwa watakatifu kwa kupitia mauti ya kimwili na kusimama mbele ya hukumu ya mwisho. Mauti haitendi miujiza. Maelezo ya Biblia kuhusu ulimwengu ujao si hadithi za masimulizi. Fikiria basi itamaanisha nini kuishi katika jamii kama hiyo iliyoathiriwa hivyo kwa ugonjwa wa kiroho na kimaadili, bila kutulizwa kwa neema ya Mungu ambayo zamani waliweza kuipokea ila kwa sasa hatimaye wameikataa daima.

Agano Jipya linatuelekeza jinsi maisha pamoja na Mungu na waliokombolewa mbinguni yanavyojaa baraka. Linaonesha pia (miongoni mwa mambo mengine) maisha haya yanavyotofautisha na jamii ambayo itakuwako nje:

> *Heri wazifuao nguo zao, ili wawe na haki ya kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya.* (Ufunuo 22:14–15)

(*b*) **Ziwa la Moto**: Hatima ya wasiotubu na wasioamini unaelezwa pia kuwa ni Ziwa la Moto. Hata kama tutafikiri kwamba maneno haya ni ya kimfano na sio ukweli, tunahakikishwa kwamba yanaelekea kwenye ukweli unaokuwa mbaya zaidi sana kuliko maana ya maneno yenyewe tu.

Zaidi ya yote, itabaki uchungu wa kujitambua kuwa umemchukiza Mungu (Warumi 2:4–6). Na pili, uchungu wa kukabili matokeo na mavuno ya tabia na maisha ya dhambi (Wagalatia 6:7–8). Na tatu, kutakuwa na uchungu wa majuto unaosababishwa na kukataa kutubu na kushindwa kutubu dhambi zile zinazoleta majuto (Waebrania 6:4–8).

Moto huo hautaangamiza watu waliomo ndani yake, kama ambavyo moto wa kidunia ungefanya. Bwana wetu Yesu anauelezea kwa maneno haya: *". . .Jahanamu; ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki"* (Marko 9:47–48). Pasipobaki kitu cha kuungua, moto unazimika; na funza anapokosa cha kula, anakufa. Lakini kwa kuwa mtazamo wa dhambi wa waliopotea hautabadilika, uchungu wa hasira ya Mungu ambao wanaupata hautaisha. Na kumbukumbu zinazochochea moto wa majuto hazitafutika.

Kwa upande mwingine, kwa jinsi chumvi inavyozuia uozo kwenye nyama, ndivyo inavyoonekana, moto wa milele utakomesha uozo (mporomoko) wa kimaadili na kiroho wa waliopotea usiongezeke (Marko 9:48–49). Kama vile C. S. Lewis alivyoandika,

> Kwa rehema zake, Mungu kaweka
> machungu ya jahanamu yasienee.
> Ili machungu yabaki yalivyo,
> Mungu katika rehema zake aliweka
> mipaka ya milele na kuyaagiza
> mawimbi ya machungu yasiipite.[1]

1 *The Pilgrim's Regress* ([1933] London: Collins/Fount, 1977) p. 227.

Uharibifu wa kimaadili na kiroho wa kila mtu hautaruhusiwa kuongezeka bila kikomo hadi kufikia wingi usiohesabika. Kwa rehema za Mungu, uharibifu huu utabaki vile ilivyokuwa siku ya hukumu ya mwisho. 'Moto' ule utazuia uharibifu kuendelea.

# 15 Sura

## Hukumu ya Mwisho

### *Wema na Ukali wa Mungu*

Fikra kwamba haki lazima itatendeka na watenda mabaya kuadhibiwa inapaswa kuingia akilini kwa kila mtu mwenye akili timamu kwa kumfanya aridhike na uamuzi huo, na hata kushangilia kwa furaha kubwa juu yake. Mshairi wa kale wa kibiblia anaeleza namna hii:

> *Mwimbieni Bwana sifa kwa kinubi. . . Mito na ipige makofi, milima na iimbe pamoja kwa furaha mbele za Bwana; kwa maana anakuja kuihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa uaminifu, na mataifa kwa adili.* (Zaburi 98:5, 8, 9)

Hata wale wasioamini kuwepo kwa Mungu na ambao hawaamini kwamba kutakuwa na hukumu ya mwisho wangepaswa kutamani iwepo. Kwa hakika hawawezi kufurahia kwamba watu mamilioni ambao wameteseka kutokana na dhuluma maishani na hata kufa bila haki kutendeka hawatapata haki kamwe kufuatana na nadharia zao.

Bado kuna upande mwingine wa mada hii. Wakati kila mtu anasimama upande wa haki, na uadilifu wetu unaafiki kwamba

haki lazima itendeke, moyo wa mwanadamu una sababu zake wenyewe na unashituka linapokuja wazo kwamba mwanadamu yeyote aadhibiwe milele. Inaonekana adhabu itakuwa kali sana na isiyo na usawa kulinganisha na makosa. Hata silika za kibinadamu zingependekeza kwamba rehema ingepaswa kushika nafasi kuliko haki nyofu isiyo na huruma. Na tukiwa tunajisikia hivyo, je, haitamlazimu Mungu kujisikia hivyo hata zaidi?

Tena kuna sababu nyingine kwa nini tunakwepa wazo la hukumu ya mwisho. Ni rahisi kueleza. Kila mmoja wetu anatambua kwamba yeye pia ametenda dhambi, wala siyo tu dhambi zile za watenda uovu wenye sifa mbaya zinazostahili kuadhibiwa, bali dhambi zake pia. Na watu wanapotambua hili, kwa kawaida wanaanza kuibua makinzano ili kujaribu kujihakikishia nafsini mwao kwamba hakuna, na hakutakuwepo kamwe jambo lolote linaloitwa adhabu ya milele. Ebu tuchunguze baadhi ya makinzano.

## Kinzano la 1

*"Mungu wa upendo asingemwadhibu mtu yeyote."*

(*a*) **Jibu la Kwanza**: Kinyume chake ni sahihi. Ni kutokana na sababu madhubuti kwamba Mungu ni Mungu wa upendo ndio maana atapatiliza dhambi. Kama mwuza madawa ya kulevya atamdunga sindano yenye madawa ya kulevya binti yako, akamfanya ayazoee madawa ya kulevya na kuuvuruga ubongo wake, Mungu hatachukulia jambo hili kama si kitu. Anampenda binti yako. Dhambi yoyote dhidi ya binti yako itasababisha ghadhabu ya Mungu. Na kama mwuza madawa ya kulevya asipotubu kamwe, Mungu hatasahau uhalifu huo, hasa kwa kuwa upendo wa Mungu ni wa milele. Na hiyo inamaanisha kwamba ataghadhabika milele dhidi ya mwuza madawa ya kulevya.

(*b*) **Jibu la Pili:** Kwa kweli Mungu ni Mungu wa upendo, na hakuna aliyeweza kutuambia kwa undani zaidi kuhusu upendo wa Mungu na kutufanya kuusikia uhalisi wa upendo wake zaidi kuliko Yesu Kristo. Yamkini kauli kuu na maarufu kuhusu upendo wa Mungu ni hii:

> *Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.* (Yohana 3:16)

Walakini inatubidi kutambua kutokana na aya hii kwamba upendo wa Mungu umedhihirishwa hasa katika kile alichokifanya ili kutuokoa tusipotee. Ametupatia zawadi iliyo kubwa zaidi kuliko nyingine miongoni mwa zote zinazodhaniwa, yaani alitoa nafsi yake yeye mwenyewe, Mwana wa Mungu mwenyewe. Na ametupatia zawadi hii ili kwamba watu kama sisi, ambao ni watenda dhambi, tuweze kusamehewa, na tusije tukapata adhabu kutokana na dhambi zetu. Lakini tena, ukweli ni kwamba ilimbidi Mungu kuchukua hatua hii kubwa mno ili kutuokoa sisi tusipotee, inatusukuma kuzingatia hatari inayomkumba mtu yeyote akipotea.

Mtazamo kama huo pia unajengwa na maneno ya Kristo:

> *Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenituma ana uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.* (Yohana 5:24)

Hapa anatuita tumwamini na kumtegemea ili kwamba aweze kutuepusha na laana zote na kutuokoa na jahanamu. Pengine tunahoji alikuwa na haki gani kusema hivi, na alitoa wito wake kwa kuzingatia misingi ipi. Jibu ni kwamba, kwanza, aliutoa kama yule hakimu wa siku ya hukumu ya mwisho:

> *Tena Baba hatamhukumu mtu yeyote, bali amempa Mwana hukumu yote. . . naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu.* (Yohana 5:22, 27)

Na katika sehemu ya pili, jibu ni kwamba Yeye ambaye atakuwa hakimu siku ya hukumu ya mwisho ndiye huyo huyo ambaye pale msalabani alibeba deni na adhabu ya sheria ya

Mungu kwa niaba ya wote watubuo na kuamini, ili kwamba wasije wakabeba adhabu na mapatilizo wao wenyewe. Bali matokeo yasiyoepukika katika hili ni: ikiwa mtu yeyote atapuuza wito wa Kristo kwa ajili ya toba na imani, hataepuka kupotea.

Kwa hiyo, kwa hatua hii tunalazimika kuitazama tena aya ambayo tuliisoma kwenye sura iliyopita na kutambua hasa kwamba inachokisema ni jambo lenye maana la kuamua iwapo mtu atatupwa katika Ziwa la Moto au la. Hizi hapa ni aya husika:

> *Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, kulingana na matendo yao. . . Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.* (Ufunuo 20:11, 12, 15)

Kwanza tambua nini hakisemwi. Haisemi kwamba kama mtu ataonekana ametenda dhambi nyingi na mbaya sana, ndipo atatupwa katika Ziwa la Moto; wala haisemi kwamba kama mtu ataonekana ametenda dhambi chache na ndogo sana na kuzifidia kwa kufanya matendo mengi mema, hatatupwa katika Ziwa la Moto. La hasha, kulingana na aya yetu hoja madhubuti ni hii: *"Iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto"* (Ufunuo 20:15).

Hicho **kitabu cha uzima ni kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo** (taz. Ufunuo 21:27), na ndani ya kitabu hicho yameandikwa majina ya wale wote ambao wametubu na kuweka imani yao kwa Mwana-kondoo wa Mungu. Na kwa sababu alilipa deni la dhambi zao kwa ajili yao, Agano Jipya linawapatia uhakika huu wenye utukufu: *"Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. . . bali wataokolewa na ghadhabu* [ya Mungu]

*kwa yeye"* (Warumi 8:1; 5:8–9). Na zaidi, wale wote waliompokea Kristo kuwa mbadala na Mwokozi wao wanaweza kujua hapa na sasa katika maisha haya kwamba majina yao yameandikwa katika kitabu hiki cha uzima. Mtume Paulo na rafiki zake walijua hilo (Wafilipi 4:3); nasi tunaweza kujua pia.

Hata hivyo, iwapo watu watamkataa Mwokozi ambaye Mungu amemtoa, kama ambavyo wengi wanafanya, majina yao hayaandikwi katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo. Mungu atafanya nini basi ili kuwaokoa? Wamefanya uchaguzi wao wenyewe. Hawataepuka kutupwa katika Ziwa la Moto, na kupata adhabu na matokeo ya dhambi zao. Walakini hawatakuwa na wa kumlaumu isipokuwa wao wenyewe. Hakika, hawataweza kumkosoa Mungu kwa ajili ya hilo. Mungu ni jumla ya wema wote. Kwa kutumia maana halisi ya mbingu hakutakuwa na mbingu nyingine kwa ajili ya wale wanaomkataa. Wala Mungu hawajibiki kutoa yasiyowezekana. Walipenda giza badala ya nuru kwa sababu matendo yao ni maovu (Yohana 3:19); na watapewa kile ambacho wao wenyewe wamechagua.

Sasa na tutambue sifa nyingine ya haki ya Mungu. Wote wanaokataa wokovu wa Mungu watakuwa sawa katika hili, yaani watatupwa katika Ziwa la Moto. Bali si wote watakaostahimili uzito sawa wa adhabu. Aya yetu inatuambia kwamba watahukumiwa sawasawa na matendo yao. Hata katika mahakama za kibinadamu za haki, watu wawili wanaweza kutiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela kwa kosa linalofanana, ila wanaweza kupokea hukumu zinazotofautiana kwa sababu ya kesi moja kuwa na hali fulani iliyopunguza ukali wa adhabu na kesi nyingine kukosa hali hiyo. Mwanamke anayeishi maisha ya kifahari ambaye majivuno yake humzuia kujinyeyekeza, kutubu na kumwamini Mwokozi, atapata hasara ya milele, lakini hataadhibiwa kwa kiwango sawa cha mateso na, tuseme kwa mfano, Hitler ambaye mikono yake imejaa damu za mamilioni ya watu.

Zaidi ya hayo, ili kuona kwamba Mungu anatenda kwa haki na usawa, ebu tujikumbushe sifa nyingine ya hukumu yake.

Wote ambao wanaweka imani yao kwa Kristo ili wapate wokovu watapata wokovu wa milele sio katika msingi wa matendo yao bali katika msingi wa imani yao. Kwa upande mwingine, wale ambao tangu kubadilishwa kwao wamekuwa wakiishi maisha ya kumpendeza Mungu watapewa thawabu ya matendo yao mema, wakati ambapo wale waamini halisi ambao hata hivyo wameishi pasipo umakini na kutenda matendo yasiyofaa watapata hasara. Matendo yao yasiyostahili yatateketea, ingawa wao wenyewe wataokolewa, *"lakini ni kama kwa moto"* (1 Wakorintho 3:14–15).

## Kinzano la 2

***"Lakini mamilioni ya watu walioishi karne za kabla ya Kristo, na mamilioni walioishi baada yake, hawakupata kusikia kuhusu Yesu. Je, itakuwa haki Mungu akiwahukumu kwa kuwa hawakumwamini Yesu?"***

Hasha, hatafanya hivyo. Mungu hatamhukumu mtu yeyote kwa kutoamini jambo ambalo hakupata kulisikia (Yohana 15:22–24). Lakini watu wote wanajua kabisa ndani ya mioyo yao kwamba Mungu yupo. Ulimwengu na vitu vyote vinatoa ushahidi wa ziada wa kuwepo kwake. Na watu wote wanajua mioyoni mwao kwamba wamemtenda Mungu dhambi (Warumi 1:18–2:16). Wale ambao wanakiri na kujikabidhi wenyewe katika rehema ya Mungu watasamehewa. Kifo na dhabihu ya Kristo msalabani ni sababu kamilifu za Mungu kuwasamehe dhambi zao hata kama hawakupata kusikia habari za Yesu (Warumi 3:25). Kwa hiyo wanadamu watahukumiwa kufuatana na mwitikio wao kwa nuru ile waliyokuwa nayo, wala si kwa kadiri ya nuru ambayo hawakuwahi kuwa nayo.

Lakini wote ambao wanasoma kitabu hiki wamesikia kuhusu Yesu, na wanahitaji kumwacha awaonye kwamba katika hukumu ya mwisho tahadhari kubwa itachukuliwa kutathmini kiwango cha nuru walichokuwa nacho kila mmoja, na nafasi gani za kuujua ukweli na kuuamini zilizokuwepo. Kwa maelezo ya Kristo, wale wenye nuru zaidi sio lazima wawe wale walioitikia inavyopaswa.

Wakati wa Kristo duniani wengi wa watu waliostaarabika na wafuasi wa dini hawakuwa tayari kutubu na kuamini kuliko wapagani walioitikia vizuri (Luka 11:29–32).

## Kinzano la 3

*"Isingekuwa haki kwa Mungu kumwadhibu mtu umilele wote kwa ajili ya dhambi, hata iwe kubwa au ndogo, zilizotendwa ndani ya kipindi kifupi cha maisha yake cha miaka sabini au zaidi kidogo."*

Lakini kinzano hili linatokana na fikra potofu za aina mbili:

1. Kudhani kwamba kwa kutenda dhambi katika maisha haya, wale ambao wanamkataa Mungu na Kristo wataacha kutenda dhambi na kuwa wenye dhambi katika ulimwengu ujao. Hiyo si kweli.

2. Kudhani kwamba kwa kukataa kutubu katika maisha haya, watatubu na kumwamini Mwokozi katika ulimwengu ujao. Lakini hilo si kweli pia. Wale ambao wamemkataa Mwokozi na kumwasi Mungu wakiwa hapa duniani, wataendelea kumkataa Mwokozi na kumwasi Mungu baada ya hapa. Wana hatia ya dhambi ya milele (Marko 3:29). Bwana wetu alisimulia simulizi kuhusu mtu tajiri (Luka 16:19–31) ambaye alijikuta ametengwa na Mungu baada ya kufa kwake. Alipokuwa kwenye mateso alionesha ushahidi wa majuto na mahangaiko, bali hakuwa na ushahidi wowote wa toba ya kweli.

## Kinzano la 4

*"Iwapo mambo hayo yote yangekuwa kweli, Mungu wa upendo angewashurutisha watu kutubu na kuamini hata wasipokubali kwa hiari yao"*

Hapana, asingefanya hivyo. Moja ya mambo yanayomtofautisha mwanadamu na wanyama wengine na mimea ni kuwa na uhuru wa uamuzi. Mwanadamu ni kiumbe cha kimaadili na cha kiroho, aliyeumbwa katika mfano wa Mungu, akiwa na nguvu ya pekee ya kuchagua ama kumpenda na kumtii Muumba

wake au kumkataa. Mungu hataondoa huo utashi huru kutoka kwa mwanadamu, hata kama ni kwa lengo la kumwokoa. Kwa maana kama angefanya hivyo, kiumbe ambacho kingeokolewa kisingekuwa mwanadamu tena, bali kingekuwa mnyama, mmea, ama hata mashine. Hata hivyo, Mungu si mtawala wa kiimla. Inawezekana kwa mwanadamu kumkataa na kumkana, na bado kubaki milele.

## Kinzano la 5

*"Kuelekeza mawazo ya watu kwenye hatima yao ya baada ya kufa kunawasumbua kimaendeleo na kuwakatisha tamaa kuyafurahia maisha yao ya hapa duniani."*

Kinyume chake ndio ukweli. Imani katika mbingu na jahanamu inaelekeza kila fikra, mtazamo, na kitendo katika maisha yetu duniani zikihesabiwa kuwa thamani zenye umuhimu wa milele. Kukataa kuamini katika mbingu na jahanamu kunamshusha na kumpunguza binadamu hadhi ya mwenendo wake wa kiroho na wa kimaadili.

## Kinzano la 6

*"Ni kiumbe kibaya kisicho na hisia wala asiye na hali ya kibinadamu tu ndiye anayeweza kuamini na kuhubiri kuhusu jahanamu ya milele."*

Lakini ilikuwa ni Yesu Kristo aliyekuwa akitufundisha, zaidi ya yeyote, kuwa Mungu ni pendo, na kwa njia ya machozi yake alituonya juu ya ukweli kuhusu jahanamu. Alizungumza juu ya somo hili zaidi ya mtu yeyote mwingine katika Biblia nzima. Yeye yule aliyekufa ili atuokoe na jahanamu, pia anatuonya kwamba hakufa pasipo sababu; na anaomboleza juu ya watu wasiotubu leo kama alivyoomboleza hapo awali juu ya Yerusalemu:

> *"Ee Yerusalamu, Yerusalemu, uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe waliotumwa kwako, mara ngapi nimetaka kuwakusanya*

*watoto wako kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake, wala hamkutaka."* (Luka 13:34)

Kwa kupitia ombolezo hili la Kristo mapigo ya moyo ya Mungu wetu Muumba husikika: *"Maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana Mungu; basi ghairini, mkaishi"* (Ezekieli 18:32).

Kwa hiyo ingekuwa busara kwetu kufuata mfano wa wale mamilioni wasiohesabika katika karne zilizopita ambao walimgeukia Mungu na kuziacha sanamu, *"ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli; na kumngojea Mwanawe kutoka mbinguni, ambaye alimfufua katika wafu, naye ni Yesu, mwenye kutuokoa kutoka kwa ghadhabu itakayokuja"* (1 Wathesalonike 1:9–10).

# 16 Sura

## Wokovu

### *Neno Linalojumlisha Yote*

Wazo la wokovu ndilo kiini cha Agano Jipya; na sababu yake ni dhahiri. Kristo alipokuwa yu karibu kuzaliwa, Yusufu, mume mtarajiwa wa Mariamu, alielekezwa kumwita mtoto jina la 'Yesu,' neno la Kigiriki ambalo kwa Kiebrania humaanisha "Bwana anaokoa." Alipewa jina hili, kama ilivyonenwa na malaika, *"maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao"* (Mathayo 1:20–21). Basi, wokovu ulikuwa ndio kusudi pekee la ujio wa Kristo hapa ulimwenguni: *"Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."* (Luka 19:10; pia taz. Yohana 3:17; 1 Timotheo 1:15).

Kwa hiyo, maneno haya wokovu, Mwokozi, kuokoa yanatokea mara kwa mara kwenye Agano Jipya. Zaidi ya hayo, 'wokovu' ni neno pana, na lenye mambo mengi. Linakusanya maneno mengine mengi ndani yake, kama vile kuhesabiwa haki, ukombozi, kuzaliwa kwa mara ya pili, uzima wa milele, n.k. ambayo tumeshayasoma; kwani kila moja ya hayo huelezea kipengele kimojawapo cha wokovu. Aidha, wazo juu ya wokovu mara nyingi hutumika katika mazingira hata kama neno lenyewe halijatajwa. Kufuatana na hilo, somo la 'wokovu' litatusaidia kupitia mawazo tuliyoeleza kwenye kitabu hiki.

## Vidokezo vya Wokovu kwa mapana

Kitenzi cha Kigiriki 'kuokoa' (*sozo*) kinabeba vidokezo kadhaa. Huweza kutumika kama kumwokoa mtu katika hatari; au kumnusuru mtu katika ugonjwa, yaani, 'kuponya.' Kwenye injili mbalimbali tunasoma Yesu akiwaokoa watu kwa namna tofautitofauti. Kwa kuitikia ombi la Petro, *"Bwana, niokoe,"* Kristo anamwokoa asizame majini (Mathayo 14:30–31). Anamponya mwanamke aliyeugua kwa muda mrefu, na kusema, *"Binti, imani yako imekuponya* [imekuokoa]*; enenda zako na amani"* (Luka 8:48). Anamhakikishia mtu ambaye binti yake wa pekee alikuwa amekufa, *"Amini tu, naye ataponywa* [ataokolewa]*,"* na akaendelea hadi nyumbani kwa yule mtu na kumwinua binti yake kutoka kwa wafu (Luka 8:49–56).

Hata hivyo, kwingineko Kristo anatumia neno 'kuokoa' katika namna ya kimaadili na kiroho. Kwa mfano, alimwambia mwanamke mwenye dhambi, lakini aliyetubu: *"Umesamehewa dhambi zako. . . Imani yako imekuokoa, nenda zako kwa amani"* (Luka 7:48, 50). Basi ni kwa maana hii kwamba maneno 'kuokolewa' na 'wokovu' yametumika mara nyingi zaidi kwenye Agano Jipya; na matendo mengi ya Kristo ya uponyaji wa kimwili na uokoaji hutumika pia kueleza maana ya wokovu katika ngazi ya kiroho.

Kwenye Yohana 9, Bwana wetu alipomfanya mtu aliyezaliwa akiwa kipofu aone, Kristo alitumia wokovu huu wa kimwili kama kielelezo cha uwezo wake wa kuwapa vipofu wa kiroho macho ya kiroho: *"Yesu akasema, 'Mimi nimekuja ulimwenguni humu kwa hukumu, ili wao wasioona waone, nao wanaoona wawe vipofu.'"* (Yohana 9:39). Nia yetu ya msingi (ingawa si ya kipekee) katika vipengele vilivyosalia vya sura hii itakuwa kuuchambua wokovu katika ngazi ya kimaadili na kiroho.

Sasa basi, kwa kuwa ni neno lenye mambo mengi, linalodokeza jinsi ambavyo Mungu ameshafanya, anafanya, na ataendelea kufanya kwa ajili ya mwamini, neno hili linazungumzwa katika nyakati tatu: wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao.

## Wokovu katika Wakati Uliopita

Kwa mujibu wa Agano Jipya, Mungu hutaka watu wote waokolewe, na kwa hali hiyo Kristo akajitoa mwenyewe kama fidia kwa ajili ya watu wote (1 Timotheo 2:3–6). Kwa hiyo, habari njema ni kwamba wokovu unapatikana kwa ajili ya watu wote, ingawa unafanya kazi endapo tu watu wataamini. Hata hivyo, mara punde mtu anapoamini, anaweza kuuzungumzia wokovu wake kuwa sasa umetimia. Hahitaji kujibana mwenyewe kwa kusema, 'yamkini natumaini kuokolewa mwishowe.' Anaweza kwa usahihi kutumia kitenzi cha wakati uliopo timilifu na kusema, 'Nimeokolewa.' Agano Jipya linanena na waamini kwa kusema: *"tumeokolewa kwa neema"* (Waefeso 2:5). Hiyo haimaanishi kwamba wanaoamini wameshauonja wokovu wote, kwani baadhi ya awamu za wokovu bado zinakuja. Lakini inakuwa kweli kwamba awamu chache za wokovu zinatekelezwa na kukamilishwa pindi mtu anapojitoa mwenyewe kwa Kristo, katika kweli na kwa hiari yake.

Baadhi ya awamu hizi ni:

1. **Msamaha:** Kwa habari ya mwanamke mtenda dhambi aliyetajwa hapo awali, Kristo alitumia njeo timilifu mara tatu: *"Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi. . . Umesamehewa dhambi zako. . . Imani yako imekuokoa"* (Luka 7:47, 48, 50). Vivyo hivyo, Mtume Yohana asema: *"Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu mmesamehewa dhambi zenu, kwa ajili ya jina lake"* (1 Yohana 2:12); na Mtume Paulo anaandika: *"Yeye* [Mungu]*. . . akiisha kutusamehe makosa yote"* (Wakolosai 2:13).

Sitiari kadhaa zimetumika katika Maandiko ili kutusisitizia ukamilifu wa msamaha huo. Mungu ameweka dhambi zetu —

(*a*) Asizione: *"Umezitupa dhambi zangu zote nyuma yako"* (Isaya 38:17);

(*b*) Kusikofikika: *"Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi"* (Zaburi 103:12);

(*c*) Zisiwepo tena: *"Mimi, ndimi niyafutaye makosa yako"* (Isaya 43:25);

(*d*) Kusikoweza kukumbukwa: *". . .dhambi yao sitaikumbuka tena"* (Yeremia 31:34);

(*e*) Kusikoweza kurejeshwa: *"Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu; . . . atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari"* (Mika 7:18–19).

2. **Kuzaliwa mara ya pili na maisha mapya ya kiroho** (taz. Sura ya 7):

(*a*) *"Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa mara ya pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu"* (Tito 3:5).

(*b*) *"Lakini Mungu. . . hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alitufanya kuwa hai pamoja na Kristo,. . . kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu"* (Waefeso 2:4–9).

3. **Upatanisho na Mungu** (taz. Sura ya 4): *"Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho"* (Warumi 5:11).

## Wokovu katika Wakati Uliopo

Wokovu hauhusu tu maisha ya mtu yaliyopita. Unagusa mambo yake yaliyopo pia. Mfano mzuri wa kuanza nao ni ule wa Zakayo (soma habari yake kwenye Luka 19:1–10). Wokovu ulipokuja nyumbani kwa Zakayo, ulimletea msamaha kwa ajili ya mambo yaliyopita, lakini pia, ghafla wokovu ulibadilisha mtindo wa maisha yake ya sasa. Ulianza kushitua dhamiri yake ya kijamii. Pale ambapo alikuwa ametoza watu kodi zaidi ya kiwango alichotakiwa kutoza kisheria, aliahidi kuwarudishia mara nne. Alifanya zaidi ya hilo. Hakuwa tayari kuendelea kuvuna pesa nyingi kwa ajili yake mwenyewe, hata kama ilipokelewa kihalali, wakati raia wenzake wengi wakiendelea kuzama katika dimbwi la umaskini. La hasha, akasema *"Nusu ya mali yangu nawapa maskini."*

Kuwajali maskini, wagonjwa, na walemavu daima kumekuwa ni alama ya Ukristo wa kweli. Kiukweli, wale ambao wameokolewa kwa njia ya injili ya Kristo, wana jukumu la kuenenda kwa njia hiyo katika mahusiano yao yote ya maisha *"ili wayapambe mafundisho ya Mungu aliye Mwokozi wetu katika mambo yote."* Yaani, wanahitaji kudhihirisha kwamba injili ina mvuto wakiwa wanaonesha matokeo yake katika maisha ya kila siku (Tito 2:10–14, hasa 10).

Hii hapa ni sehemu nyingine inayoonesha jinsi wokovu unavyohitaji kumtawala Mkristo maishani mwake. Kristo anaeleza hivi: *"Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza* **nafsi** *yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha"* (Marko 8:35). Itatusaidia tukianza kwa kuuelewa usemi huu, kama tukiona kwamba neno la Kigiriki lililotafsiriwa hapa kama **"nafsi"** linabeba maana pana. Linaweza kumaanisha uhai wa mtu (kama kwa mfano katika Mathayo 2:20): *"kwa maana wamekufa walioitafuta* ***roho*** *ya mtoto."* Linaweza pia kumaanisha maisha ya mtu ya ndani kabisa, yote ambayo humfanya mtu kuwa zaidi ya uwepo wa kimwili tu, yaani upendo wake, nguvu, ufahamu, hisia, uwezo, utashi na ari zake (kama ilivyo kwenye 3 Yohana 2): *"Naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako* [ya mwili]*, kama vile* ***roho*** *yako ifanikiwavyo."* Usemi wa Bwana wetu (Marko 8:35) unabeba vidokezo vyote, kama tutakavyotazama hivi karibuni.

Walakini ni kwa jinsi gani mtu anaweza kuokoa maisha yake, au nafsi yake, kwa kuiangamiza? Inaonekana ni maelezo yanayopingana. Kwa kweli inawezekana kuuelewa ikiwa tu tunakumbuka kwamba wakati huu uliopo si jumla ya awamu zote: kuna wakati mwingine, yaani ufalme wa Mungu unaokuja. Huu ulikuwa ule ambao Kristo alifundisha akisema: *"Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu"* (Marko 8:38).

Kristo alikuwa ametabiri kwamba watu wenye mamlaka walioko Yerusalemu wangemwua. Ndipo Petro, hali akihisi kwamba iwapo hili lingetokea, wangemwua naye vivyo hivyo, alijaribu kumshawishi Kristo aepukane na hili ili asiuawe. Bali Kristo hakutaka kuharibu dhima yake kwa ajili ya kuyaokoa maisha yake. Alimwonya Petro asijaribu kuyaokoa maisha yake katika ulimwengu huu kwa kumkana Kristo; ikiwa angefanya hivyo, angeyapoteza katika ulimwengu ujao. Twafahamu kuwa Petro mwishowe alipoteza ujasiri wake na kumkana Kristo. Lakini hili lilikuwa ni kuteleza kwa muda tu, na kutoka humo Kristo alimrejesha kwake kwa kumwombea (Luka 22:31–34).

Lakini fundisho linabaki kwa ajili yetu sote. Tunakiri kwamba hatuupati wokovu kwa kuwa mashahidi wa imani wanaokufa kwa ajili ya Kristo. Wokovu ni zawadi ya bure. Ila hatuwezi kuwa na zawadi ya wokovu bila ya Mwokozi. Maandiko yanasema *"Mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake"* (Wafilipi 1:29). Basi ebu fikiria kama tukikutana na muda ambapo tunapaswa kuchagua kati ya mawili: ama kumkana na kumkataa Kristo ili kuyaokoa maisha yetu ya kimwili hapa ulimwenguni, au kushikilia imani yetu katika Kristo, kuwa waaminifu kwake, na hivyo kupoteza maisha yetu hapa ulimwenguni. Basi tujiandae kuyapoteza maisha yetu katika ulimwengu huu, ili tuwe na uhakika kuyaokoa katika ulimwengu ujao; lakini iwapo tutayaokoa maisha yetu katika ulimwengu huu kwa kumkana Kristo, tutayapoteza katika ulimwengu ujao.

Aidha, maisha katika ulimwengu huu siyo kitu tunachoweza kukiweka kwenye sanduku ili kuyatunza. Inabidi kuyaishi maisha: nguvu zake, muda, ari, upendo, na uwezo wake inabidi vitumike kwa watu au kwenye vitu au kwenye miradi. Swali ni: Je, tutavitumia kwenye nini?

Mwamini anaalikwa kuyatenda yote ayatendayo kwa moyo kama kwa Bwana (Wakolosai 3:23) na kutoa muda na nguvu zake kwa kadiri awezavyo katika kuisambaza injili ya Kristo. Ikiwa atapanga kuyatumia maisha yake kwa jinsi hii, mapema au

baadaye atajikuta akiwa anatoa aina zote za dhabihu na kujikana mwenyewe. Kwa mtu mwenye mawazo ya kidunia, mwamini ataonekana kuwa anayapoteza maisha yake na kuyatupilia mbali. Lakini kwa kweli, kila jambo ambalo mwamini ama anafanya kwa ajili ya Kristo au anatumia kwa ajili ya Kristo na matakwa yake, atavuna faida ya kudumu na ya kubaki milele. Matokeo yake yatadumu milele (Yohana 12:25).

Ikiwa, kwa upande mwingine, mwamini hayuko tayari kuishi kwa ajili ya Kristo, na badala yake anatumia muda, nguvu, upendo, na uwezo wake kwa uchoyo na ubinafsi na kwa mambo ya kidunia yasiyo na tija wala yasiyostahili, ndipo mbele ya ufalme wa milele wa Mungu, yale yote ambayo mwamini ametumia kwa mambo haya ya kidunia yatapotea milele. Na Kristo ajapo mara ya pili atayatathmini matendo yake mtu huyo, matendo yake yatateketezwa na atapata hasara, ingawa yeye mwenyewe ataokolewa (1 Wakorintho 3:10–15).

## Wokovu katika Wakati Ujao

Wakati mwamini anaweza kusema kwa uhakika kuwa, "Nimeokolewa," sehemu muhimu za wokovu wake bado zitapatikana kwenye wakati ujao. Hiyo ndiyo sababu mwamini anatakiwa kutegemea kuzipokea. Si kwa sababu hana uhakika wa kuzipokea bali kwa sababu bado haziko tayari kwa sasa.

Kwa usahihi, anaweza kuzungumzia pia kwa ujasiri na kukiri kwa unyeyekevu, "Nitaokolewa." Hivi vigezo vinavyofuata vya wokovu vinajumuisha:

1. Wokovu kutoka katika ghadhabu ya Mungu: *"Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye"* (Warumi 5:9; taz. pia 1 Wathesalonike 5:9–10).

2. Ukombozi wa miili yetu: hili pia ni jambo ambalo litafanyika katika ujio wa pili wa Kristo.

(*a*) *"Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili*

*mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"* (Wafilipi 3:20–21).

(*b*) *"Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu. Kwa maana tuliokolewa kwa tumaini; lakini kitu kinachotumainiwa kikionekana, hakiwi tumaini tena. Kwa maana ni nani anayekitumaini kile akionacho? Bali tukikitumainia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi"* (Warumi 8:23–25).

**3. Utakaso wa mwisho wa Mkristo** (taz. sura ya 13):

(*a*) *"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu"* (taz. 1 Petro 1:3–4).

(*b*) *"Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu"* (Wakolosai 3:4).

**4. Mlango wa Mkristo kuingia mbinguni:**

Njia ya kuingia mbinguni kwa mwamini iko kwa namna mbili. Hali ya wale watakaokufa kabla Bwana hajarudi inaelezwa kwa *"kutokuwemo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana"* (2 Wakorintho 5:8) ingawa miili yao haijafufuliwa bado. Kisha atakapokuja Bwana, miili ya waamini hao itafufuliwa, miili ya waamini walio hai itabadilishwa, na wote watanyakuliwa kumlaki Bwana mawinguni (1 Wathesalonike 4:13–18).

> *Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. . . Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda.* (1 Wakorintho 15:51–52, 54)

Ni katika maana hii Maandiko yanasema: *"kwa maana sasa wokovu wetu uko karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini"* (Warumi 13:11) — karibu zaidi, kwa sababu kwa kila siku inayopita ujio wa pili wa Kristo unakaribia zaidi.

# Marejeo ya Biblia


**AGANO LA KALE**

**Mwanzo**
1 *71*
1:31 *16*
3 *25, 30*
3:1–7 *98*

**Kutoka**
34:5–7 *15*

**Mambo ya Walawi**
19:2 *15*
19:18 *15*

**Kumbukumbu la Torati**
6:13 *12*
25:1 *37*

**1 Samweli**
2:2 *11*

**1 Mambo ya Nyakati**
16:29 *11*

**Zaburi**
43:4 *10*
92:15 *13*
98:5–9 *127*
103:12 *138*

**Mithali**
17:15 *38*
30:20 *47*

**Isaya**
5:7–30 *14*
5:15–16 *14*
5:16 *13*
5:24 *14*
6:3 *14*
6:5 *14*
38:17 *138*
43:3 *18*
43:11 *73*
43:25 *138*
45:11–12 *11–12*
45:18 *12*
45:20–22 *17*
46:1–7 *11*
53:4–6 *92*
53:5 *17*
53:6 *63*
53:10–12 *92*
54:5 *18*
55:7–8 *63*

**Yeremia**
31:34 *139*

**Ezekieli**
11:19–20 *99*
18:32 *135*

**Mika**
7:18–19 *139*

**AGANO JIPYA**

**Mathayo**
1:20–21 *136*
2:20 *140*
3:8 *68*
3:10 *65*
4:4 *54*
4:10 *12*
5:23–24 *29*
5:33–37 *78*
5:43–48 *111*
14:30–31 *137*
15 *104*
27:3–5 *62*
27:11–26 *22*
27:62–66 *87*
28:1–10 *89*

# Marejeo ya Biblia

*Mathayo*
28:11–15 *87*
28:16–20 *90*

**Marko**
1:15 *61*
3:29 *133*
8:35 *140*
8:38 *140*
9:47–48 *125*
9:48–49 *125*
10:45 *49*

**Luka**
6:43–44 *65–6*
7:29 *37*
7:47 *138*
7:48 *137, 138*
7:50 *137, 138*
8:48 *137*
8:49–56 *137*
9:22 *53*
11:29–32 *133*
12:4 *53*
12:47–48 *122*
12:48 *122*
13:3 *68*
13:5 *68*
13:34 *134–5*
15 *36*
15:10 *61*
15:32 *56*
16:19–31 *122, 133*
16:25 *121*
18:9–14 *38*
18:13 *42*
19:1–10 *139*
19:10 *136*
22:31–34 *141*
22:31–32 *100*
23:1–25 *22*
24 *90*

**Yohana**
1:1–4 *71*
1:1–3 *11*
2:13–16 *47*
3:16 *58, 129*
3:17 *26, 136*
3:19 *131*
3:36 *55*
5:22 *121, 129*
5:24 *42, 129*
5:27–29 *121*
5:27 *129*
5:36 *76*
6 *79*
6:26 *79*
6:28–58 *80*
6:35 *80*
7:1–7 *81*
7:16–17 *72*
8:13 *74*
8:14 *74*
8:28 *83*
8:31–36 *80*
9 *137*
9:39 *137*
10:11 *84*
10:14–17 *84*
10:28 *58*
12:25 *60, 142*
12:37 78
13:6–11 *106*
14:6 *78*
15:22–24 *132*
15:24 *76*
16:1–3 *53*
16:7–14 *91*
16:28 *91*
18:28–19:16 *22*
17:1–3 *53*
17:3 *58*
17:17 *116*
19:8–12 *22*
20:1–10 *87*
20:11–18 *89*
20:19–23 *90*
20:30–31 *72, 77*
21 *90*

**Matendo**
1:4–9 *91*
1:21–22 *91*
2:36–39 *30*
2:38 *91*
4:12 *94*
9 *89*
9:32 *101–2*
11:18 *61*
15:8–9 *105*
17:30 *68*
20:21 *63, 68, 69*
20:28 *52*

**Warumi**
1:18–2:16 *132*
1:27 *13*
2:4–6 *125*
2:14–16 *48*
2:14–15 *119*
2:16 *121*
3:10–18 *21–2*
3:19–28 *110*
3:19 *40*
3:20 *41*
3:23–26 *42*

## Mwelezo wa Biblia


*Warumi*
3:23 *40, 65*
3:25 *132*
3:28 *43, 94*
4:5 *94*
5:1–2 *117*
5:1 *33, 42–3*
5:5 *105*
5:6–11 26
5:6 *22*
5:8–9 *130–1*
5:9 *142*
5:11 *33, 139*
5:19 *26*
6:1–2 *111*
6:3–4 *66*
6:6–11 *114*
6:8–11 *66*
6:14 *114*
6:15 *111*
6:16–23 *52*
6:23 *59*
7:4 *115*
7:5 *24*
7:6 *116*
7:7–25 *111*
7:7–9 *24*
7:7–8 *112–13*
7:12 *112*
7:15 *112*
7:18–19 *112*
7:19 *20*
7:21–24 *112–13*
7:22 *112*
7:23 *112*
7:25 *112*
8:1 *130–1*
8:3 *112*
8:4 *115*
8:7 *23*
8:13–17 *111–12*
8:14–17 *105, 116*
8:18–25 *52*
8:23–25 *143*
8:26–30 *116*
10:9 *69*
12:1–2 *106–7*
13:11 *144*

**1 Wakorintho**
1:2 *102*
1:18 *80–1*
1:22–23 *80–1*
1:30 *108*
2:2 *80–1*
2:5 *80–1*
3:10–15 *142*
3:14–15 *132*
6:11 *102*
6:15–17 *67*
6:16–17 *115*
6:19–20 *107*
9:24–27 *60*
10:13 *100*
15:3–8 *89–90*
15:3–4 *92*
15:20–23 *85*
15:51–52 *143*
15:54 *143*

**2 Wakorintho**
4:17 *59*
5:1 *58–9*
5:8 *54, 143*
5:14–15 *107*
5:18–21 *29*
5:19–21 *32*
5:19 *29, 30*
6:1 *34*
7:1 *110*
7:10 *62*

**Wagalatia**
2:19–21 *67*
2:20 *67*
3:10–12 *94*
3:13 *48*
5:16–24 *116*
5:19–21 *21*
6:7–8 *125*
6:8 *59, 116*

**Waefeso**
1:7 *48*
1:13–14 *52*
2:1–3 *65, 123*
2:4–9 *139*
2:4–5 *57*
2:5 *138*
2:8–10 *99–100*
2:8–9 *95*
2:11–18 *33–4*
2:18 *105*
3:5 *101*
4:17–24 *111*
4:17–19 *123*

**Wafilipi**
1:23 *54*
1:29 *141*
3:12 *117*
3:20–21 *52, 142–3*
4:3 *131*

**Wakolosai**
1:14–17 *49–50*
1:15–22 *28–9*

*Wakolosai*
1:17 *11*
1:19–20 29
1:20 *34*
1:21 *24*
2:13–15 *49*
2:13 *138*
3:4 *143*
3:23 *141*

**1 Wathesalonike**
1:9–10 *135*
1:9 *63*
4:13–18 *143*
5:9–10 *142*

**1 Timotheo**
1:9–11 *23*
1:12–17 *24*
1:15 *26, 136*
2:3–6 *84–5, 138*
2:5–6 *50, 93–4*
4:7–8 *59*
6:11–12 *59*
6:12–16 *100*

**2 Timotheo**
2:5 *60*
2:13 *51*
4:7–8 *100*

**Tito**
1:2 *51*
2:10–14 *140*
2:11–14 *52*
3:5 *104, 139*

**Waebrania**
5:9 *59*
6:1 *63*
6:4–8 *125*
7:25 *100*
9:11–12 *48*
9:12 *59*
9:13–14 *103, 104*
9:15 *59*
9:27 *42, 120*
10:5 *103*
10:7 *103*
10:10 *103*
10:11–12 *94*
10:14 *106*
10:19–22 *106*
11 *100*
11:3 *71*
12:1–13 *117*
12:1 *60*

**Yakobo**
2:10 *40*
2:19 *74*
2:24 *43*

**1 Petro**
1:2 *104*
1:3–4 *85, 143*
1:6–7 *100*
1:8 *86*
1:14–16 *105*
1:18–19 *49*
1:18 *46*
1:21 *85*
2:5 *106*
2:9–10 *14–15, 106*
3:14–15 *12*

**2 Petro**
1:1–11 *115*
1:5–11 *60*
3:2 *101*
3:9 *83*

**1 Yohana**
1:1–4 *58*
1:5 *13*
1:7 *104*
1:9 *68, 114–15*
2:12 *138*
2:21 *78*
3:2 *117*
3:4 *25*
3:16 *91*
4:10 *50*
4:16 *15*
4:18 *84*
4:19 *106*
5:1 *108*
5:9–13 *97*
5:10 *98*
5:11–13 *60*
5:11 *98*

**3 Yohana**
2 *140*

**Yuda**
6 *123*

**Ufunuo**
1:5–6 *106*
2:5 *68*
2:16 *68*
2:21 *68*
3:3 *68*
4:8 *12*
4:11 *12*
5:9–10 *106*

*Ufunuo*
5:11–14 *35*
20:11–15 *55, 119–20, 122, 130*
20:11 *130*
20:12 *121, 130*
20:13 *123*
20:15 *130*
21:27 *130*
22:14–15 *124*

**OTHER ANCIENT LITERATURE**

**Lucretius**
*De Rerum Natura*
Kitabu 1 82

**Other books by David Gooding**
(published by Myrtlefield House)

*The Riches of Divine Wisdom* (NT use of OT)
*According to Luke* (The Third Gospel)
*In the School of Christ* (John 13–17)
*True to the Faith* (Acts of the Apostles)
*An Unshakeable Kingdom* (Letter to the Hebrews)
*How to Teach the Tabernacle*
*Windows on Paradise* (Gospel of Luke)

**Other books by John Lennox**

*God and Stephen Hawking: Whose Design Is It Anyway?*
(Lion, 2011)
*God's Undertaker: Has Science Buried God?*
(Lion, 2009)
*Gunning for God: A Critique of the New Atheism*
(Lion, 2011)
*Miracles: Is Belief in the Supernatural Irrational?*
VeriTalks Vol. 2. (The Veritas Forum, 2013)
*Seven Days That Divide the World* (Zondervan, 2011)

**Vitabu vinavyosaidia kuelewa imani**

# Imani yetu Ndiyo Ushindi

*Hans Legiehn*

Kurasa 216

Biblia inasema nini kuhusu Mungu, Ulimwengu, Dhambi, Wokovu, Kanisa, Mambo Yajayo, Maandiko Matakatifu.

Mafundisho ya msingi kuhusu imani ya Kikristo yakielezwa katika mafungu saba. Kitabu hiki kinafaa sana kwa kujifunza maneno makuu ya Neno la Mungu. Kinatoa mwanga mkali kwa kuonesha njia ya wokovu katika Biblia.

# Panorama ya Biblia

Migawo saba ya nyakati za Historia ya Wokovu; ikioneshwa na kuelezwa katika michoro 12 ya rangi.

*Panorama ya Biblia* inataka kuchora picha ndefu ioneshayo taratibu zote za matendo ya Mungu ya kumwokoa mwanadamu; katika mazingira mbalimbali ya nyakati zilizopita, wakati huu na ujao. Ramani za rangi zinamsaidia msomaji wa Biblia kuelewa na kueleza mfululizo wa historia katika Biblia.

Vitabu vyote vinapatikana kutoka kwa

**Kanisa la Biblia Publishers**

**P. O. Box 1424**

**Dodoma Tanzania**

**www.klb-publishers.org**

# Kuhusu Waandishi

**David W. Gooding** ni Profesa Mstaafu wa Kiyunani cha Agano la Kale katika Chuo Kikuu cha Malkia (Queen's University), Belfast, Ireland ya Kaskazini na yeye ni mwanachama wa Royal Irish Academy. Aliandika vitabu vinavyofafanua Injili ya Luka, Matendo ya Mitume na vitabu vingine.

**John C. Lennox** ni Profesa wa Mathematics katika Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza. Anafahamika katika nchi nyingi kwa kuleta michango mikubwa katika nyanja za sayansi, falsafa na dini. Yeye ni Mkristo anayejadili kwenye midahalo kuhusu suala la kuwepo kwa Mungu au la.